Nipashe
Ijumaa Agosti 9, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579992
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Shein apigia debe lugha ya Kiswahili kwa SADC

UKURASA 2


UCHUMI
Viuatilifu vyakwamisha ulimaji pamba Malinyi
Ukurasa 19
BUFE
Ijumaa Agosti 9, 2019
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Mrajisi: Huu ndio Ushirika, umesimama 'damudamu' na sekta kilimo
Ukurasa 16
KILIMO NYANDA ZA JUU KUSINI
Watafiti TARI walivyofungua kilimo darasa zawadi kuu kwa Nanenane
Ukurasa 14
UCHUMI Ukurasa 18
Biashara katika picha Ukurasa 17

UKURASA 13

# Mikopo elimu ya juu inavyogeuka shubiri

**WANUFAIKA** walalamika deni kuongezeka kila mwaka. Kati ya 480,000 waliokopeshwa, 11,000 tu wafanikiwa kumaliza deni miaka 25... *Endelea ukurasa wa 2*


Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitazama ng'ombe wa kisasa, alipotembelea banda la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) Kitaifa kwenye uwanja wa Nyakabindi, mkoani Simiyu, jana. Wa pili kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Tellak. **PICHA: OWM**

## Waziri Mkuu aagiza ripoti timu ya mawaziri migogoro ya ardhi

UKURASA 2


### YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**LUKUVI AWASIMAMISHA KAZI MAOFISA 183 ARDHI**
WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amepitisha fagio la chuma wizarani...

**UKURASA WA 4**

**12 MATATANI UMILIKI KAMPUNI ZA KUBADILI FEDHA BILA KIBALI**
JESHI la Polisi mkoani Tanga, linawashikilia wafanyabiashara 12 kwa tuhuma za kumiliki...

**UKURASA WA 4**

**WANUNUZI PAMBA WAHIMIZWA KASI**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wanunuzi wa pamba katika maeneo mbalimbali nchini...


## Fatma Karume aibuka udukuzi

UKURASA 3

MICHEZO
YANGA: WALETENI, TUMEIVA UK. 32
MAONI, KATUNI UK.6

# Waziri Mkuu ataka ripoti timu mawaziri wanane

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Kassimu Majaliwa, amewaagiza mawaziri wanane waliopewa kazi ya kutembelea maeneo yenye migogoro ya wakulima, wafugaji na wahifadhi, kukamilisha taarifa ili changamoto hiyo imalizwe mapema.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana mkoani Simiyu katika maadhimisho ya kitaifa ya maonyesho ya Nanenane.

"Pamoja na mafanikio kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, Sekta ya kilimo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ikiwamo ukame, milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mazao, teknolojia duni za kilimo na uhifadhi wa mazao na migogoro ya wakulima na wafugaji, migogoro ya wafugaji na wahifadhi," alisema.

Majaliwa alisema serikali imeendelea kuzitatua changamoto hizo na kwamba migogoro kati ya wafugaji na mipaka ya hifadhi tayari imeifanyiwa kazi.

"Tumeifanyia kazi kwa kuteua timu ya mawaziri wanane kwenye sekta zinazogusa maeneo hayo kuyatembelea yote yanayolalamikiwa, ninawahakikishia migogoro hiyo inafanyiwa kazi.

"Wanakamilisha taarifa, tunataka kuimaliza kabisa. Wito wangu kwa mawaziri mliohusika kwenye hili, harakisheni mchakato huo ili wakulima na wafugaji wanaoishi kandokando ya hifadhi wajue hatima ya kazi zao, nataka tuwaeleze mipaka ipo wapi," aliagiza.

Alisema lengo ni kuona uwezekano wa baadhi ya hifadhi kupunguzwa ukubwa wake pale ambako wanaona hakuna tija ili wananchi waendeleze maeneo hayo kwa shughuli za ufugaji na kilimo. Kuhusu zao la pamba, Majaliwa alisema serikali kupitia Benki Kuu (BoT) imewaunganisha wanunuzi na wenye benki ili waweze kupata fedha za kununua pamba kutoka kwa wakulima.

Alisema soko la pamba limekumbwa na changamoto ya ununuzi lakini kuanzia Jumatatu, wakulima watakuwa wanafurahia matunda ya jasho lao.

Majaliwa alisema baadhi ya wanunuzi wameshakwenda kwenye vituo vya ununuzi ili kuinunua pamba na serikali imeanza kupata taarifa za vituo kulipa pamba iliyokuwa vituoni kwanza.

Kuhusu sekta ya uvuvi, Majaliwa alimwagiza waziri mwenye dhamana kuhakikisha elimu zaidi inatolewa kwa wavuvi ili kuondoa migongano kati yao na serikali na iandae mpango maalum wa aina ya nyavu zinazotakiwa kutumiwa wakati wa kuvua.

# Mikopo elimu ya juu inavyogeuka shubiri

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wamelalamika kuhusu kile wanachokiita uonevu katika marejesho ya mikopo hiyo.

Miongoni mwa masharti yanayolalamikiwa na wanufaika wa mikopo hiyo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ni deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka kunakosababisha ugumu wa kumaliza kulilipa. Takwimu za HESLB zinaonesha kati ya Watanzania 479,779 waliopatiwa mikopo hiyo tangu serikali ilipoanza kuitoa mwaka 1994, ni wanufaika 11,214 (asilimia 2.3) waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao.

Akiwa mjini Shinyanga juzi, Kashinje Emmanuel (33), mmoja wa wanufaika wa mikopo hiyo, aliiambia Nipashe kuwa alitarajia kumaliza kulipa mkopo wake ndani ya kipindi cha miaka 18, lakini ameshangaa kuona deni linaongezeka kila mwaka ilhali ameshaanza kulilipa tangu mwaka 2015.

"Mimi nilisoma Udom (Chuo Kikuu cha Dodoma) 2009-2012. Bodi (HESLB) ilinipa jumla ya Sh. milioni 8.04, wakati naanza kulipa mwaka 2015, deni lilikuwa limefika Sh. milioni 12 maana tayari walikuwa wameshanipiga penalti na tozo nyingine.

"Nikaanza kulipa kwa kukatwa Sh. 56,000 kila mwezi kwenye mshahara wangu na nikajipa matumaini kwamba deni lingemalizika ndani ya miaka 18.

"Kilichonishangaza ni kwamba licha ya kuanza kulipa, deni halipungui kwa kiasi kikubwa, linapungua kidogo sana, (HESLB) wanaongeza asilimia sita kila mwaka, ni ngumu kwangu kulimaliza kama mshahara wangu utaendelea kuwa hivi," alisema mwalimu huyo wa Shule ya Sekondari Com iliyoko mjini Shinyanga. Mnufaika mwingine wa mikopo hiyo, Fortunata Ntwale, aliiambia Nipashe jijini Dar es Salaam jana kuwa naye anaumizwa na kuongezeka kwa deni hilo kwa asilimia sita kila mwaka pamoja na makato makubwa yanayofanyika katika urejeshaji wa mkopo baada ya Bunge kupitisha marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Novemba 2016, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2016, ambao pamoja na mambo mengine, ulipendekeza kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili mnufaika wa mkopo arejeshe mkopo kwa makato si chini ya asilimia 15 ya mshahara wake wa kila mwezi badala ya asilimia nane ya awali.

"Mimi nilisoma sheria pale UDSM (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) 2011-2014, nimeanza kurejesha mkopo mwaka huu. Kwa kweli makato ya asilimia 15 ya mshahara ni makubwa sana. Anayeomba mkopo huo kwa sasa inabidi afikiri mara mbili maana hata ajira zenyewe ni shida.

"Kibaya zaidi, unapigwa penalti kama hutalipa deni mapema baada ya kuhitimu masomo. Hata ukiwahi kuanza kulipa, bado deni linaongezeka kwa asilimia sita kila mwaka, na kuna makato mengine

INAENDELEA UK.8



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akimsikiliza Mkurugenzi wa Biashara ya Shirika la Air Tanzania, Patrick Ndekama(wa tano kulia), alipotembelea banda la maonesho la shirika hilo, kabla ya kufunga wiki ya nne ya Maonesho ya Viwanda ya SADC, katika viwanja vya Ukumbi wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Shein asafisha njia ya Kiswahili SADC

**Gwamaka Alipipi na Beatrice Moses**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuna haja Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi za mawasiliano katika majukwaa ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Amesema anaamini hatua hiyo itaimarisha umoja na mshikamano kwa wanachama wa jumuiya hiyo na kukuza shughuli za biashara na viwanda.

Dk. Shein aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana wakati akifunga maadhimisho ya Maonyesho ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya SADC.

"Historia inatuonyesha Kiswahili kimeweza kuwaunganisha Watanzania kuwa wamoja, licha ya kwamba Watanzania wanazo lugha tofauti za makabila mbalimbali.

"Kiswahili kimekuwa na mchango mkubwa katika harakati za ukombozi wa Afrika. Hivi sasa, Kiswahili kimerahisisha mawasiliano na kukuza biashara katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na tayari Umoja wa Afrika (AU) umekikubali Kiswahili kiwe ni lugha rasmi.

"Kwa hivyo, wazo la kukifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi za SADC ni muhimu na vyema tukaungana katika kulifanyia kazi suala hili," alisema.

Rais Shein pia alizitaka nchi za SADC kuendeleza viwanda, kununua na kuzipenda bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya jumuiya hiyo.

Alizitaka kujenga utamaduni wa kuwapenda na kuwatumia wataalamu wazawa na kuondokana na utegemezi wa wataalamu kutoka nje, sambamba na kujenga misingi imara ya kuendeleza teknolojia asilia.

"Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kuhakikisha kwamba kila mmoja wetu anaunga mkono utelekezaji wa maazimio yaliyopitishwa katika vikao vilivyofanyika pamoja na mikakati ya serikali zetu zote ya kuendeleza viwanda kwa kununua na kuzipenda bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu wenyewe," alisema.

Rais Shein alisema kwa kufanya hivyo ni kutafsiri kwa vitendo dhamira ya nchi za SADC kuunda umoja kwa ajili ya kuongeza fursa ya masoko na ajira.

Alisema nchi hizo zitaweza kuongeza masoko na ajira ikiwa zitanunua bidhaa zinazozalishwa na viwanda kutoka jumuiya yao wenyewe na vinavyoendeshwa na wataalamu wazalendo.

Alisema nchi za SADC zinatakiwa kuongeza ubora wa bidhaa za viwandani ili ziweze kushindana na zile ambazo watu wengine hupenda kuzinunua.

Alisema kunapaswa kutengenezwa kwa bidhaa zenye ubora katika utengenezaji na ubunifu wa hali ya juu utakaoweza kuwavutia wanunuzi wengi.

Rais Shein pia alisema katika utafutaji wa masoko, nchi za SADC zinapaswa kuweka mkazo katika Technolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokana na utandawazi.

HABARI KITAIFA

# Fatma Karume afunguka udukuzi wa mawasiliano

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu wa Chama cha Wanasheria (TLS) na wakili wa kujitegemea, Fatma Karume, amezishauri kampuni za mawasiliano ya simu nchini kuwalinda watumiaji wao dhidi ya udukuzi wa taarifa binafsi.

Amesema kampuni hizo zinao wajibu wa kuchukua hatua madhubuti pale inapobainika taarifa za mteja kudukuliwa na kusambazwa katika mitandao ya kijamii.

"Kampuni za simu zina wajibu wa kuchukua hatua kulinda wateja wao kwa kuwa wao wana mkataba na wateja na madhara ya udukuzi si kwa wadukuaji, bali ni kwa kampuni na wateja," Fatma alisema katika mahojiano na moja ya vituo vya televisioni jijini Dar es Salaam juzi.

Wakili huyo alisema si jambo jema taarifa binafsi za watu kuwekwa hadharani na kama italazimika kufanyika hivyo, basi ni muhimu pakawapo na utaratibu wa kisheria ili kuepuka kukiukwa kwa haki za msingi za wateja. "Tukumbuke huu udukuzi ulianza na nani? Unakumbuka (Freeman) Mbowe (Mwenyekiti wa Chadema) 'telephone conversation' (mawasiliano ya simu) na Wema Sepetu, ulianza pale Watanzania tukawa tunacheka hee hee hee.

"Tunamcheka Mbowe, wakatoka pale wakamwingilia Nape (Nnauye-Mbunge wa Mtama) na (Abdulrahman) Kinana (Katibu Mkuu mstaafu wa CCM).

"Walipomaliza na hapo, wakaingilia January (Makamba) na babaake (Yusuph Makamba), walipomaliza wakaja kwa (Benard) Membe na mtu mwingine.

"Unasikiliza January Makamba anaongea na Yusuph Makamba, mtoto na baba, hii siyo sawa hata kidogo," Fatma alisema.

Wakili huyo aliongeza kuwa ni muhimu nchi kutunga sheria itakayodhibiti udukuzi wa mawasiliano ya watumiaji wa mitandao ya simu isipokuwa kwa matakwa maalum ya kisheria na sababu zinazojitosheleza za kufanya udukuzi huo.

Hivi karibuni, kulivuja mawasiliano ya simu yaliyodaiwa kuwa na sauti za viongozi wastaafu wa CCM. Mawasiliano hayo yalisambazwa kwenye mitandao ya kijamii, huku mmoja wao akikiri sauti iliyodukuliwa ni yake na anawafahamu waliofanya hivyo ingawa hawezi kuwataja kwa kile alichoeleza kuwa ni sababu za kimaadili.

Kuvuja kwa sauti hizo pia kuliwaibua watetezi wa haki za binadamu ambao waliitaka serikali kutunga sheria kulinda taarifa binafsi ili kuepusha ukiukwaji wa haki ya faragha.

Ibara ya 16 ya Katiba ya Tanzania inaeleza kuwa kila mtu anastahili kuheshimiwa na faragha yake kulindwa, na mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali hii namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha yaweza kuingiliwa bila ya kuathiri ibara hiyo.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa shamba la miwa Kilombero, Mohamed Salum, wakati alipotembelea mabanda ya maonyesho katika kilele cha Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane mkoani Morogoro jana. **PICHA: OMR**

# Lukuvi awasimamisha kazi maofisa 183 ardhi

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amepitisha fagio la chuma wizarani kwake baada ya kuagiza kusimamishwa kazi kwa maofisa 183 wa wizara hiyo kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili.

Maofisa hao wanatuhumiwa kuingilia mfumo wa kukadiria na kukusanya kodi ya pango la ardhi kinyume na taratibu na kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.

Katika taarifa ya wizara hiyo iliyotolewa juzi usiku, Lukuvi alimwelekeza Katibu Mkuu wa wizara hiyo kuwasilisha majina ya maofisa hao kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ili uchunguzi uanze mara moja.

Wengi wa waliotumbuliwa ni maofisa ardhi wa wilaya, maofisa ardhi wasaidizi wa wilaya, wahasibu, wataalamu wa teknolojia ya mawasiliano (IT), wathamini wa ardhi, makatibu muhtasi, maofisa ardhi wateule na watunza kumbukumbu.

Katika sakata hilo wengine waliokumbwa ni watunza fedha na maofisa kutoka makao makuu ya wizara hiyo.

Alipoulizwa kama majina hayo yameshawasilishwa Takukuru, Meneja Mawasiliano wa taasisi hiyo, Doreen Kapwani, alisema jana ilikuwa sikukuu hivyo ni vyema atafutwe leo kwa ajili ya ufafanuzi.

"Leo ni sikukuu kwa hiyo suala hilo hakuna wa kufuatilia ila kesho ni siku ya kazi hivyo ukinitafuta nitakupa maelezo kwa sababu hata hiyo taarifa unayosema sijaiona," alisema.

Jitihada za kumpata Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Diwani Athumani, kujua kama majina hayo yameshawasilishwa mezani kwake ziligonga mwamba kwani simu yake ilikuwa inaita muda wote bila kupokelewa.

## Adaiwa kuchinja mke, kujinyonga hadi kufa

**Na Mohabu Dominic, GEITA**

MKAZI mmoja mkoani Geita, ameua mkewe kwa kumchinja, kisha na yeye kujinyonga.

Tukio hilo lilitokea katika kijiji cha Nyakayenze Kata ya Busonzo wilayani Bukombe mkoani Geita.

Diwani wa Busonzo, Nicas Safari Mayala, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea usiku wa kuamkia Jumanne.

Diwani huyo aliwataja marehemu kuwa ni William Zanzibar (23) anayedaiwa kumchinja mkewe, Matisho Mahilan (20) kwa kutumia kitu chenye ncha kali shingoni kisha na yeye kujinyonga hadi kufa.

Tukio hilo tukio linadaiwa kuibua majonzi na simanzi kubwa kutokana na wawili hao kuacha mtoto mdogo.

Diwani Mayala aliwaomba viongozi wa dini na kisiasa kutoa elimu kwa jamii kupunguza matukio ya aina hiyo ya kujichukulia sheria mkononi.

Aliongeza kuwa matukio ya kujichukulia sheria mikononi licha ya kuathiri familia, pia yanapoteza nguvukazi ya Taifa kwa kuzingatia wote walikuwa bado vijana.

Katika tukio la pili lililotokea katika Kijiji cha Luezela wilayani Geita, ambapo mwanamke Laulensia Tibasima Kadadi (50) anadaiwa kujinyonga kwa kutumia kitenge chake usiku wa kuamkia juzi.

Akizungumzia tukio hilo kwa wanahabari Samson Kachimu, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lwezela, alisema jana kuwa mwili wa marehemu uligunduliwa na familia asubuhi yake.

Kuhusu chanzo cha kifo hicho, Kachimu alisema ni siku chache baada ya Tibasima apimwe na kubainika alikuwa na maradhi.

Hata hivyo, alisema alipatiwa matibabu, lakini hakupata nafuu, hivyo inawezekana sababu hizo zikawa chanzo cha kuchukua uamuzi huo.

Kila mara pamoja na kupata tiba, lakini hali yake ilikuwa bado akiendelea kuugua kila mara huenda hali hiyo imechangia kufikia maamuzi hayo.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Dismas Kisusi, alithibitisha kutokea kwa tukio la mume kuua mke kisha naye kujinyonga.

Hata hivyo, huhusu tukio la pili la Tibasima kujinyonga, Kamanda Kisusi alisema atafuatilia na kulitolea ufafanuzi zaidi.

**Akizungumzia tukio hilo kwa wanahabari Samson Kachimu, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lwezela, alisema jana kuwa mwili wa marehemu uligunduliwa na familia asubuhi yake.**

HABARI KITAIFA

# 12 matatani umiliki kampuni za kubadili fedha bila kibali

**Na Dege Masoli, TANGA**

JESHI la Polisi mkoani Tanga, linawashikilia wafanyabiashara 12 kwa tuhuma za kumiliki kampuni za kubadilisha fedha bila kufuata taratibu za kisheria.

Kwa mujibu wa sheria ya fedha, wanatakiwa kuwa na kibali cha Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Leons Rwegasira, alisema jana kuwa wafanyabiashara hao walikamatwa kwenye operesheni ya kushtukiza iliyofanywa na Jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vya usalama wakiwamo maofisa wa Hazina.

Alieleza kuwa mbali na watu hao, pia kuna fedha za Kitanzania na za kigeni walizokamatwa nazo pamoja na madini, kemikali na noti bandia.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, fedha za Kitanzania walizokutwa nazo ni Sh. milioni 63.3, na fedha za kigeni na thamani yake kwa fedha ya Kitanznaia kwa viwango vya kubadilishia fedha siku ya jana kwa mujibu wa Conveter, ni Dola za Marekani 65,961 (sawa na Sh. milioni 151.7), fedha za Kenya Sh. 236,549 (sawa na Sh. milioni 5.3).

Nyingine ni Paundi 400 (sawa na Sh. milioni 1.1) na Euro 270 (sawa na Sh. 694,884), Rupia zipatazo 1,349, fedha ya Afrika Kusini Rand 1,020 (sawa na Sh.154,810), fedha ya Oman Rial 521 (sawa na Sh.milioni 3.1) na Uganda ni Sh 2000 (sawa na Sh. 1,246).

Aidha, alieleza tuhuma nyingine zinazowakabili ni kukutwa na madini na kemikali ambazo hazijabainika ni za aina gani na matumizi yake.

Kamanda huyo alisema pia watuhumiwa hao wamekutwa na fedha bandia. Aidha, aliwataka watu wanaotaka kufanya biashara hiyo kufuata taratibu za kisheria ikiwamo kuwa na vibali kutoka BoT ili kuepukana na kuingia kwenye makosa ambayo yatawafanya kuharibu mfumo wa maisha yao.

"Tunataka watu wafuate sheria inayowataka kusajiri kampuni zao BoT na kuingia kwenye utaratibu wa kulipa kodi ya serikali, vinginevyo hawatakuwa salama kwani Jeshi la Polisi halitamvumilia mtu yeyote atakaekwenda kinyume cha sheria," alisisitiza Rwegasira.



Mchuuzi wa mboga za majani, akipeleka kuuza kwa bei ya jumla katika Soko la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. Mboga za majani zina faida nyingi za kiafya kwa binadamu, kutokana na asili yake ya kuwa na vitamini kwa wingi, madini kwa wingi, kukinga mwili kwa magonjwa mbalimbali na kurekebisha na kuweka uzito sawa. **PICHA: MIRAJI MSALA**




## Waziri Mkuu ataka kasi ununuzi pamba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wanunuzi wa pamba katika maeneo mbalimbali nchini wahakikishe wanaongeza kasi ya ununuzi wa zao hilo ili wakulima waweze kupata fedha zao kwa wakati.

Pia Waziri Mkuu amemwagiza Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga pamoja na Manaibu Waziri wake kubaki katika mikoa yote inayolima zao la pamba hadi wakulima wote watakapolipwa fedha zao na kuhakikisha pamba yote iliyomo mikononi mwa wakulima inauzwa.

Alitoa maelekezo hayo jana alipotembelea Chama cha Msingi cha Itemelo kilichoko eneo la Dutwa wilayani Bariadi, Mkoa wa Simiyu kwa ajili ya kujionea mauzo ya pamba.

Waziri Mkuu alisema ataendelea kusimamia mwenendo wa zao hilo kwa ukaribu lengo likiwa kuona wakulima wananufaika kwa kupata tija. Alisema serikali inataka kuona pamba yote iliyoko kwa wakulima inatoka ili wakulima waweze kulipwa fedha ambazo zitawawezesha kujikimu kimaisha pamoja na kununua pembejeo kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwataka viongozi wa AMCOS wahakikishe wanawatambua wakulima kwa majina, maeneo wanayoishi pamoja na ukubwa wa mashamba yao ili waweze kuagiza pembejeo kulingana na mahitaji halisi. Hata hivyo, Waziri Mkuu aliwasihi wakulima kufungua akaunti katika taasisi mbalimbali za kifedha, lengo likiwa ni kuhifadhi vizuri fedha wanazozipata kutokana na mauzo ya pamba ili ziweze kuwasaidia baadaye.

Pia Majaliwa aliwasisitiza wakulima hao waendelee kutunza vizuri pamba yao na kuipeleka ghalani ikiwa katika hali nzuri ya usafi na ubora wa hali ya juu, kwani kwa sasa pamba ya Tanzania inasifika kwa ubora katika soko la dunia. Kwa upande wa masoko hususan ya pamba, aliwasisitizia wananchi wa Dutwa na Watanzania kwa ujumla kuwa serikali inaendelea kuhakikisha uwapo wa masoko ya uhakika wa mazao yote hususan ya kimkakati. Waziri Mkuu aliongeza kuwa moja ya ajenda muhimu ya ziara yake ya kiserikali aliyoifanya nchini Misri Julai 2019, ilikuwa ni kutafuta masoko ya uhakika ya mazao ya Tanzania likiwamo na zao la pamba.

Naye Waziri Hasunga alisema hali ya malipo kwa wakulima wa pamba kwa sasa ni ya kuridhisha kwa kuwa wakulima katika maeneo mbalimbali wameanza kulipwa.

## Hatima maombi ya askofu kujulikana leo

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya kusikilizwa maombi ya Askofu Mulilege Kameka wa Kanisa la House of Prayers Shield of Faith Christian Fellowship dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ya kutaka Kamishna Mkuu wa Uhamiaji kwenda kujieleza mahakamani kwa kuidharau amri ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kujulikana leo.

Mapema Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam iliamuru Kamishna Uhamiaji kumwachia huru Askofu Kameka baada ya kujiridhisha kwamba ni raia wa Tanzania.

Uamuzi huo unatarajiwa kutolewa leo mbele ya Jaji Dk. Atuganile Ngwala, baada ya kusikiliza hoja za pingamizi la awali la AG na majibu ya mlalamikaji.

Pingamizi la AG liliwasilishwa na Mawakili wa Serikali Jakline Nyanyori na Tuli Helela ambao walidai kwa nyakati tofauti kwamba mlalamikaji amewasilisha maombi yake chini ya kifungu ambacho hakiipi mahakama hiyo mamlaka ya kuyasikiliza.

Nyantori alidai kuwa kwa mujibu wa hati ya maombi hayo, mlalamikaji ameegemea kifungu cha 392 (A), na 114 A (b) wakidai kwamba kifungu cha 114 kinatengeneza kosa la jinai.

Hata hivyo, walidai mlalamikaji alipaswa kufuata matakwa ya kifungu cha 9 cha ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) ikiwamo kulalamika rasmi polisi au mahakamani ili itengenezwe hati ya mashtaka na mashahidi wangeitwa kuthibitisha kosa hilo.

Askofu huyo kupitia kwa wakili wake John Malya, amewasilisha mahakamani hapo maombi ya kutaka Kamishna Mkuu wa Uhamiaji kwenda kujieleza kwanini asifungwe kwa kukiuka amri halali ya mahakama ya kumwachia huru askofu huyo.

Awali Askofu huyo alituhumiwa kwamba si raia wa Tanzania, lakini mahakama hiyo ilisikiliza na kutoa hukumu kwamba imejiridhisha kuwa ni Mtanzania, lakini mpaka sasa yupo mahabusu katika Gereza la Segerea.

Mahakama hiyo iliyoketi Machi 8, mwaka huu, iliamuru kuwa askofu huyo ni raia halali wa Tanzania ambaye ni mzaliwa wa Kijiji cha Maenje wilayani Mbozi mkoani Songwe.

Mahakama hiyo iliagiza askofu huyo atolewe mahabusu ndani ya siku mbili na mwenye pingamizi afuate taratibu za kisheria.

# Wakulima sasa kulipwa kwa wakati kupitia mfumo TMX

**Na Mwandishi Wetu**

CHANGAMOTO ya ucheleweshwaji wa malipo kwa wakulima baada ya kuuza mazao yao inatarajiwa kuwa historia baada ya Serikali kuzindua mfumo wa uuzaji wa mazao kupitia Soko la Bidhaa (TMX), ambao kuanzia mwaka ujao utaanza kutumika kununua na kuuza baadhi ya mazao ndani na nje ya nchi.

Ununuzi wa mazao ya wakulima kupitia Soko la Bidhaa unalenga kuongeza ufanisi katika mifumo ya masoko ambayo imekuwa na changamoto kwa muda mrefu kwa kuwaunganisha wauzaji na wanunuzi wa bidhaa, kuleta ushindani kwenye bei, kupunguza gharama na kuweka uwazi.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alizindua mfumo huo jana katika kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane kitaifa kwenye Viwanja vya Maonesho Nyakabindi mkoani Simiyu kwa niaba ya Rais John Magufuli.

Waziri Mkuu alisema mfumo huo utawahakikishia wakulima upatikanaji wa malipo kwa muda mfupi na wanunuzi kuwa na uhakika wa kupata mazao na bidhaa zenye ubora na zinazotosheleza mahitaji yao.

"Baadhi ya mazao tunayotarajia kuanza nayo ni pamoja na dengu, choroko, mbaazi, ufuta, korosho, kahawa na kokoa. Mfumo huu utasaidia upatikanaji wa masoko ya uhakika na kwa uwazi na hivyo kuifanya nchi ijulikane kimataifa juu ya uzalishaji wa mazao hayo na mengine," alisema.

Pia, alisema katika kuhakikisha mafanikio yanapatikana kwenye sekta za kilimo, viwanda na biashara ni lazima soko la bidhaa lipewe ushirikiano kwenye ngazi zote kuanzia wizara, mikoa na halmashauri za wilaya ili mazao ya kimkakati pamoja na yale yenye changamoto ya masoko yauzwe kupitia soko hilo muhimu.

"Taratibu zote za uendeshaji wa biashara hiyo zikamilike kwa ushirikiano wa vyama vya ushirika, TAMISEMI, Wakala wa Stakabadhi Ghalani na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha na Mipango.

Pia elimu kwa wadau wote itolewe kwa muda wote ili kuwaandaa washiriki wa mnyororo mzima wa thamani za mazao," alisema.

Alisema Soko la Bidhaa Tanzania ni taasisi iliyoanzishwa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Bidhaa ya mwaka 2015 na Kanuni za Masoko ya Bidhaa za mwaka 2016.

INAENDELEA UK. 8

# Wagonjwa wa figo SADC kupokelewa

**Na Beatrice Moses**

TANZANIA inatarajiwa kuongeza kupokea idadi ya wagonjwa watakaoletwa kutibiwa nchini kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), baada ya kufanikiwa kuboresha na kuanzisha huduma za kisasa ikiwamo upandikizaji wa figo.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wakati akizungumza jana kwenye ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alibainisha kuwa kupitia maonyesho hayo, sekta ya afya imepata fursa ya kuonyesha kuwa Tanzania sasa inakuwa nchi ya utalii wa kimatibabu na kupitia huduma za kisasa zinazotolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Alitaja huduma hizo ni upandikizwaji wa figo, vifaa vya kusikia kwa watoto na kutibu kwa kutumia radioloji unaofanywa kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Alisema huduma hizo awali zilikuwa hazipatikani nchini wala katika nchi za SADC, zaidi ya Afrika Kusini inayotoa upandikizaji wa figo, lakini nyingine hazijaanza, hivyo Tanzania inapata fursa

INAENDELEA UK. 8


## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## TAARIFA KWA UMMA

## TAHADHARI YA UWEPO WA MATAPELI KWA WATEJA WA TMDA

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inapenda kuwatahadharisha wateja wake kuwa wamejitokeza watu ambao hujifanya kuwa ni watumishi wa TMDA na kuonesha nia ya kuwasaidia wateja wanaohitaji huduma kwa lengo la kuwatapeli.

2. Watu hao ambao ni matapeli wamekuwa wakiwasumbua wateja kwa njia ya simu za mkononi wakiwataka kuonana nao nje ya Ofisi na katika muda ambao si wa kazi au kuwataka watume pesa kwa njia ya simu ili huduma walizoomba zifanyiwe kazi kwa haraka.

3. TMDA kupitia ofisi ya Makao Makuu na Ofisi zake za Kanda, inapenda kuutarifu umma kuwa huduma zote zitolewazo na TMDA hazitolewi kwa kificho au nje ya Ofisi za TMDA, hivyo inapotokea mtu anakushawishi akupe huduma kwa utaratibu tofauti na ulioainishwa hapo juu, tafadhali toa taarifa mara moja katika Ofisi zetu za Makao Makuu na Kanda. Hivyo watu wenye kuonesha dalili za kutaka kutoa msaada kwa kujificha au nje ya Ofisi za TMDA sio watumishi wa Mamlaka.

4. Kwa taarifa hii, wateja wote wa TMDA mnaelekezwa kupata huduma kutoka kwa watumishi wenye vitambulisho halali na waliopo katika ofisi zetu tajwa hapo juu au Kituo cha forodha na kwamba malipo yote ya ada na tozo kwa huduma zitolewazo yanatakiwa yafanyike kupitia benki au mawakala waliothibitishwa wa benki husika baada ya kupatiwa ankara kifani (Profoma invoice) na Namba ya Malipo ya Serikali (Control Number).

5. Kwa maelezo zaidi unaweza kuwasiliana nasi kupitia ofisi za TMDA Makao Makuu au Ofisi za Kanda zilizopo Dar Es Salaam, Mwanza, Simiyu, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mtwara na Tabora au kupiga simu bila malipo kupitia **Na. 0800110084.**

**Imetolewa na:**

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),**
**Mtaa wa Mwanza, Kitalu T, Kiwanja Na.6**
**S.L.P 1253, Dodoma Au**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751**
**Simu bila Malipo: 0800110084**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nanenane ilete uwekezaji zaidi

**NANENANE** ilihitimishwa jana, lakini jukumu la kuendeleza kilimo, ufugaji na uvuvi ndiyo kwanza linaanza.

Maadhimisho hayo ya Nanenane yameendelea kutudhihirishia kuwa kilimo si tu kuwa ni mhimili wa uchumi bali pia ni msingi wa afya ya Watanzania, hivyo kunahitajika uwekezaji zaidi kwenye kilimo.

Bajeti ya kilimo inayopangwa iakisi ukweli kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa na kama ulivyo uti wa mgongo wa binadamu hakuna anyeruhusiwa kuuchezea.

Tunasisitiza kuwa ni lazima kuwekeza zaidi kwenye kilimo kwa kuwa wakulima wetu, wavuvi na wafugaji wametambua kuwa japo kwa miaka mingi kilimo hakikuhusishwa na biashara, leo wamejielewa na kufahamu kuwa kilimo ni biashara. Kujitambua huko ndiko kunakouhitaji zaidi mkono wa serikali.

Aidha, pamoja na kazi hiyo kufanywa na serikali kupitia maonyesho hayo ambayo hufanywa kitaifa, kikanda na kiwilaya kwenye maeneo mbalimbali nchini, uwekezaji wa kukiboresha na kukiimarisha kilimo unahitajika zaidi.

Hata hivyo, tunazipongeza taasisi za utafiti, masoko na uhamasishaji kwa kuwafungua wakulima, wavuvi na wafugaji macho na ambao sasa wametambua kuwa zamani kazi yao iliishia shambani na masuala mengine yangefanywa na ngazi nyingine za kiuchumi.

Ndiyo maana kupitia hamasa mbalimbali kama ilivyoonekana kwenye maonyesho hayo imethibitika kuwa wakati huu wakulima wanashindana miongoni mwao na wameanzisha viwanda vya kuongeza thamani mazao yao badala ya kuyatoa shambani, tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Kazi kubwa inayofanywa na serikali na wadau imetambulisha ukweli huo kuwa zama hizi kilimo ni biashara tena ni jukumu lenye tija zaidi duniani kwa kuwa ndicho chanzo cha chakula ambacho kila binadamu anakihitaji hivyo serikali imewahusisha na wavuvi na ufugaji tena kuwapa nafasi wazalishaji hao ili kuwa na uwanja mpana zaidi katika kuendesha shughuli zao.

Wakati Nanenane ikihitimishwa leo tunawapongeza wakulima na kuwatia moyo kuwa ndiyo tegemeo la kupatikana kwa chakula, malighafi kwa viwanda vya Tanzania na kwa ujumla ndicho kinachotegemewa kwenye kuusukuma uchumi wa nchi. Ikumbukwe kuwa serikali inapolenga kuanzisha viwanda ni wazi kuwa vingi vitategemea moja kwa moja malighafi kama maziwa, nyama, nafaka, pamba, miwa na mbegu za mafuta ili kuzalisha bidhaa muhimu za viwandani. Ndiyo maana inahitajika kuwekeza zaidi.


Aidha, kutokana na kusinyaa kwa soko la ajira rasmi, kilimo leo ni ajira si tu kwa wakulima bali pia kwa mamilioni ya Watanzania wakiwamo vijana na wazee. Hivyo ikihitaji serikali kuwa karibu zaidi na sekta hii.

Kwenye sekta ndiyo ndiko wanakoajiriwa madereva wa malori, wauzaji sokoni, ndiyo mhimili wa hoteli za nyota tano na viwanda mbalimbali ambavyo vimeunganishwa na kilimo, ufugaji na uvuvi. Tunaungana na kauli ya serikali kuanzia Tanzania ilipopata Uhuru hadi leo inayosisitiza kuwa kilimo ni mhimili na ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa taifa.

Kwa vile mazao kama kahawa, chai, korosho, ngozi, tumbaku, samaki na viungo vya aina mbalimbali vimeendelea kuwa chanzo cha fedha za kigeni. Pamoja na kuwa mhimili wa uchumi tungependa kuongeza kuwa kilimo ndiyo mhimili wa afya ya Mtanzania. Hii ni kwa sababu kutoka shambani, baharini na kwenye zizi la mfugaji kuna uhakika wa vyakula, kuanzia nyama, mboga, matunda, samaki na nafaka zinazoliwa na kuwapa wananchi afya.

Ndiyo maana tunaona kuwa serikali iongeze zaidi nguvu kwenye kilimo kwa kubuni teknolojia nyepesi, rahisi ili kukiboresha zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Bodaboda tumieni vijiwe vyema staili hii ya uchumi

**KATIKA** hili naomba nianze kuwa mtaaluma wa lugha kwa kuweka sawa nadharia yangu katika lugha, ili kuweka sawa msingi wa hoja tuelezane vizuri.

Nikipitia msingi huo, nianze kutoa maana ya kijiwe kwamba ni kitu gani? Niseme ni mkusanyiko wa watu wengi wanaojishughulisha na yote ya kuwaongezea kipato.

Vivyo hivyo, kijiwe ni mahali watu wanajikusanya na kujadili mambo mbalimbali yanayowahusu.

Hivyo mtu unapopita mitaani ni kawaida kukuta watu wamekaa katika ama mikusanyiko au aina fulani ya makundi katika sura ambayo yana malengo ya pamoja.

Niseme ni neno lililozoeleka kutamkwa na watu wanapowaona wenzao wamekusanyika katika maeneo hayo.

Katika hilo, nianze kuzungumzia maisha ya biashara za pikipiki aina ya bodaboda, kwamba ninaposema kijiwe cha bodaboda, ni ile sehemu ambayo bodaboda hujikusanya kwa kawaida wastani zaidi ya 10, kwa ajili ya kufanya biashara zao.

Vipo vijiwe ambayo vinamilikiwa na watu na wamekuwa wakipata fedha kupitia vijiwe hivyo. Baadhi ni kwamba, bodaboda wamejisajili na kuzipa majina, ili waweze kunufaika na mikopo ikiwamo kutambulika.

Hivi karibuni, madereva wa bodaboda wa wanaounda umoja uitwao 'Bodaboda Group' eneo la Mlimani City Jijini Dar es Salaam, wamezindua umoja wao ambao wanalenga kujiinua kiuchumi.

Mwenyekiti wao, Jafari Yahaya, anasema kikundi chao kilianzishwa tangu mwaka 2014 na kupata usajili mwaka jana na hadi sasa kina wanachama 25 waliofanikiwa kufungua akaunti na kuhifadhi zaidi ya shilingi milioni moja.

> **Anasema katika orodha hiyo, kila mwanachama kwa wiki anachangia fedha Sh. 20,000 zinazotunzwa benki. Anataja changamoto yao ni kwamba, madereva wa bodaboda hawaruhusiwi kufika maeneo ya mijini na mazingira muhimu ya biashara kama vyuo vikuu jirani.**

Anasema kufunguliwa kwa umoja huo, kumewasaidia kujenga mshikamano na kusaidiana katika shida, wakiishi katika mfumo kila mwana kikundi kwa siku anachangia zaidi cha Sh. 1000. Ni pesa anayopatiwa mwana kikundi anayeumwa.

Yahaya anasema, kuwapo matukio ya ajali katika sehemu za kazi, kikundi chao kimehakikisha kila mwana kikundi kimenufaika na kadi za matibabu, kwa maana ya bima za afya.

Anasema katika orodha hiyo, kila mwanachama kwa wiki anachangia fedha Sh. 20,000 zinazotunzwa benki.

Anataja changamoto yao ni kwamba, madereva wa bodaboda hawaruhusiwi kufika maeneo ya mijini na mazingira muhimu ya biashara kama vyuo vikuu jirani.

Ombi lake ni kwamba, serikali isiwazuie kwa sababu umoja huo una vitambulisho vyao maalum na anapaza sauti kwa wafadhili wajitokeze kuwasaidia, wapate eneo ambalo watakalolitumia kama shamba, kwa ajili ya kuwekeza shughuli zao za maendeleo.

Anataja changamoto nyingine wanayokumbana nayo, ni baadhi yao kutomiliki bodaboda, hivyo ni kilio kingine kinaviendea vyombo vya kuwakopesha.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Makongo, jijini Dar es Salaam Husina Hondo, anaahidi kuzifikisha changamoto hizo kwa mamlaka za juu, ili kuwapatia ufafanuzi mkubwa ambao ndio watazitolea majibu.

Mtendaji huyo amekipongeza kikundi hicho na kuvitaka vingine viige mfano wa kuweka akiba na kuwa na kadi za bima.

Alisema vikundi vikiwapo ni rahisi kupatiwa mikopo inayotolewa na serikali.

## BARUA & MJADALA

# Wakazi Malamba Mawili tukumbukwe kwa serikali kutupatia kituo cha polisi

*NDUGU Mhariri pole na majukumu ya kila siku kwa ujenzi wa taifa letu changa, na pia ninashukuru kupata nafasi katika gazeti lako ili niweze kutoa dukuduku langu.*

*Kwanza kabisa mimi ni mkazi wa Malamba Mawili, jijini Dar es Salaam, eneo hili linakabiliwa na ukosefu wa huduma mbalimbali za muhimu ikiwa ni pamoja na kituo kidogo cha polisi.*

*Tulikuwa tukitegemea kituo cha polisi cha Kwa Yusuf kilichokuwa kando ya barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, umbali wa zaidi ya kilometa mbili kutoka Malamba, lakini kimehamishiwa mbali zaidi baada ya bomoabomoa iliyofanyika kando ya barabara hiyo.*

*Kutokana na hali hiyo, tumejikuta tukiwa mbali zaidi na huduma za polisi, hivyo tukikumbwa na matatizo ambayo yanahitaji msaada wao inawezekana ikawa vigumu kuwapata kwa wakati kwa sababu ya umbali.*

*Kwa hali hiyo ndugu Mhariri, naomba zifanyike jitihada za makusudi za kuhakikisha eneo hili linapata huduma za polisi kuliko kutegemea maofisa wa polisi wale wa doria tu, ambao inawezekana likatokea tukio wakati hawapo eneo hili.*

*Nakumbuka sisi wakazi wa eneo hili tulikutana kwa ajili ya mkakati wa kutafuta aneo ambalo linaweza kutolewa ili kujenga kituo kidogo cha polisi ambapo eneo lilipatikana, lakini masharti yakawa ni magumu, hivyo ikashindikana kuwezesha ujenzi wa kituo hicho.*

*Kuna mtu alijitolea kutoa eneo, lakini ikaelezwa katika kikao kwamba siku hizi ili kujenga kituo cha polisi ni lazima eneo la kiwanja liwe kubwa, hivyo mpango wa ujenzi ukawa umeishia hapo kimsingi pamoja na mtu huyo kuwa tayari kutoa eneo lake.*

*Malamba Mawili kwa sasa imepanuka sana inahitaji kuwa na huduma hiyo, hivyo tunaomba ufanywe utaratibu ambao utasaidia kupata eneo la kutosha ili sisi wananchi tuchangie ujenzi.*

**Mkazi Malamba Mawili_ Dar**

**WASILIANA NASI:**
TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Kipindupindu kiwe jukumu binafsi, isiachiwe serikali tu




**Na Moses Ismail**

**NIANZE** kuzungumzia hili kwa kuzitalii takwimu zilizotolewa na Naibu Waziri wa Afya, Faustine Ndugulile, kwamba kufikia Juni 17 mwaka huu watu sita walishafariki kwa ugonjwa wa kipindupindu na wengine 391 wakiwa wamepata maambukizi ya ugonjwa huo na kupewa tiba.

Nionavyo mie idadi hii ya waliofariki na waliopatwa na maambukizi, inaweza kuonekana ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya wagonjwa na idadi ya watu waliofariki kwa ugonjwa huo kwa takwimu za miaka iliyopita.

Kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa mwaka jana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, katika kipindi cha mwezi wa Machi tu mwaka jana idadi ya wagonjwa wa kipindupindu ilikuwa ni watu 1,448 huku idadi ya vifo ikiwa ni 27 tu.

Ukilinganisha na idadi hii ya takwimu za Juni 17 mwaka huu, utaona kuna udhibiti mkubwa wa maambukizi ya ugonjwa huo pamoja na vifo vitokanavyo na madhara yake.

Hata hivyo, ugonjwa huo wa mlipuko una tabia ya kujirudia tena katika kila kipindi cha majira ya mvua za mwaka kwa kusababishwa na mifumo mibovu ya udhibiti wa mifumo ya maji machafu ambayo ndiyo chanzo kikuu cha ugonjwa huo.

Kwa tabia yake ya kujirudiarudia kwa majira hayo ya mvua kila mwaka, nategemea kuwa pengine idadi hii ya wagonjwa 391 na vifo vya watu 17 iliyotolewa sasa na Naibu Waziri, vinaweza kuongezeka na pia naomba Mungu aepushe hilo. Kwa mujibu wa maelezo ya matabibu ugonjwa huu, unaoweza kuua haraka, husababishwa na bakteria wanaofahamika kwa jina la kitaalamu kama vibrio cholera.

Ni bakteria wanaozaliwa na kuishi kwenye kinyesi cha binadamu na huwa hatari zaidi pindi mtu anapokunywa maji au chakula kilicho na bakteria hao.

Vilevile ugonjwa huu huambukiza kwa mtu kugusa matapishi au kinyesi cha mgonjwa wa kipindupindu bila ya kuwa na kizuizi.

Inashauriwa wenye kuwasaidia watu walioambukizwa ugonjwa huu nao wapatiwe dawa za kuwazuia kupata maambukizi.

Kwa miaka mingi serikali imekuwa ikitoa elimu ya watu kujikinga na ugonjwa huo kupitia wataalamu wake wa afya na kuendesha kampeni za vipindi vya radio, televisheni na hata makala za magazeti kila unapofika msimu wa mvua ili watu wajikinge na balaa la kipindupindu.

Nimeshuhudia tangu nikiwa bado mdogo kampeni za kudhibiti ugonjwa huu kwa mafunzo maarufu ya kuchemsha maji ya kunywa kabla hujayanywa, kunawa mikono kila unapotoka chooni, kuosha matunda kabla ya kula na mafunzo mengine kadha wa kadhaa ili kuepuka ugonjwa huo.

Lakini hata hivyo, pamoja na kampeni hizo, bado mlipuko wa ugonjwa huo unaendelea kujitokeza mwaka hadi mwaka ingawa athari zake si mbaya kama zile za miaka ya 1978 hadi miaka 1980 ambapo watu wengi waliougua kipindupindu waliweza kuwaambukiza ndugu zao na kusababisha madhara kuwa makubwa zaidi.

Unapowasikiliza watu na kutafuta maoni yao juu ya swali hilo, utagundua wana ufahamu mkubwa tu wa sababu za maambukizi na pia namna ya kuukwepa ugonjwa huo.

Watakuambia ni kwa sababu ya kukosa maji salama ya bomba vijijini na baadhi ya miji, kutokuwa na miundombinu ya maji kupitisha majitaka katika maeneo mengi, kukosa vyoo salama na sababu nyingine nyingi ambazo kimsingi zinaonyesha kuwa tunafahamu sababu za ugonjwa huo.

Katika hali kama hii ndipo Mjadala unapojiuliza, iwapo tunafahamu kuwa maji yasiyo salama ni hatari kwa kuyanywa au hata kuyakanyaga, kujisaidia ovyo vichakani au kwenye mito kunaleta kipindupindu, kwa nini basi tusikabiliane na mambo hayo? Tunasubiri nini?

Kwa vyovyote iwavyo ni kwamba jukumu la kujizuia na maambukizi ya kipindupindu bado lipo mikononi mwa kila mmoja wetu na bahati nzuri serikali kwa upande wake imeshatimiza kwa kiwango kikubwa jukumu lake la kutoa elimu ya kujilinda na ugonjwa huo.

Iwapo tutazingatia mafunzo yaleyale ya msingi ya kujiepusha na kupindupindu kama vile kuchemsha maji kabla ya kuyatumia, kujisaidia ovyo vichakani au kwenye mito, kuosha matunda kabla ya kula na kuwahi hospitalini kila mtu anapopatwa na ugonjwa wa kuhara na kutapika, basi tutaudhibiti ugonjwa huu.

Mjadala unasema ni ukweli uliodhahiri kuwa serikali imeshatimiza wajibu wake wa kutoa elimu juu ya ugonjwa huu na inaendelea kufanya hivyo.

Jukumu kubwa linabaki kwetu sisi wananchi kuamua kupambana na sababu na vyanzo vyote vya maambukizi ya ugonjwa huu ili kulinda afya zetu na kuokoa maisha yetu.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Mkulima Shadidu Ali, Mkazi wa Kijiji cha Kwamadebe, Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma, akimwonyesha mkungu wa ndizi Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (kulia), alipotembelea banda la Halmashauri ya Wilaya hiyo, katika kilele cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane,Kanda ya Kati, kwenye viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mikopo elimu ya juu inavyogeuka shubiri

**INATOKA UK. 2**

ya asilimia moja ambayo bodi inatukata kwa ada ya uendeshaji ilhali watumishi wake wameajiriwa ili wafanye kazi hiyo.

"Nafikiri kuna haja kuiangalia upya sheria hii, inatuumiza wananchi. Kwenye mshahara ukikatwa bima ya afya, kodi ya serikali, NSSF na Bodi ya Mikopo unabakiwa na fedha kidogo sana, inavunja moyo.

"Penalti imetukumba watu ambao tulipohitimu chuo, hatukupata kazi, tungerejesha mikopo kupitia vyanzo vipi? Huu ni mkopo wa serikali kwa wananchi wake, siyo wa kibiashara, ulenge zaidi kusaidia na siyo kukomoa," Ntwale alishauri.

Akiwa mjini Mtwara jana, mnufaika mwingine wa mikopo hiyo, Nzumi Malendeja, aliambia Nipashe kuwa kuna haja serikali kufanya marekebisho mengine kwenye Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili wanufaika walipe kiasi kilekile walichokopeshwa badala ya deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka.

Malendeja alisema alinufaika na mkopo wa HESLB kwa kupatiwa Sh. milioni nane alipokuwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) kuanzia mwaka 2009 hadi 2012 na alianza kurejesha mkopo huo Machi mwaka huu baada ya kuajiriwa na Aga Khan Foundation, deni likiwa limefika Sh. milioni 22.

"Ninaona ni deni ambalo haliishi kwa sababu linaongezeka kila mwaka, nafikiri wanufaika tulipe lakini kusiwe na ongezeko la asilimia sita kila mwaka.

"Pia, makato ya asilimia 15 ni makubwa mno, yanapunguza hata uwezo wa mnufaika kukopeshwa na taasisi nyingine za kifedha kwa sababu tayari anakuwa na mzigo wa kulipa deni hilo la HESLB, NSSF na kodi ya serikali.

"Ninaamini makato haya makubwa ndiyo yanayotengeneza mazingira ya wanufaika kutafuta mbinu za kukwepa kurejesha fedha walizopewa," Malendeja alisema.

Kifungu 7.2.1.1 cha Mwongozo wa HESLB wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa Wanafunzi kinabainisha kuwa, ili kuhakikisha mfuko wa ukopeshaji unakuwa endelevu, mnufaika wa mkopo wa bodi hiyo atalipa tozo ya kulinda thamani ya fedha ambayo itakatwa asilimia sita kwa mwaka tangu tarehe mnufaika aliyoanza kupokea mkopo.

Vilevile, katika kifungu 7.2.1.2 cha mwongozo wake huo, HESLB inaeleza kuwa itakata asilimia moja ya ada ya uendeshaji kwa mwanafunzi mnufaika.

Pia, katika kifungu 7.2.1.3 cha mwongozo huo, inaelezwa kuwa ikiwa mnufaika atashindwa kulipa mkopo baada ya kipindi cha neema cha miezi 24 baada ya kuhitimu masomo yake, ataongezewa makato ya adhabu ya asilimia 10.

**KAULI YA HESLB**

Akizungumza na Nipashe kwenye ofisi ya HESLB zilizoko Mwenge jijini Dar es Salaam juzi, Meneja wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa bodi hiyo, Omega Ngole, alisema changamoto ya deni kuongezeka na wanufaika kushindwa kumaliza kulilipa inatokana na wengi wao kuchelewa kuanza kulipa, hivyo kukumbana na adhabu.

Alisema ili mnufaika aweze kumaliza deni lake kwa wakati na kutoonekana linaongezeka kila mwaka, anatakiwa kuanza kulipa kwa wakati uliopangwa na bodi.

Akifafanua zaidi kuhusu suala hilo, Ngole alisema kwa mnufaika aliyepewa mkopo wa Sh. milioni 6.12, kama atalipa kwa wakati (bila penalti), akiwa na mshahara wa kati ya Sh. 700,000 na 750,000, atakatwa Sh. 109,000 kila mwezi na atamaliza kulipa deni lake la Sh. milioni 7.201 (ongezeko la Sh. milioni 1.081) katika kipindi cha miaka mitano na miezi saba.

Kwa mnufaika aliyepata mkopo wa Sh. milioni 13, Ngole alisema deni lake litakuwa Sh. milioni 17.082 na kama atalipa bila penalti, mshahara wake ukiwa kati ya Sh. milioni moja na milioni 1.4, kila mwezi atakatwa Sh. 150,000 na atamaliza kulipa deni katika kipindi cha miaka tisa na miezi mitano.

Ngole pia alisema mnufaika aliyepewa Sh. milioni 20, atatakiwa kulipa Sh. milioni 26.516 kama hatapigwa penalti na atakamilisha kulipa deni lake katika kipindi cha miaka tisa na miezi minane ikiwa mshahara wake ni kati ya Sh. milioni 1.5 na milioni 1.9 kwa kukatwa Sh. 225,000 kila mwezi.

Meneja huyo pia alieleza kuwa mnufaika aliyekopeshwa Sh. milioni 50 atatakiwa kurejesha Sh. milioni 65.978 na kama atalipa kwa wakati kwa kukatwa kila mwezi asilimia 15 ya mshahara wa kuanzia Sh. milioni 3.8 (Sh. 570,000), deni lake litakamilika katika kipindi cha miaka tisa na miezi saba.

Ngole alibainisha mpaka sasa, ni wanufaika 11,214 waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 2.3 ya wanufaika wote 479,779 waliopewa mikopo yenye jumla ya Sh. trilioni 3.889 tangu serikali ilipoanza kuitoa mwaka 1994.

Alisema HESLB ipewe jukumu la kusimamia urejeshwaji wa mikopo hiyo mwaka 2007, wahitimu 11,214 waliofanikwa kumaliza madeni yao, wamelipa jumla ya Sh. bilioni 67.6 na kupewa vyeti.

Meneja huyo alisema jumla ya wahitimu 145,656 hawajaanza kulipa mikopo yao ya jumla ya Sh. bilioni 432.5 na wana zaidi ya miaka 10 tangu wahitimu masomo yao. Kiasi hicho cha fedha ni zaidi ya mikopo iliyotolewa na HESLB kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, katika mwaka huo wa fedha (2018/19), bodi hiyo ilitoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 427 kwa wanafunzi 123,285. Kati yao, wa mwaka wa kwanza walikuwa 40,544 na wanaoendelea na masomo walikuwa 82,741.

Ngole alisema wahitimu 162,983 wanaendelea kurejesha mikopo yao kila mwaka na kwa mwaka jana walifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 183 na mwaka huu wanatarajia kukusanya Sh. bilioni 221.

Alisema wanufaika wengine 123,329 ni wanafunzi ambao wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali nchini na hawajaanza kurejesha mikopo, hivyo kuwekwa kundi moja na wadaiwa wengine ambao wako katika kipindi cha neema cha miaka miwili baada ya kuhitimu.

"Jumla ya wahitimu 145,656 ambao tunawaita sugu, hawajawahi kurejesha mikopo yao hata kidogo, fedha ambazo zinafika Sh. bilioni 432.5. Tuna mikakati mbalimbali ya kuhakikisha tunawapata ili waanze kurejesha," Ngole alisema.

Meneja huyo aliitaja mikakati ya bodi hiyo kuhakikisha inawanasa wanufaika hao wa mikopo yake kuwa ni pamoja na kukutana na wadau wa kimkakati kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Chama cha Waajiri (ATE) na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kubadilishana taarifa za kuwabaini.

Ngole pia alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wanufaika na waajiri kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo yao kwa wakati.

Alisema bodi hiyo pia inafanya ziara za ukaguzi kwa waajiri kwa kupitia orodha ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi wao.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam juzi, Mwanasheria Frank Mushi aliwataka waombaji wa mikopo hiyo kutokimbilia kutia saini mkataba ya kupewa mkopo hadi pale wanapojiridhisha kuhusu masharti ya mkopo huo.

"Kibaya zaidi sheria za mikataba zinasema inapotokea mkataba umeandikwa na mkautia saini, wote mnakuwa mmefungwa na 'terms' (masharti) za ule mkataba.

"Kwa hiyo, lazima mwanafunzi anapotia saini aangalie kwa umakini masharti yaliyomo. Chochote kinachofanyika kama ni ongezeko la sita au nini, lazima atambue mapema.

"Lakini nafikiri sheria iangaliwe kama Bodi ya Mikopo ni taasisi inayofanya biashara au ipo na nia ya kuwasaidia wananchi hasa kipindi hiki ambacho kuna changamoto kubwa ya ajira," alisema.

## Wakulima sasa kulipwa kwa wakati kupitia mfumo TMX

**INATOKA UK. 5**

"Napenda kusisitiza kuwa kuanza kufanya kazi kwa mfumo huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ibara namba 22(g)(ii) ya 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17– 2020/21) na Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza sekta ya Kilimo (ASDP II)".

Vile vile, Waziri Mkuu alizindua mfumo mwingine wa Kielektroniki wa Kusimamia Biashara za Kilimo (Agricultural Trade Management Information System – ATMIS)."Mifumo hii inalenga kuongeza ufanisi wa shughuli mbalimbali za kuendeleza sekta za kilimo nchini na kuimarisha biashara ya mazao na bidhaa za kilimo.

Akizindua mifumo hiyo, Waziri Mkuu alisema serikali inasimamia utekelezaji wa BluePrint inayolenga kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. "Kupitia BluePrint hiyo, changamoto mbalimbali zimeainishwa na kuwekewa utaratibu wa kutatuliwa."

Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni kuwapo kwa mlolongo mrefu wa kupata vibali na leseni za uwekezaji na biashara na wateja kulazimika kufuata vibali hivyo kwenye Ofisi za Taasisi zilizopewa mamlaka ya kutoa leseni na vibali hivyo.

## Wagonjwa wa figo SADC kupokelewa

**INATOKA UK. 5**

ya kupokea wagonjwa kutoka nchi wanachama wa SADC.

Alisema hatua hiyo inajenga mazingira kwa wanajumuiya ya SADC kutokuwa na haja ya kupeleka wagonjwa wao kutibiwa nje ya nchi za jumuiya hiyo, badala yake watapokelewa na kutibiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

Awali, alibainisha Wizara ya Afya inaamini mkutano wa SADC utaongeza idadi ya wagonjwa wanaopokelewa kutoka Jumuiya hiyo ambayo ilikuwa ni wagonjwa 24 kila mwezi, kutoka nchi za SADC na hasa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Comoro na Malawi.

Waziri Ummy alisema kupitia Mkutano wa SADC unaofanyika nchini kuna mambo mengi ambayo Tanzania itanufaika, miongoni mwa hayo ni huduma za kisasa za afya zinazotolewa nchini kwa sasa.

Aliyasema hayo baada ya kutembelea maonyesho ya viwanda ya SADC na alipita kujionea mabanda ya sekta ya afya ikiwamo la Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na kusema kuna huduma za tiba ya kisasa zinazotolewa katika taasisi hizo.

"Katika maeneo haya ya maonyesho tumejipanga vizuri kutoa huduma ya tiba ya dharura, kuna ambulance 22, pamoja na vyumba maalum vilivyotengeneza kwa huduma hizo kwa mtu atakayepata matatizo ya kiafya katika mkutano huu," alisema.

# Halmashauri yabanwa kujibu hoja 70 za CAG

**Na Tiganya Vincent,** URAMBO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Urambo imetakiwa kujibu hoja 70 za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2017/18 ikiwamo ya kulipa deni la Sh. milioni 467 kwa ajili ya mikopo ya vikundi mbalimbali ili zimalizike na kufutwa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkaguzi Mkuu kutoka Ofisi ya CAG Mkoa wa Tabora, Aniecet Mushumbusi, wakati wa kikao maalumu cha Baraza la Madiwani ya kupitia hoja ya mbalimbali za mwaka 2017/18.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilikuwa na hoja 101 ambapo kati ya hizo 25 zilifutwa, 59 ziko katika hatua mbalimbali ya utekelezaji, 11 hazikutekelezwa kabisa, sita zinajirudiarudia na 70 zimesalia.

Mushumbusi alisema kuchelewa kujibu hoja hizo kutasababisha ziendelee kujirudiarudia katika mwaka mwingine wa fedha.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, aliwataka wateja wa halmashauri zote kuongeza kasi katika kujibu hoja zinazotolewa na CAG ili kujifuta na kutozalisha hoja mpya.

Alisema kumekuwapo na kasi ndogo kwa watendaji kujibu hoja za CAG, jambo ambalo limesababisha kuendelea kuwa na hoja za zamani ambazo zingekuwa zimefuta, lakini kwa sababu hiyo zimeendelea kuonekana katika vitabu vya CAG.

Makungu alisema serikali haitasita kumchukulia hatua mtendaji yeyote ambaye atachelewesha kujibiwa kwa hoja na yule atakayesababisha uzalishaji wa hoja.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, aliwaagiza watendaji wa Halmashauri ya Urambo kufanyia kazi dosari zote zilizoibuliwa na CAG ikiwamo kutolipa deni la Sh. milioni 467, na kushindwa kukusanya deni la Sh. milioni 31 kutoka kwa vikundi vilivyokopeshwa na halmashauri hiyo.

Alisema ni vema fedha hizo zikapelekwa kwenye vikundi mbalimbali ili ziwe chachu ya maendeleo na wajitahidi kukusanya deni hilo ili nazo ziweze kusaidia vikundi vingine vya vijana, wanawake na walemavu.

Naye Mbunge wa Urambo, Margaret Sitta, alipendekeza kuundwa kwa timu ya wataalamu wachache ambao watasaidia katika kufuatilia kila siku majibu ya hoja za CAG ili ziweze kufutwa na kuisaidia halmashauri hiyo kuitwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa ajili ya kujibu hoja.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutusubiri timu ya CAG au LAAC ndio waanze kutafuta majibu na vielelezo vya hoja mbalimbali.



Wafanyakazi wa mkandarasi wa ujenzi wa daraja jipya la Selander, wakikata kiu kwa maji ya madafu, kando ya Barabara ya Barack Obama, eneo la Aga Khan, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Iringa yapata jukwaa la mchele

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WADAU wa mnyororo wa ongezeko la thamani zao la mchele, wameunda jukwaa la Wilaya ya Iringa kwa lengo ya kutambulisha mchele wa mkoa wa Iringa.

Akizungumza wakati wa kikao cha mrejesho cha wadau wa mchele Mratibu wa Wilaya (FAO-Rice), Lefdedy Msamba, alisema jukwaa hilo litakuwa ni chambo cha wadau walio katika mnyororo wa ongezeko la thamani katika sekta ya mchele.

Aliongeza kuwa walengwa wa jukwaa hilo ni wauzaji wa pembejeo, wakulima, watoa huduma mbalimbali, wasindikaji, wafanyabiashara, wasafirishaji, taasisi za fedha, taasisi za utatifi na taasisi nyinginezo katika sekta zisizo za serikali.

Msamba alisema dhumuni la kuundwa kwa jukwaa ni kupata ufumbuzi wa changamoto zilizo katika sekta ya mchele na kubuni njia za kushughulikia changamoto za kijamii, mazingira, kiuchumi na fursa kwenye sekta ya mchele.

Jukwaa la wilaya la wadau wa mnyororo wa ongezeko la thamani la zao mchele limetokana na shughuli ambazo wadau wa mchele wamekuwa wanafanya kwa kushirikiana na Baraza la Mchele Tanzania tangu 2016.

Mkoa wa Iringa unazalisha mchele na kufanya mchele unaozalishwa mkoani hapa haujulikani kwa hiyo, Jukwaa la Wilaya Iringa litakuwa chombo maalumu cha kutambulisha mchele katika masoko.

# Tasaf yawezesha ujenzi barabara, kilimo cha miti

**Na Restuta Damian,** NGARA

WANANCHI wa Kijiji cha Murgina Kata ya Mabawe na Kijiji cha Munyenzi wilayani Ngara mkoani Kagera wametumia nguvu kazi kutengeneza barabara yenye urefu wa kilomita 8.5 na kuwekeza kilimo cha miti ekari 14 ili kurahisisha uhamishaji wa mazao pamoja na uhifadhi mazingira.

Miradi hiyo imeweza kuwapatia ujira wanufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini Tasaf kama sehemu ya kuwapatia kipato chenye kuboresha maisha yao kwani miradi hiyo iko chini ya serikali ya kijiji kwa manufaa ya wananchi wakiwamo walengwa wa mpango huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mara baada ya mkutano wa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, wenye kusikiliza shughuli za utekelezaji wa mpango wa Tasaf 3 sehemu ya kwanza uliodumu kwa muda wa miaka mitatu na kuelekea sehemu ya pili ya mpango huo unaonza mwezi Agosti mwaka huu.

Anania Mpebuye, mkazi wa kijiji cha Murgina Kata ya Mabawe, alisema serikali ilileta wazo la kuanzisha kutengeneza barabara ya vumbi baada ya kuona wakulima wanahangaika kutoa mazao shambani.

Alisema wakati mwingine wamekuwa wakikosa huduma ya afya ikilinganishwa na ubovu wa miundombinu ya barabara kutokupitisha magari yanayoleta huduma ya afya.

"Tulikuwa hatupati huduma ya afya kwani barabara ilikuwa haipiti kwa magari yanayokuja kijiji kwetu na kulazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma wanawake wanapotaka kujifungua." alisema Mpebuye.

Aidha, alisema mradi huo ulipoanzishwa vijana wenye uwezo wa kufanya kazi walipatiwa ajira ya kulipwa kwa eneo shilingi elfu 5,000 ikiwa nyenzo zilizotumika ni majembe na koleo.

Verediana Julius, mkazi wa kijiji cha Muyenzi, alisema mradi wa shamba la miti ni manufaa ya kila mwananchi hasa wanufaika wa mpango huo kwa kujifunza namna uhifadhi mazingira na kwa manufaa ya baadaye.

Julius alisema kupitia vikundi vilivyoundwa na kwa makubaliano ya kuweka umoja wa uzalishaji fedha inayopatikana kutoka kwenye madirisha ya uhawilishaji malengo, ni kuwa na shamba la miti kwa ajili ya biashara ya thamani shuleni na taasisi zinazohitaji miti au mbao.

Mtendaji wa Kijiji cha Murgina, Valerian Tibaijuka, alisema kuibuka miradi ya aina hiyo ni kulingana na jiografia ilivyokaa ambapo kwa kijiji hicho shughuli kubwa ni kilimo na idadi ya wanufaika wa mpango ni 121.

Tibaijuka alisema ujira kwa wakazi hao ni asilimia 75 ikiwa gharama iliyotumika matengenezo ya miundombinu hiyo Sh. milioni 19.3 na jumla ya Sh. milioni 125.5 zilipokelewa kwa ajili ya malipo ya walengwa.

Mtendaji wa Kijiji cha Muyenzi, Nicolus Mundewe, alisema kijiji hicho kinajumla ya wakazi 2,923, wanawake ni 1,613, wanaume 1,310. Kati ya hao walengwa ni 113 ambao waliweza kufanya ujira kwenye shamba la miti ya kijiji na kulipwa.

Naye Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Dk. Mery Mwanjelwa, alisema ubunifu wa miradi hiyo ya kudumu unufaishe walengwa wote na kuhakikisha wanaweza kusimama wenyewe kwa maisha yao.

Alisema wataalamu ambao wameingia na kusaidia elimu ya utarayarishaji mashamba ya miti na kuboresha barabara watumike pia kuwapatia sehemu sahihi ya soko.

## Vijana watakiwa kujiunga vikundi

**Na Yasmine Protace**

VIJANA wametakiwa kujiunga katika makundi ikiwamo kuyasajili ili waweze kunufaika na mikopo ambayo imekuwa ikitolewa na serikali.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, Omary Kumbiramoto, wakati akifungua mafunzo ya mwezi mmoja kwa watoto waliotoka katika mazingira magumu Kata ya Ukonga.

"Nawapongeza viongozi wa kituo cha maarifa Kipunguni kwa kuwakumbuka watoto walio na mazingira magumu na kuamua kuwapatia elimu bure ili waweze kujiongezea kipato," alisema.

Aliongeza kuwa serikali inayasaidia makundi maalumu kwa kuwatatulia changamoto zao ikiwamo kuwawezesha kwa mikopo wanawake na vijana, hivyo ni jukumu la vijana kujiunga katika makundi ili mnufaike na mikopo hiyo.

Aliongeza kuwa elimu ambayo imetolewa na kituo hicho itawasaidia vijana hao kujiongezea kipato.

Mkurugenzi wa Kituo cha Maarifa ya Jamii, Selemani Bishagazi, alisema vijana 100 watanufaika na mafunzo hayo kutoka kwa walimu wataalamu waliobobea katika masuala ya ujasiriamali.

"Mafunzo haya ni mwezi mmoja yanatolewa na hakuna gharama zozote ambazo watalipa na watajifunza kutengeneza mifuko, mishumaa, batiki, kuweka dawa kichwani, kutengeneza keki, kupamba ukumbi na kilimo cha mboga," alisema.



Mchuuzi wa miwa akiandaa bidhaa yake kwa ajili ya kuwauzia wateja, eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam juzi, huku akiwa umefunga ufagio kwenye tolori ambao huutumia kufagia kwenye eneo analofanyia biashara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia ataka Watanzania kuvilinda viwanda

**Na Idda Mushi na Christina Haule,** MOROGORO

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewataka viongozi na Watanzania kuvilinda viwanda vilivyopo na vinavyoanzishwa kwa kutambua kuwa ni mali yao, na sio mali ya wawekezaji peke yao.

Alisema ni vyao kwa sababu bidhaa zinazozalishwa zinategemea malighafi ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na zinazozalishwa na wananchi na kuchangia ukuaji wa mapato ya mtu mmoja mmoja, mkoa na taifa.

Makamu wa Rais alisema hayo wakati akizindua viwanda vya kuchakata mazao ya jamii ya mikunde cha Mahashree Agro Processing kilichopo Mikese wilayani Morogoro na cha kuchakata mpunga cha Muruz Wilmer East Africa Miller l.t.d kilichopo Kihonda Manispaa ya Morogoro.

Samia aliwahimiza wananchi wa Morogoro kuilinda miradi mikubwa inayopita maeneo yao ikiwamo mkubwa wa reli ya kisasa, na umeme wa Rufiji unaotegemea maji yatokanayo na mabonde na mito ya Morogoro, hasa kwa kulinda mazingira ili umeme upatikane wa kutosha kusaidia viwanda vilivyopo na vinavyoanzishwa.

Alipongeza hatua ya wawekezaji wa sasa wa viwanda kutafuta kwanza masoko kabla ya kuanza uzalishaji, na kuwahimiza wananchi kuchangamkia fursa ya kuzalisha kwa wingi mazao kwa vile tayari wana maeneo ya kuuzia bidhaa zao sambamba na kuuza kwenye masoko ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Licha ya Morogoro kuwa miongoni mwa maghala ya taifa ya chakula, Makamu wa Rais akashangazwa kuona bado mkoa huo ni miongoni mwa inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wenye udumavu, hivyo akahimiza masoko ya kunde kutumike pia kwa mahitaji ya soko la ndani.

"Mwaka juzi Tanzania ilikuwa na shida kubwa ya soko la mbaazi, kama kiwanda kama hiki (cha kuchakata mazao ya kunde) kingekuwapo kingesaidia kuondoa tatizo hili, kuwapo kiwanda hiki hawatanunua tu mbaazi, bali na mazao mengine jamii ya mikunde," alisema na kuongeza:

"Mwekezaji amekusudia kuwasaidia Watanzania, kiwanda kina thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 30, asingeweza kuwekeza hivi kama hajui anafanya nini:

Samia alisema hayo akiwa katika Kiwanda cha Mahashree, na kupongeza asilimia 40 ya ajira kutolewa kwa wanawake.

Aidha, alisema Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa ya kupotea kwa mazao ya kilimo, hivyo uwapo wa viwanda hivyo kutasaidia sana kukabiliana na tatizo hilo.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema kuanzishwa kwa viwanda vingi kunaongeza uhakika wa masoko ya mazao ya wakulima, na kwamba uwapo wa reli ya kisasa, umeme mkubwa na wa uhakika unadhihirisha uhakika wa serikali ya awamu ya tano ya Tanzania ya viwanda.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Suleiman Sadiq Murad, aliwahimiza wenye viwanda kuzingatia utunzaji wa mazingira, hasa ikizingatiwa kuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha kuchakata mpunga na kuzalisha mchele, Basheigha Haroun, alisema kiwanda hicho kitagharimu dola milioni 20 na kina uwezo wa kuzalisha na kuchakata tani 600 za mpunga kwa siku kwa awamu mbili, kwa kuanza na tani 300.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha Mahashree, Malick Mahashree, alisena wameshapata masoko ya bidhaa watakazozalisha katika nchi mbalimbali duniani ikiwamo China, India na Ujerumani na wataendesha shughuli zao kwa mfumo wa mikataba, kurahisisha mikopo na kusimamia masuala ya mbolea, na watazingatia pia ulimaji wa kilimo hai.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Stephen, alisema Mkoa wa Morogoro umeanzisha viwanda vipya zaidi ya 3,000 vikiwamo viwanda vidogo 302 na vikubwa 20, vya kati na vidogo kabisa.

Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, aliahidi wizara yake itaendelea kutengeneza mazingira rafiki na wezeshi kuhakikisha shughuli za uzalishaji na uendeshaji wa viwanda zinafanikiwa ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, shule, hospitali na vituo vya afya.

# Siri ya mtama kuzuia uzee, magonjwa sugu yafichuliwa

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

KITUO cha Utafiti wa Kilimo (TARI) Ilonga, kimetafiti mbegu ya mtama mwekundu na rangi ya kawia ambao umeonyesha kuwa na sifa ya kuzuia uzee, magonjwa ya kansa na moyo.

Pia umebainisha kumsaidia mtu kutozeeka haraka endapo atautumia mtama huo kama chakula.

Akizungumza katika maonyesho ya Nanenane katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu, mtafiti wa mazao baada ya mavuno, Salvatory Kundi, alisema mtama mwekundu na kawia umebainika kuwa unapokula unazalisha chembechembe zinazofahamika kama autoxidants zenye uwezo wa kusafiri haraka katika mwili.

Alisema chembechembe hizo za autoxidants zinaposafiri haraka katika mwili zinasaidia kuharibu chembechembe nyingine zinazosababisha mwili kuuchosha na kumwonyesha mtu kuanza kuzeeka.

"Mtu akila mara kwa mara huu mtama kwa ajili ya matumizi ya chakula utamsaidia kupunguza uzee licha ya kuonekana kwa umri mkubwa, hivyo tunawashauri Watanzania waanze kula huu mtama ili kuepuka na uzee wa mapema," alisema Kundi.

Akizungumzia kuhusu magonjwa ya kansa na moyo, alisema kuwa mtama huo unasaidia unamengenya chakula taratibu na kutoa sukari kidogo kidogo, hivyo kumpunguzia mtu kutopata magonjwa hayo endapo atautumia mara kwa mara.

Mtafiti huyo alisema kuwa mbegu hiyo ya mtama sasa ipo katika mchakato wa kutolewa rasmi mwakani na kuanza kuuzwa kwa wakulima, na kwamba zinafanyiwa majaribio na Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (Tosci).

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe, ambaye alitembelea banda la TARI, alisema umefika wakati sasa kwa watafiti hao kuhakikisha utafiti mbalimbali wanaofanya unawafikia wakulima ili kuongeza tija kwa kulima kilimo biashara cha zao la mtama, ambacho kinaonekana kupitia utafiti wa mbegu hiyo kitawaongezea kipato.

Mhandisi Mtigumwe alisema watafiti wa kilimo wamekuwa wakifanya kazi nzuri na kupata mbegu bora zinazohimili magonjwa na zinazohimili mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo, alisema matokeo ya utafiti hayawafikii wananchi na kuitaka TARI sasa kuhakikisha utafiti unawafikia wakulima.

Mwenyekiti wa Bodi ya TARI, Dk. Yohana Budeba, aliagiza taasisi hiyo kuweka mpango mkakati wa kuhakikisha uzalishaji wa mbegu za mtama na mazao mengine ya nafaka unaongezeka kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima nchini.



Mbunge wa Jimbo la Solwa, Shinyanga Vijijini, Ahmed Salum, akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijiji cha Lyabukande jana, wakati akinadi utekelezaji wa ahadi zake alizoahidi kwenye uchaguzi mkuu uliopita mwaka 2015. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mifuko feki yamsimamisha kazi mkuu wa kituo TBS

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATUMISHI wawili wa Shirika la Viwango (TBS), akiwamo mkuu wa kituo cha mpaka wa Namanga mkoani Arusha, Emmanuel Kiwango na mwenzake Jenipher Jackson, wamesimamishwa kazi kwa tuhuma za kuingiza nchini mifuko mbadala ya plastiki isiyo na viwango.

Mifuko hiyo ina thamani ya Sh. milioni moja, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Mkurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS),Dk. Ngenya Yusuf. Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha, Dk. Yusuf, alisema kusimamishwa kazi watumishi hao wawili kumetokana na ukosefu wa maadili ya utumishi kazini.

Alisema mifuko hiyo mbadala isiyo na viwango ilipitishwa mpakani hapo wiki hii Agosti 5, na watumishi hao wa TBS na kupata kibali cha kuingia nchini kinyume cha sheria.

Alisema baada ya kupita mpakani hapo Jeshi la Polisi liliikamata mifuko hiyo mbadala ambayo haijakidhi viwango.

"Tumekuwa tukipata malalamiko mengi katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha kuwa kuna utitiri wa mifuko hiyo isiyo na viwango, tulidhani wafanyabiashara wanapitisha kwa njia za panya, kumbe hata mpakani ambapo kuna wataalamu nako wanashindwa kuzuia magendo wanaruhusu bidhaa zisizo na ubora kuingia nchini," alisema Dk. Yusuf.

Alieleza kuwa kwa vile watumishi hawa wa TBS wameruhusu mifuko hiyo kuingia nchini kinyume cha sheria, yawezekana pia wanapitisha bidhaa nyingine zisizo na ubora hivyo amewasimamisha kazi na ikithibitika ilikuwa ni tabia yao watachukuliwa hatua za kisheria.

"Natoa onyo kwa wafanyakazi wa TBS popote walipo pamoja na wale wanaofanya utafiti wa sampuli za bidhaa mbalimbali waache mara moja tabia zisizofaa ikiwamo kuondoa malalamiko kwa wafanyabiashara wanaohitaji huduma za TBS kwa ajili ya kuendelea na biashara zao," alisema mkurugenzi huyo. Alisema kuna malalamiko kwa wafanyabiashara kuchukua muda mrefu kupewa majibu ya bidhaa zao hivyo hatasita kuwachukulia hatua wafanyakazi wote watakaosababisha ucheleweshaji huo au uzembe usio wa lazima kwa wafanyabiashara.

# Wafugaji washauriwa kusikiliza wataalamu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewashauri wafugaji kutumia mbinu zinazotolewa na wataalamu kuzalisha nyasi kwa ajili ya malisho ya mifugo yao, ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa nyasi uliopo katika maeneo mbalimbali ya wafugaji.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Felix Nandonde, alisema hayo wakati akizungumza katika mdahalo uliowashirikisha wadau mbalimbali wa mifugo kuangalia changamoto, fursa na mafanikio yaliyopo katika sekta ya maziwa.

Mjadala huo uliandaliwa na wadau pamoja na shirika linalojihusisha na kilimo na ufugaji la Agri Pro Focus.

Aliwaambia washiriki kuwa kutokana na changamoyo hiyo wamewataka kutumia mbinu hizo, ili waachane na kutegemea malisho ya kubahatisha badala yake kujiandalia malisho ya uhakika kwa ajili ya kuongeza idadi ya mifugo na malisho nchini.

Alisema endapo wafugaji watakuwa tayari kutumia mbinu hizo za kulima mazao ya majani ya kulisha wanyama wao itasaidia sana kuongeza wingi wa maziwa nchini na kuwezesha kuanzishwa kwa viwanda vingi zaidi kwa ajili ya usindikaji wa maziwa pamoja na kuongeza mnyororo wa thamani.

"Kupitia mdahalo huu tumeweza kujua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hiyo ya mifugo, huku kubwa ikiwa ni ukosefu wa malisho, hivyo changamoto zote tutazifanyia kazi ili kuhakikisha maziwa yanapatikana ya kutosha na kuona ongezeko la unywaji wa maziwa kwa ujumla kwani bado unywaji wa maziwa upo chini sana," alisema Nandonde.

Mratibu Mwandamizi wa Shirika la Agri Pro Focus, Ernest Likoko, alisema wamekuwa wakifanya kazi na sekta ya kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuangalia changamoto zilizopo, ili ziweze kupatiwa ufumbuzi hasa zilizoibuliwa katika mdahalo huo ambazo zitapelekwa kwenye mkutano mkuu wa wadau wa maziwa Afrika utakaofanyika wiki ijayo, Agosti 13 nchini Kenya.

Alisema wanatarajia kuanzisha jukwaa la wadau katika sekta ya maziwa ambalo litaweza kuendeleza sekta hiyo sambamba na kuja na suluhisho la changamoto hizo, ambapo jukwaa hilo litawajumuisha wafugaji, wakulima, wadau kutoka serikalini, pamoja na mashirika binafsi.

Likoko alisema kuwa, wanaendelea kuhamasisha wadau ili kuleta maendeleo ya sekta hiyo sambamba na kuendeleza usindikaji wa maziwa kwenye viwanda mbalimbali lengo likiwa ni kuongeza idadi kubwa ya wanywaji wa maziwa.

Kwa upande wa Meneja Msaidizi wa Mradi wa Kuongeza Kipato na Ajira kwa Vijana na Wanawake, wa Shirika la Maendeleo la Uholanzi ( SNV),Paschal Tekwi, alisema kuna changamoto nyingi katika sekta ya mifugo, hivyo wamekuwa wakihakikisha wanatoa mikopo kwa wanawake ili waweze kununua vitendea kazi kwa ajili ya kuendeleza sekta ya maziwa nchini.

Alisema vijana wengi wanahitaji kufuga lakini bado hawajajengewa mazingira bora ikiwemo kupatiwa mikopo ya mitamba ya ng'ombe bora wa maziwa, ili waweze kujiajiri, hivyo kuna haja ya wadau mbalimbali kuweka nguvu kwa pamoja katika uratibu kwenye mnyororo wa thamani kwenye sekta ya maziwa na kwa kufanya hivyo tutaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## Likizo bila malipo kikwazo unyonyeshaji watoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

LIKIZO ya uzazi bila malipo imetajwa kuwa sababu inayochangia baadhi ya wanawake kuwanyonyosha maziwa mbadala watoto wao na kuwaachisha kunyonya mapema.

Aidha, imebainika wanawake wanaopata likizo ya uzazi isiyo na malipo au yenye mshahara kidogo hurudi kazini mapema kabla ya wakati au siku chache baada ya kujifungua.

Hayo yamesemwa kwenye kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani yaliyofanyika Kata ya Riroda wilayani Babati mkoani Manyara chini ya uratibu wa Shirika la World Vision Tanzania (WVT).

Akifunga maadhimisho hayo Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alisema Tanzania imefanya juhudi kubwa katika ulishaji wa watoto wachanga na wadogo, lakini hali bado hairidhishi.

Alisema watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama bila kupewa maji na vyakula vingine kwa miezi sita mfululizo baada ya kuzaliwa mkoani Manyara ni asilimia 40.6 huku kitaifa ikiwa ni asilimia 57.8.

"Takwimu za kimataifa zinaonyesha karibu zaidi ya nusu asilimia 61.2 ya watu wote duniani wanategemea kipato chao kiuchumi kutoka kwenye sekta zisizo rasmi," alisema Elizabeth na kuongeza:

"Kwa Afrika, karibu asilimia 90 ya ajira zote hususani wanawake hutoka sekta isiyo rasmi na wafanyakazi wake wanakabiliwa na vikwazo vinavyozuia unyonyeshaji maziwa ya mama ipasavyo," alisema Mkuu wa Wilaya.

Kitundua alivitaja vikwazo hivyo kuwa ni pamoja na kuishi mbali na sehemu wanazozifanyia kazi, kufanya kazi kwa muda mrefu bila kupata mapumziko na kufanya kazi katika mazingira hatarishi.

"Zaidi ya hayo wafanyakazi hao hususani wanawake hukosa uelewa wa namna bora ya kufanikisha unyonyeshaji wa maziwa mama na faida za kufanikisha kazi anayoifanya kwa wafanyakazi na familia zao.

Kwa upande wake Ofisa Lishe Shirika la World Vision Tanzania wilayani Babati Joan Msuya, aliwataka wazazi kujipa uvumilivu wa kukuta kimwili kwa miezi mitatu tangu mama anapokuwa amejifungua.

"Suala la unyonyeshaji ni la kisaikolojia baba anatakiwa kuvumilia na kuepuka kumpa mkewe msongo wa mawazo, mama akijua mumewe anatoka nje ya ndoa maziwa huwa hayatoki hivyo kumsababishia mtoto udumavu," alisema Msuya.

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wenzake wanaonyonyesha Felista Munna (37), alisema elimu waliyopewa na World Vision kuhusu faida za unyonyesha imewasaidia kuimarisha afya ya mwili na akili kwa watoto wao.

Aidha, Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto mkoani Manyara, Emma Ngatoluwa, aliyataja matokeo ya utafiti wa masuala ya afya wa mwaka 2018 ulioonyesha mambo kadhaa kuhusu wanawake kunyonyesha mkoani humo.

# Mghwira atoa siri mlo kamili

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameitaka jamii kuzingatia kula mlo ulio kamili ili kujikinga na maradhi ukiwamo utapiamlo ulioonekana kuwakumba watoto walio wengi kwa siku za hivi karibuni hususani katika mkoa wa Kilimanjaro.

Akizungunza na wananchi wa Kijiji cha Maruwa kata ya Kirua Vunjo Magharibi katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro aliwahimiza wazazi kujikita katika kuziangalia lishe za watoto hasa kuanzia miaka sifuri hadi 12.

Alisema tafiti zinaonyesha kuwa katika mkoa huu ni miongoni mwa mikoa mitatu iliyofanya vizuri kiuchumi, lakini inakabiliwa na changamoto ya utapia mlo kwa watoto na lishe iliyozidi kwa watu wazima.

"Mkoa wa Kilimanjaro tunakabiliwa na changamoto ya utapia mlo kwa watoto na uzito uliozidi kwa watu wazima hii inaonyesha wazazi hawana muda wa kutosha na watoto wao, hivyo nawaagiza viongozi kwanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya kwa kushirikiana na maofisa ustawi wa jamii kuhakikisha mnatoa elimu kwa wananchi namna bora ya kupata lishe bora.

Alisema kutokana na changamoto hizi ni wajibu wa wazazi na walezi kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha watoto wanapata mlo ulio kamili na kwa wazazi watakaoshindwa kufanya hivyo hatua kali za kisheri ziweze kuchukuliwa.

Kwa upande wake mwakilishi wa mganga mkuu wa mkoa, Dk. Bogius Mwamgunda, alisema ni ukweli mkoa wa Kilimanjaro tunakabilia na changamoto za utapia mlo kwa watoto lakini jitiada mbali mbali zimeshachukuliwa ili kutokomeza changamoto hiyo.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hili imebainika kuwa baadhi ya wazazi hawana uelewa wa kutosha juu ya namna bora ya kuwalisha watoto licha ya kuwepo kwa kipato.

" Wapo baadhi ya wananchi wanatumia muda mwingi kufanya biashara na hawana muda wa kutosha kuwatizama watoto wao hali ambayo inapelekea watoto kutopewa lishe inayostahili hivyo kwa maagizo ya serikali mkuu wa mkoa tayari amesaini mkataba na watendaji wa kila halimashauri pamoja na watendaji wake ili kuona namna gani wanavyoweza kukabiliana na changamoto hiyo," alisema Dk. Mwamgunda.

Aidha, baadhi ya kinamama katika kijiji hicho, Ester Macha amesema kuwa licha ya wao kupewa elimu kliniki lakini bado changamoto ya utapia mlo haiwezi kuisha ikiwa serikali haitapiga marufuku wanawake kwenda katika maeneo ya pombe nyakati za jioni.

# DC awakumbuka waendesha Bajaj

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameahidi kutoa mkopo wa Bajaj 15 kwa waendesha bajaji wilayani humo ili kuwawezesha vijana hao kujiajiri na kuchangia pato la taifa.

Ole Sabaya alisema hayo wakati akizungumza na madereva bajaji wa Hai mjini katika kikao kilicholenga kufanya tathmini ya utatuzi wa changamoto zinazowakumba madereva hao zilizowasilishwa kwenye kikao cha awali kilichofanyika mwezi Mei, mwaka huu, kikiwakutanisha madereva bajaji na mkuu huyo wa wilaya.

Ole Sabaya amemtaka Mwenyekiti wa madereva Bajaj, Pendaeli Nkya, kuweka utaratibu wa wazi wa kupata majina ya madereva wanaohitaji mikopo ndani ya vikundi vyao ili wapatiwe mikopo hiyo na kuondoa changamoto zinazowakumba katika kazi hiyo.

Amesema kuwa baadhi ya changamoto zilizowasilishwa na madereva hao ni pamoja na ubovu wa baadhi ya barabara ikiwamo ya St. Dorkas iliyopo katika kata ya Muungano ndani ya mamlaka ya Mji Mdogo wa Bomang'ombe ambayo hivi sasa imeshaanza kufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe.

Aidha, amesema pamoja na kutatua kero hizo serikali itaendelea kuwa nao wakati wote na kwa changamoto zozote kwani madereva bajaji wanafanya kazi vizuri na kuwataka waendelee na uaminifu katika kazi yao.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Hai (DTO), Mbarouk Abdalah, alisema hali ya usalama barabarani kwa wilaya ya hiyo iko salama na kuwataka madereva kuendelee kuzingatia sheria za usalama barabarani na kuacha tabia ya kuzidisha abiria kwenye vyombo vyao jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao.

Na baadhi ya madereva wameishukuru serikali ya wilayani Hai kwa kusikiliza kero zao na kuzitatua kwa wakati huku wakimpongeza mkuu wa wilaya hiyo kwa kuwa mstari wa mbele katika kutetea wanyonge.

Mkuu wa Wilaya ya Hai mara ya mwisho alifanya mkutano na madereva hao ambapo alipokea kero mbalimbali zinazowakabili kwenye majukumu yao na kuendelea kutatua baadhi ya kero ikiwamo ubovu wa barabara unaosababisha kuharibu vyombo vyao ambazo hadi kufanyika kwa kikao cha pili barabara zote za maeneo ya Mji Mdogo wa Hai zimerekebishwa na nyingine zikiendelea kushughulikiwa.



Meneja wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) mkoani Manyara, John Mwigula, akizungumza na wadau wa madini wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro juu ya ulipaji kodi juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mamia ya wazee wanufaika kliniki maalum

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Anderson Memorial Rehabilitation and Care Organization (AMRCO), limeendesha programu maalumu ya kliniki kwa wazee wasiojiweza na watu wenye ulemavu kwa ajili ya vipimo vya magonjwa yasiyoambukiza.

Kliniki hiyo imeendeshwa kwa siku mbili hivi karibuni katika eneo la Longuo B Manispaa ya Moshi na Mwika Wilaya ya Moshi Vijijini ambako zaidi ya wazee na wenye ulemavu 300 walinufaika na kliniki hiyo.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Grace Saria, alisema vipimo vilivyotolewa kwa makundi hayo ni pamoja na magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu pamoja na vipimo kwa wenye magonjwa ya kinywa na meno.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, lengo la kutolewa kwa vipimo hivyo bure ni kuwawezesha watu wasiokuwa na uwezo wakiwamo wazee na walemavu kupatiwa huduma hiyo muhimu.

Shirika hilo lilianzishwa mwaka jana likiwa na lengo la kuwahudumia wazee na watu wenye ulemavu ikiwamo kuwatembelea kwenye makazi yao na kuainisha changamoto zinazowakabili.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa wazee wengi wanaishi na kutunzwa na vijana kutokana na watoto wao kukimbilia mjini kutafuta maisha hivyo vijana hao kutokuwa na stadi za namna ya kuwatunza hatua ambayo imewafanya kujitosa kuwapa vijana hao stadi za namna ya kuwatunza wazee hao.

"AMRCO iliona hilo pengo kwa hiyo tunashirikiana na baadhi ya watumishi wa kanisa na tunataka 'parishwakers' akienda kumpa chakula cha bwana huyo mzee amwangalie holistically na tunashirikiana pia na manesi na madaktari wastaafu walioko huko vijijini," amesema.

Alitoa wito kwa watu wanaoishi na wazee wasiojiweza pamoja na watu wenye ulemavu kutowaficha majumbani na badala yake wawe wakiwasaidia kuwapeleka kwenye maeneo husika ili wapatiwe vipimo ili kubaini changamoto za kiafya zinazowakabili.

Kliniki ya kwanza ilifanyika kwenye ofisi za shirika hilo zilizopo Kata ya Longuo B Manispaa ya Moshi, huku kliniki ya pili ikifanyika kwenye Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mwika Mrimbo Uuwo Dayosisi ya Kaskazini.

Kwa upande wake mmoja wa madaktari walioshiriki katika kliniki hiyo, Mrosso Leonard alisema kumekuwapo na changamoto nyingi kwa wagonjwa wa kisukari kusitisha matumizi ya dawa hatua ambayo imekuwa ikiwasababishia baadhi yao matatizo zaidi ya kiafya.

"Baadhi yao huacha kutumia dawa kutokana na kukata tamaa, lakini sababu nyingine ni kutokuwa na watu wa kuwasimamia kwa ukaribu wakati wa kutumia dawa hali hii kuwafanya kupata matatizo zaidi na wanapokuja kwenye hospitali zetu wanakuwa wameshaathirika zaidi kiafya," alisema.

Kwa mujibu wa daktari huyo, kuna uhitaji mkubwa wa wagonjwa wa kisukari na shinikizo la damu kutokana na wengi wao kutofikiwa na huduma za matibabu na kutoa wito kwa AMRCO kuendelea na kampeni hiyo kwa kuyafikia makundi ya wazee zaidi walioko vijijini.



## Viuatilifu vyakwamisha ulimaji pamba Malinyi

Ukurasa 19


# BUFE

Ijumaa Agosti 9, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA





## Mrajisi: Huu ndio Ushirika, umesimama 'damudamu' na sekta kilimo

Ukurasa 16



KILIMO NYANDA ZA JUU KUSINI

# Watafiti TARI walivyofungua kilimo darasa zawadi kuu kwa Nanenane

Ukurasa 14

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

### KILIMO NYANDA ZA JUU KUSINI

# Watafiti TARI walivyo… darasa zawadi kuu kw…

- Uyole yawaonyesha wakulima pa 'kutokea'
- Afrika: Tanzania ya 2 kunde, ya 4 mahindi

**Na Nebart Msokwa, Mbeya**

MIKOA ya Nyanda za Juu Kusini, imo katika maeneo yanayoongoza nchini kuzalisha mazao mbalimbali hata ikabatizwa jina la utani 'Ghala la Taifa la Chakula.'

Siri ya tija yao ni uwepo wa ardhi yenye rutuba na hali ya hewa nzuri, mvua inayoambatana na maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Hapo kunaorodheshwa utajiri wa mazao kama mahindi, mpunga na mihogo, ambayo kwa mujibu wa Wizara ya Kilimo, ina kipaumbele kwa taifa kuhakikisha nchi inajitosheleza kwa chakula na ziada inauzwa ugenini.

Pia, kuna mazao mengine kama maharage, soya, karanga, ulezi, mtama, ndizi, ngano, viazi. Mazao ya biashara ni kahawa, kakao, tumbaku, chai, alizeti, pareto na parachichi, inayozidi kushika kasi kwenye biashara ya kimataifa.

**Maonyesho Kilimo**

Mwanzoni mwa mwezi Juni mwaka huu, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Uyole, kwa kushirikiana na Baraza la Nafaka Ukanda wa Afrika Mashariki (EAGC) na kampuni za pembejeo za kilimo, ziliandaa maonyesho ya kilimo cha biashara, ambayo kwa mara ya kwanza yalifanyika mkoani hapa.

Ulingo wake ulikuwa katika mashamba ya Tari- Uyole, yalipowakutanisha wadau wa kilimo; wakulima, watengenezaji na wasambazaji pembejeo, wafanyabiashara wa mazao kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na wasindikaji mazao.

Taasisi zingine zikiwamo benki na taasisi za kiserikali zilishiriki kwenye mnyororo wa thamani wa mazao yaliyoshirikishwa.

Ulikuwa uwanja kwa wakulima kujifunza kwa nadharia na vitendo, kutoka kwa wataalamu wa kilimo, kuhusiana na mbinu za kuongeza tija kwenye uzalishaji na mashamba darasa yaliyoandaliwa kwa kufuata kanuni bora za kilimo.

**Mwenyekiti Bodi**

Mwenyekiti wa Bodi ya Tari nchini, Dk. Yohana Budeba, anawataka wakulima kuitumia taasisi hiyo na nyinginezo za utafiti, kupata elimu ya kilimo bora, ikiendana na mbegu zilizofanyiwa utafiti na kuthibitishwa na ubora na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu nchini (Tosci).

Anasema, endapo wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini watatumia vizuri stadi walizofundishwa kwenye maonyesho, kuna uwezekano mkubwa uzalishaji ukaongezeka maradufu na taifa kuuzamauzo nje ya nchi.

"Tukijitosheleza kwa chakula, tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuuza nje ya nchi ziada hasa baada ya kuongezwa thamani na hii itatusaidia kuinua uchumi wa taifa letu," anasema Dk. Budeba.

**Mkurugenzi Mkuu**

Mkurugenzi Mkuu wa Tari nchini, Dk. Geofrey Mkamilo, anasema lengo la maonyesho lilikuwa kuwafundisha wakulima



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Wiliam Ntinika (Kulia), akipata maelezo kutoka kwa watafiti wa mazao kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), Kituo cha Uyole kuhusu kilimo bora cha maparachichi wakati wa Maonyesho ya Kilimo na Biashara, yaliyofanyika jijini Mbeya. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

> **"Tukijitosheleza kwa chakula, tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuuza nje ya nchi ziada hasa baada ya kuongezwa thamani na hii itatusaidia kuinua uchumi wa taifa letu," anasema Dk. Budeba.**

mbinu bora na kuachana na kilimo cha kujikimu, badala yake wajikite katika kibiashara.

Anasema, ni maonyesho yaliyowakutanisha wakulima wa Nyanda za Juu Kusini na taasisi mbalimbali, aina ya teknolojia na elimu wanayohitaji, darasa linalopatikana kwa wakati na eneo moja, badala ya kuhangaika kuzitafuta.

Dk. Mkamilo anasema, zaidi ya kampuni na taasisi 10 zinazozalisha mbegu za mazao ziliandaa mashamba darasa ya kutoa nafasi wakulima kuchagua mbegu walizotaka, kulingana matokeo pamoja na ushauri waliopewa.

"Pia wakulima wamekutanishwa na wanunuzi wa mazao, ili kuwahakikishia soko la mazao wanayozalisha. Tunataka wakulima waachane na kilimo cha mazoea na badala yake walime kibiashara," anasema Dk. Mkamilo.

Msisitizo wake ni kwamba, wakulima wengi nchini wamekuwa wakilima maeneo makubwa,



# fungua kilimo a Nanenane

lakini wanaambulia mavuno kidogo, kutokana na kutumia teknolojia zilizopitwa na wakati, ilhali hawazingatii maelekezo ya wataalamu wao.

Anasema, mtazamo mpya wa mageuzi ni kwa wakulima kufundishwa kilimo katika eneo dogo, inayotumia teknolojia za kisasa, mbegu na mbolea sahihi, ili kupata makubwa yanayowaongezea kipato na kulinda mazingira.

**Meneja Nafaka**

Meneja wa Programu za Baraza la Nafaka Ukanda wa Afrika Mashariki nhini Tazania, Ikunda Terry anasema kazi kubwa ya baraza hilo nchini ni kuhamasisha biashara ya mazao ya wakulima katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Anasema, shirika hilo limekuwa likishirikiana na taasisi za utafiti katika kubuni mbinu zinazoongeza tija katika uzalishaji mazao na kwamba maonyesho hayo ya kilimo biashara, ni miongoni mwa njia walizobuni kusaidia kutimiza lengo.

Terry anarejea historia kuwa, ni muda mrefu maonyesho hayo yalikuwa yanafanyika katika Kanda ya Kaskazini, mkoani Arusha, ndipo wakaamua yafanyike katika Nyanda za Juu Kusini, kutokana na umuhimu wake taifa.



**“Asilimia 17 ya ardhi katika Ukanda wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ipo Tanzania. Pia, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 40 ya ardhi ya Tanzania inafaa kwa kilimo bado haijatumika ipasavyo,” anasema Terry.**

Anasisitiza Tanzania ni miongoni mwa mataifa yenye ardhi bora kwa kilimo, lakini haijatumika ipasavyo. Rai yake ni wakulima kutumia fursa ya maonyesho kuongeza uzalishaji wao shambani.

“Asilimia 17 ya ardhi katika Ukanda wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ipo Tanzania. Pia, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 40 ya ardhi ya Tanzania inafaa kwa kilimo bado haijatumika ipasavyo,” anasema Terry.

Terry anataja mafanikio ya Tanzania kuwa katika orodha ya nchi zinazoongoza kwa uzalishaji wa baadhi ya mazao kimataifa; zao la kunde inashika nafasi ya pili barani Afrika, nyuma ya Nigeria na duniani iko katika nafasi ya 10.

Vilevile anasema, kwenye uzalishaji mahindi Tanzania inashika nafasi ya nne barani Afrika, akitaja changamoto iliyopo, ni ubora wa chini kutokana na utunzaji duni wa baadhi ya wakulima, baadhi ya mazao yanakuwa machafu.

Ushauri wake ni Watanzania wazingatie teknolojia wanazofunzwa kwa kuzitumia kwenye uzalishaji, kuna uwezekano mkubwa ikaongoza barani Afrika.

**Sumu kuvu**

Mtafiti wa mazao kutoka Tari - Uyole, Leonard Sabula, rai yake ni wakulima wahifadhi mazao yao yakiwa yamekauka vizuri, kuepuka kuoza kunakosababisha sumu kuvu, ambayo ni hatari kwa afya ya mlaji.

Anawaasa wakulima kwamba kiwango cha unyevu kinachoruhusiwa kubaki ni asilimia 14, ndipo wanaweza kuhifadhi kwenye mifuko, wakihakikisha mazao hayagusi ukuta wala sakafu, ikiwa katika sehemu safi na kavu, kuepuka kutengeneza unyevu.

Lingine analoshauri ni wakazi kuepuka ulaji vyakula vyenye dalili za sumu kuvu, wala kulisha wanyama kwa madai sumu hiyo itawarudia walaji kupitia kula nyama iliyoathirika na sumu kuvu.

Sabul anadokeza kwamba, wanyama wanapokula nafaka iliyoathirika na sumu kuvu, huwa wanadumaa na kupunguza kiwango cha uzalishaji,

INAENDELEA UK. 18

# Njaa inakuja Burundi, Zimbabwe imeshafika

**Na Mwandishi Wetu**

HALI mbaya ya hewa, joto kuongezeka kumeleta athari nchini Burundi kuna shaka ya kuathiri kiwango cha uzalishaji chakula katika nchi hiyo.

Wataalamu waliokuwa jijini Geneva, Uswisi wanasema, joto hilo limevuruga mfumo wa uzalishaji chakula na upatikanaji wake, shida kubwa ni hali ya hewa.

Inaelezwa kitaalamu kwamba, katika orodha ya nchi 10 ambazo ziko hatarini kuvuna chakula kidogo duniani, inatoa kwa kiasi kikubwa hewa ya ukaa ambayo ina athari katika uzalishaji.

Katika hilo zinatajwa nchi tano katika ngazi ya juu ya hali mbaya zaidi ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Madagascar, Yemen na Sierra Leone.

Hapo zinafuatiwa katika orodha hiyo, na Chad, Malawi, Haiti, Niger na Zambia.

“Watafiti wetu wanaonyesha kuingzeka hewa ya ukaa angani inayoendana na kupungua tija ya chakula tunachokula, tukiwa ni watu tunaoumia zaidi na hili na ongezeko la hea ukaa,” anasema Dk. Samuel Myers, Mtafiti Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Harvard, Marekani.

Pia, kuna maoni ya watafiti wengine kwamba, ripoti yha kutokuwa na uhakika wa chakula, inawagusa matajiri na masikini, kwamba athari ya hali ya hewa inaendana moja kwa moja na uwezo wa jamii kujilisha

Mtaaluma Profesa Doreen Stabinsky, anahimiza kwamba vigezo vilivyopo vinaashiria hali si nzuri na kuna haja ya kuchukuliwa hatua

Wakati inaelezwa Burundi imo katika nafasi ya ‘kumi bora,’ ndugu zao wa Zimbabwe kumeshaharibika kwa watu zaidi ya milioni tano wamekumbwa na njaa na wanaendelea kutaabika.

Taarifa ya Umoja wa Taifa, inakiri hali ni mbaya, huku Mpango wa Chakula Duniani (WFP), imeanzisha kazi ya kukusanya Dola za Marekani milioni 331 kuwaokoa waathirika.

Mkuu wa shirika hilo, David Beasley, anasema suala hilo linapaswa kufanyika kazi katika mtazamo wa dharura.

Hiyo inaelezwa kwamba hali iliyotokea ni zao la ukame uliochukua sura katika nchi hiyo, huku bei ya mazao ikipanda maradufu.

Pia, kiwango cha maji kushuka katika maeneo ambako kunazalishwa umeme katika |Bwawa la Kariba na kupoteza umeme, ikizaa athari nyingine ya kiuchumi na kijamii.



Moja ya matukio ya ugawaji chakula nchini Burundi,. **PICHA: MTANDAO.**

UCHUMI

# Mrajisi: Huu ndio Ushirika, umesimama 'damudamu' na sekta jirani kilimo

## ...simulizi za soko, manunuzi, mtaji

**Na Mary Geofrey**

JANA ilikuwa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini, maarufu Nanenane. Uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa uko katika historia ya kushikiliwa na sekta ya kilimo, ambayo katika sura yake ya kufanikiwa, inashirikiana na sekta, vyombo na wadau wengi .

Ikiwa ni mwajiri zaidi ya theluthi tatu ya Watanzania, kilimo, chombo cha ushirika kilichotapakaa katika sehemu nyingi nchini, ni mdau wake wa karibu, ikichukua sura ya mtaji, muunganisho na masoko ambako ina nafasi kubwa.

Hapo inapozungumziwa ushirika, imeshikamana kupitia chombo kiitwacho, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Nchini. Hicho ni chombo muhimu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yake, chini ya uratibu wa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini,Tito Haule,

Anasema katika kutekeleza majukumu yake, inaongozwa na Mpango wa Maendeleo Endelevu, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa na miongozo ya kisheria, ikiwamo kilimo .

Haule anasema uhamasishaji uliofanywa na tume pamoja na wadau wengine wa ushirika kwa makundi mbalimbali ya kijamii nchini, umesababisha kuanzishwa na kusajiliwa vyama vya ushirika 2,377 kuanzia mwaka 2015 hadi Septemba mwaka jana.

Haule anasema ongezeko hilo limefanya jumla ya vyama vyote vya ushirika nchini kufikia 11,149 , Katika mjumuiko huo kuna Shirikisho la Vyama vya Ushirika; vyama vikuu vya ushirika 51; miradi ya pamoja 39; na vyama vya ushirika vya msingi 11,058, ambavyo vyote vina majukumu makubwa ikiwamo kukuza kilimo nchini

Anasema, katika taratibu za uongozi, wajumbe wa bodi wanapaswa kukaa madarakani kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu na kufanyika uchaguzi mwingine wa viongozi.

"Lengo la usimamizi wa chaguzi hizo ni kuhakikisha zinaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni za vyama vya ushirika vilivyopo.

"Tume imeendelea kutatua migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo ukosefu wa elimu juu ya dhana ya ushirika, kutofuata sheria na taratibu za uendeshaji wa vyama vya ushirika na ubadhilifu," anafafanua.

Haule anasema, pia wanashirikiana na Wizara za Kilimo, pia Ofisi ya Rais -Serikali za Mitaa na wadau wengine kuhamasisha Watanzania hususani vijana, wanawake na vikundi vyenye mwelekeo wa ushirika kujiunga au kuanzisha vyama hivyo vya ushirika.

Anasema tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masoko wakiwamo wa Bodi ya Leseni za Ghala, Soko la Bidhaa, Wakala wa Vipimo na bodi za mazao, zimeendelea kuvijengea vyama vya ushirika uwezo wa masoko ya bidhaa zake.



Mkulima Kenneth Mwang'amba, akiwajibika katika shamba lake la kahawa, wilayani Mbozi. Soko lao hupitia mlango wa Ushirika. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**USHIRIKA NA MKULIMA**

Haule anasema matumizi ya mifumo ya masoko, imechangia kuboresha mauzo na kuimarisha ushindani wa mazao ya kimkakati na mengine ya biashara, zikiwamo kakao, ufuta na miwa.

Pia, anasema mfumo wa ununuzi wa mazao ya kilimo unahusisha wakulima kukusanya kupitia vyama vya ushirika vya msingi, wakilenga masoko ya pamoja kwa njia ya minada au uuzaji moja kwa moja.

Aidha, Haule anasema ununuzi wa mazao ya mkulima kupitia vyama hivyo kunasababisha wakulima kuwa na nguvu ya pamoja ili kupata bei zenye tija; kuanzisha na kuendesha maghala na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yao.

Haule anaeleza mtazamo mkuu katika kilimo nchini, ni kuhakikisha inamsogezea mkulima vipaumbele vyake.

**STAKABADHI GHALANI**

Mdau maarufu wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, Michael Tsaxara, anasema ununuzi wa mazao kwa njia ya ushirika ni bora na umelenga kumsaidia mkulima kukaa mbali na urasimu uliokuwapo, hata kumfanya mkulima asinufaike na kilimo chake.

> **"Lengo la usimamizi wa chaguzi hizo ni kuhakikisha zinaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kanuni za vyama vya ushirika vilivyopo.**

"Ununuzi wa mazao kwa njia ya ushirika mkulima anapata fedha zake zote bila ya kuwapo kwa mtu wa kati, mathalani kwenye ufuta kupitia vyama vya ushirika zao hilo liliuzwa kwa Sh. 3,000 kutoka Sh. 1,800 iliyokuwa awali na wakulima wamepata faida," anasema.

Tsaxara anasema, kumekuwapo faida kubwa ikiwamo kudhibitiwa walanguzi wa mazao wanaopangia bei wenyewe na kutumia vipimo visivyohakikiwa, jambo lisilokubalika katika soko la mazao.

Katika hilo, anatoa mfano kwa kutoa pongezi kwenye msimamo wa Tume ya Taifa ya Ushirika, kutaka zao la dengu linunuliwe kwa njia ya mnada na si wakala au wafanyabiashara kununua kwa wakulima majumbani na mashambani.

Katika namna ya kujigamba, anasema mbadala umekuwa vyama vya msingi kujikusanya kutafutia masoko kwa pamoja.




Makao makuu ya vyama vya ushirika vya Kagera, mjini Bukoba na KNCU mjini Moshi, Kilimanjaro. Vyote vina historia ya mzizi mkongwe.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani(Corecu), Rajabu Ng'onoma, anaunga mkono kuwa uuzaji mazao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, umekuwa wa faida kubwa kwao.

Anataja faida hizo kuwa ni kuuza mazao kwa bei kubwa, tofauti na kila mkulima kuuza mazao kwa bei yake binafsi, ambayo wakati mwingine hawapati faida na inageukia kumnyonya mkulima.

**USHIRIKA VS MASOKO**

Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Titus Kamani, anasema wameendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda kupitia vyama vya ushirika na tayari vyama 108 vinamiliki viwanda vidogo na vya kati vipatavyo 166.

Anasema, ni lazima vyama vya ushirika kupitia kwa maofisa wake walioko nchini kote, kutafuta masoko yenye tija kwa manufaa ya wanaushirika kila waliko.

"Tafuteni watu wazuri wa kutafuta masoko mazuri ya mazao ya wana - ushirika na msiwe watazamaji, nawahakikishia mkipata soko zuri la zao, sisi tutatoa idhini mkauze popote.

"Lakini tunataka tuondoke kwenye kuuza mazao ghafi, tuuze mazao yaliyosindikwa ili kulinda ajira kwa watu wetu na kuongeza thamani ya mazao yetu," anasema Dk. Kamani.

Anasema zaidi kuwa: "Lazima mali za ushirika zirudi, viongozi orodhesheni mali za ushirika zilizo kwenye mikono isiyo sahihi zilizoshindwa kurudishwa, orodha iwasilishwe tume. Mali zote hasa ardhi na majengo zinazomilikiwa na ushirika zitafutiwe hati." Suala la ushirika linaenda mbali, kwamba linagusa mitaji midogo na mikubwa, kupitia vyama vya kuweka na kukopa vilivyoshika kasi nchini kote, pia baadhi ya benki na asasi za kifedha, kutoa mikopo kwa mkondo huo.

Pia, ni mtazamo ambao umekuwa na historia ndefu kuwaunganisha wanajamii kiuchumi, kijamii na hata kisiasa, kabla na hata baada ya uhuru wa Tanganyika.

Itakumbukwa, baadhi ya vyama vya ushirika mfano vya Bukoba mkoani Ziwa Magharibi (sasa Kagera) na KNCU ya Kilimanjaro inabeba historia pana, kupita uchumi na maendeleo kama ya elimu na siasa ya wakazi wake.

Hata katika kipindi kabla na baada ya uhuru, katika mfumo wa chama kimoja, ushirikika ulikuwa moja ya idara muhimu za vyama tawala wakati huo, Tanu na badaaye CCM.

Hivi sasa inashuhudiwa ushirika ulivyo mithili ya 'chanda na pete'na mfumo wa ununuzi katika kilimo nchini na uzalishaji mazao kama kahawa katika ,maendeo kama ya Kagera, Kilimanjaro, Wilaya za Mbiga (Ruvuma) na Mbozi mkoa wa Songwe.

# BIASHARA KATIKA PICHA




Ofisa Uhusiano wa Benki ya ABC Tawi la Dodoma, Dinah Titus (katikati), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dr Rehema Nchimbi (wapili toka kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dr Binilith Mahenge (kulia), walipotembelea banda la benki hiyo kwenye kilele cha Maonyesho ya Nanenane Kanda ya Kati yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma jana.



Mkuu wa Mkoa wa Singida Dr Rehema Nchimbi (kushoto) na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dr Binith Mahenge (wapilitoka kushoto)wakikagua shamba darasa la zao la tamutamu la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama Mkoani Singida ,kwenye maonesho ya sikukuu ya wakulima nanenane Kanda ya kati yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma jana



Meneja Mauzo kampuni ya Hughes Motrs, Lawrence Kisoka (kushoto), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dr Rehema Nchimbi (katikati) na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dr Binith Mahenge (kulia), walipotembelea banda la kampuni hiyo kwenye maadhimisho ya Sikukuu ya Nanenane Kanda ya Kati yaliyofanyika viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma jana. **PICHA ZOTE: IBRAHIM JOSEPH**

UCHUMI

mathalani maziwa kwa ng'ombe.

"Mazao yetu yakishakuwa na hali ya sumu kuvu yanapoteza ubora na hayawezi kupata soko. Hivyo, tuyakaushe vizuri ili yasiathirike na kuvu hao, lakini ikitokea yakawa yameshaathirika, tusiwalishe hata kuku, maana sumu hiyo ni hatari," anasema Sabula.

Anaisifu asasi anayotumikia kwamba, inawalisha Watanzania mbegu bora za mazao, zilizofanyiwa tafiti na kuna maabara yenye vipimo vya kisasa kupima ubora wa udongo.

**Mkurugenzi Uyole**

Mkurugenzi wa Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, anadokeza kuwa uhakika wa chakula na kipato cha mkulima, unaanzia kwenye uhakika wa pembejeo, zikiwamo mbegu bora za mazao.

Anasema lengo la Kituo cha Uyole, ni kuwaleta wadau pamoja kupatawa njia tofauti, ikiwamo ya kilimo biashara, ili waweze kushirikiana na kuongeza uzalishaji unaohakikisha upatikanaji mbegu bora za kilimo na pembejeo zingine.

Anasema Kituo cha Uyole kimejipanga kuwahudumia Watanzania kukuza uchumi na kipato cha mtu mmoja mmoja, kupitia mnyororo wa thamani shambani.

"Maonyesho haya ni mwanzo tu, tutafanya maonyesho mengine mengi na makongamano mbalimbali ili kuhakikisha wakulima wanapata elimu ya kutosha na kuinua kiwango cha uzalishaji hivyo tunawakaribisha wananchi kwenye kituo hiki," anasema Dk. Bucheyeki.

**DC Ntinika ashauri**

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliyewakilisha Mkuu wa Mkoa Mbeya, Albert Chalamila anawashauri wataalamu wa kilimo kufikisha teknolojia kwa wakulima.

Anawataka pia wataalamu kufikisha utafiti wao kwa wakulima na kuziweka katika lugha inayoeleweka, ili wananchi washawishike kuzitumia shambani na kufuatilia matokeo yake.

Ntinika anawataka wananchi kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo, itakayowasaidia kuepuka madhara yanayohusu viuatilifu na mbolea kwa jumla.

Vilevile, anawashauri wananchi wa Kanda ya Nyanda za Juu kuitumia fursa ya soko la mahindi lililotafutwa na Rais Dk. John Magufuli kuzalisha mazao hayo kwa wingi, ili nao wapate kupenya katika fursa hiyo.

Kaimu Mkuu huyo wa Mkoa wa Mbeya, anawapa mbinu wazalishaji na waagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi na wafanyabiashara wa mbolea, kuhakikisha wananchi bidhaa zao zinafika kwa wakati, ili waendane vizuri na kalenda ya misimu ya kilimo.

**Waziri Hasunga**

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, katika hilo anawataka wakulima wazalishe mazao mbalimbali kwa wingi, pasipo kuhofu kukosekana soko, kwani lipo la uhakika katika dirisha la ndani na nje ya nchi.

Anasema Wizara hiyo kwa sasa imeunda timu maalumu za kutafuta masoko ya mazao katika mataifa mbalimbali ili kuhakikisha kila zao ambalo wananchi wanazalisha linapata soko la uhakika. Waziri anasisitiza kwamba kilimo ni sekta inayoajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, ndio maana serikali inajitahidi kuweka kwenye sekta ya kilimo kwa kuingizia ruzuku kwenye pembejeo za kilimo, kujenga miundombinu ya umwagiliaji na maghala ya hifadhi.

"Hivi tunatarajia kuanzisha bima ya mazao ili wakulima wafidiwe mazao yao yanapoathiriwa na majanga," anasema Waziri Hasunga.

Anawataka wananchi kuvutumia vituo vya utafiti wa mazao kujifunza mbinu za kilimo bora, kuhudhuria maonyesho ya kilimo yanayofanyika nchini, ikiwamo maonyesho ya wakulima ya Nanenane, ambayo kilele chake kilikuwa jana, ikilenga wajifunze



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (wa pili kushoto), akiwa na maofisa wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), wakisikiliza maelezo ya wazalishaji wa mbegu bora za mazao wakati wa maonyesho ya kilimo biashara yaliyofanyika jijini Mbeya. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

## KILIMO NYANDA ZA JUU KUSINI

# Watafiti TARI walivyofungua kilimo darasa zawadi kuu kwa Nanenane

> **"Anawataka pia wataalamu kufikisha utafiti wao kwa wakulima na kuziweka katika lugha inayoeleweka, ili wananchi washawishike kuzitumia shambani na kufuatilia matokeo yake.**



Wakulima kutoka mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wakipata mafunzo ya kilimo bora cha mahindi katika moja ya mashamba darasa ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari) Kituo cha Uyole, jijini Mbeya. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

UCHUMI

Na Lazaro Mateko



Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Majura Kasika (kulia), akivuna pamba shambani mwishoni mwa wiki, akiwa na mkulima wa wilayani humo, Meshack Majebele. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viuatilifu vyakwamisha ulimaji pamba Malinyi

## Mayowe ya kukata tamaa yasikika

SERIKALI imeshaamua kuzipa kipaumbele sekta ya kilimo nchini, kwa kuchagua mazao matano ya kibiashara inayoyawekea mkazi kwa ajili ya kujipatia fedha za kigeni na kuinua uchumi wa wakulima kwa ujumla.

Mazao hayo matano ya kibiashara ni pamba, tumbaku, korosho, chai na kahawa, ambayo imekuwa ikijitahidi kuimarisha uzalishaji wake.

Pia, kuna mazao ya kupewa kipaumbele katika uzalishaji; katani, ufuta, alizeti, mbaazi na ngano.

Lengo kuu la serikali katika eneo hilo, ni kupata fedha za kigeni itakayoinua uchumi wa wakulima kwa ujumla na imekuwa ikiwataka viongozi wa wilaya na mikoa hiyo kusimamia kilimo cha mazao matano ya kibiashara.

Malinyi ni moja ya wilaya zilizochangamkia kilimo cha mazao hayo ya kibiashara mkoani Morogoro na hasa pamba, katika msimu wa mwaka 2017/2018 na kulima hekta 297 za zao hilo katika msimu huo.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Malinyi, Martin Mhode, anasema wakulima wamejikuta wakipata mavuno kidogo kuliko walivyotarajia, hali iliyowakatisha tamaa na kulazimika kulima hekta chache katika msimu huu wa mwaka 2018/2019.

**MATARAJIO**

Mhode anasema, msimu uliopita wa mwaka 2017/2018, wakulima walilima hekta 297 na walitarajia kupata tani tani 372. 05 za pamba, lakini wakavuna tani 32. 58 ambayo ni sawa na asilimia 8.8 ya matarajio.

"Hali hiyo ilitokana na kutumia viuatilifu visivyo na ubora, ambavyo vilichangia kuvuna pamba mbovu na kusababisha wakate tamaa, ingawa msimu huu vimeletwa viuatilifu vizuri," anasema Mhode. Anasema, miongoni mwa wakulima walioathiriwa na ubovu wa viuatilifu hivyo, ni mkuu wa wilaya hiyo, Majura Kasika, aliyelima ekari 10 na kuishia kupata kilo 1700 tu, ambazo ni sawa na asilimia 17 ya matarajio yake.

"Lakini msimu huu wakulima wamepata viuatilifu, ambavyo vimesaidia wavune pamba safi, tofauti na msimu uliopita ingawa hawakujitokeza wengi kutokana na changamoto za msimu uliopita," anasema.

Anasema, utumiaji wa viuatilifu visivyo na ubora umesababisha ukosefu wa mazao na hata soko na hivyo baadhi yao kutolima pamba msimu huu, na lakini serikali ya wilaya bado ina jukumu la kuhimiza kilimo hicho.

Ofisa kilimo huyo anasema, kutokana na hali hiyo, msimu huu wa 2018/2019 zimelimwa hekta 83.6 na matarajio yao ni kupata tani 104.5 kwa vile baadhi ya wakulima walikata tamaa baada ya changamoto za msimu uliopita.

"Changamoto hizo haziwezi kutukatisha tamaa bali tutaendelea kusimamia jambo hili ili kuhakikisha kwamba hazijirudii tena ili wakulima wanufaike na kilimo cha pamba na pia nchi iinuke kiuchumi," anasema.

**DC AHAMASISHA**

Mkuu wa Wilaya hiyo, Majura Kasika, anasema yeye ni miongoni mwa waliolima pamba simu huu kwa ajili ya kuhamasisha wakulima wasikate tamaa kwa sababu ya vya kua wadudu visivyo na ubora walivyopewa msimu uliopita.

Anasema msimu huu pamba imepasua vizuri na ni nyeupe na yenye ubora, na kwamba mikakati ya kuhimiza kilimo cha zao hilo wilayani humo bado inaendelea kusimamiwa kwa vitendo na viongozi wa wilaya.

"Mimi nimeonyesha kwa vitendo kwa kulima ekari mbili za pamba kama njia mojawapo ya kuhamasisha wakulima waendelee kujitokeza kwa wingi kulima zao hilo msimu ujao," anasema Kasika.

Anafafanua kuwa, kilimo cha pamba kilikoma wilayani humo katika zama za miaka ya 1990, kutokana na changamoto mbalimbali zilizosababisha wakulima kukopwa mazao yao na wengine kufariki dunia bila kulipwa fedha zao.

"Kilichosababisha wakulima kuhamia kwenye zao la mpunga kama la biashara, iliwafanya wavamie hifadhi ya bonde la mto Kilombero lililohifadhiwa kama pori tengefu," anasema.

> "Lakini msimu huu wakulima wamepata viuatilifu, ambavyo vimesaidia wavune pamba safi, tofauti na msimu uliopita ingawa hawakujitokeza wengi kutokana na changamoto za msimu uliopita," anasema.

Anasema uvamizi huo na kuendesha shughuli za kibinadamu, ulisababisha kupoteza uoto wa asili wa bonde hilo ambalo linachangia asilimia 65 ya maji yanayoenda Bonde la mto Rufiji, ambako kuna mradi mkubwa wa serikali unajengwa wa kuzalisha umeme wa maji megawati 2115.

"Jitihada kubwa zimefanywa na ofisi yangu ili kuhakikisha wakulima wote waliovamia bonde hilo kwa ajili ya kilimo cha mpunga wanaondoka huko na kujikita zaidi katika mazao ya biashara ikiwamo pamba," anasema.

Anasema, kutokana na umuhimu wa kuhifadhi bonde, kwa miaka mitatu sasa serikali ya wilaya inaendelea na operesheni ya kuokoa bonde na baioanuwai zake ikiwamo wanyama aina ya Sheshe ambao anasema imethibitika kuwa wako katika bonde la mto Kilombero pekee.

**ULIMAJI PAMBA**

Zao la pamba inalimwa kwa wingi kwenye baadhi ya mikoa, hasa ya kanda ikiwamo Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Mara, Geita na mengine kwa uchache kama Tabora, Singida, Tabora, Pwani, Kigoma, Katavi na Morogoro.

Wenyeji wa mikoa ya kanda ya ziwa wamekuwa wakiita pamba kwa jina la dhahabu nyeupe, kutokana na ukweli kwamba ndilo zao kuu la biashara ambalo wamekuwa wakilitegemea kiuchumi.

Hata hivyo, kilimo cha pamba kimekuwa kikikumbata na changamoto nyingi ikiwamo kutumia viuatilifu visivyo na ubora, bei kuwa chini na hata ukosefu wa soko la uhakika la zao hilo, na kusababisha wakulima kukata tamaa.

Tangu miaka hiyo ya 1990, pamba ilikuwa miongoni mwa mazao yaliyokosa mwelekeo na kukosa mchango wa maana katika pato la taifa, lakini sasa serikali imelivalia njuga ili kuhakikisha inarudi kwenye hadhi.

Tangu kupatikana uhuru mwaka 1961, pamba ilikuwa miongoni mwa mazao makuu ya biashara yaliyotajwa, huku mengine yakiwa ni tumbaku, kahawa, pareto, katani, korosho na ufuta.

Pamba limekuwa zao linalokumbwa na changamoto nyingi ambazo serikali imekuwa ikijitahidi. Hivyo bado kuna matumaini kwamba baadaye wakulima watanufaika na zao hilo.

UCHUMI

Na Mwandishi Wetu

# Mbegu bora zilivyowaamsha kwa mara ya pili walima miti Mufindi

## • Neema ya misonobari na mikaratusi



Miche ya miti ikiwa shambani wilayani Mufindi. **PICHA: MTANDAO**

KWA Aidan Fitavangu, kilimo cha miti ni kila kitu kwake, kama ilivyo kwa wakazi wenigne wa kijiji cha Nzinyi, wilayani Mufundi, ambako ni umbali wa kilomita 600 kutoka soko kuu la jijini Dar es Salaam

Anakitazama kilimo hicho kama nyenzo muhimu katika kupambana na umasikini maeneo ya milimani na anaendelea:"Katika miaka ile nilikuwa ninakiangalia kilimo cha miti kuwa kinaweza kuwa moja ya miradi yenye tija katika kilimo kijijini hapa."

"Tulikuwa tumezoea kilimo cha chai na nafaka kama chanzo cha mapato, lakini sasa miti imeanza kutuonyesha njia mbadala," anaeleza Fitavangu, huku amejikita katika kazi ndogo kwenye shambani lake la ekari tatu na nusu.

"Nilianza kilimo hiki miaka michache iliyopita na ndoto zangu zinaelekea kutimia. Nina matarajio makubwa kwenye kilimo hiki. Haikuwa rahisi kwangu kuingia katika kilimo hiki hadi nilipoelezwa kuhusu matumizi ya mbegu bora za miti," anasema.

Fitavangu, baba wa watoto watatu na muumnini wa biashara ya kilimo cha miti, anabainisha kuwa mbegu bora za miti ni muhimu kuwezesha mavuno bora na kipato zaidi. Huku akiwataka wakulima wenzake katika eneo hilo kuanza kilimo cha miti kwa kutumia mbegu bora ili kupata manufaa ya haraka, anatamka: "Ninatarajia kuvuna miaka michache ijayo kwa kuwa nimetumia mbegu bora.

"Uzalishaji mbegu za miti ni hatua muhimu kwa mnyororo wa thamani, kama ambavyo huwezi kuoka mkate mzuri kwa unga mbovu. Kadhalika, unahitaji mbegu bora ili miti ikue sawa sawa."

Anasema mbegu bora za miti, zinatoka kwenye vitalu vilivyopandwa kitaalamu kutoka vyanzo vinavyojulikana vya miti iliyoboreshwa na ina uwezo mkubwa wa kukua vizuri.

Pia, Fitavangu anasema mbegu hizo zenye ufanisi zinasaidia kuondoa hisia kwamba 'kilimo cha miti hakilipi' kwa kuwa kinachukua muda mrefu kukomaa kati ya miaka 15 hadi 20.

### MBEGU MPYA

Mwakilishi wa asasi ya Jambe Agro, Stephen Salum ana ufafanuzi: "Vifaa vya kupandia na huduma za kuwapa wakulima wa ngazi zote utaalamu na ujuzi unaweza kuongeza ubora wa msitu."

Salum anasema, huwa wanawawezesha wakulima wa miti kuongeza kipato cha ngazi ya kaya, ikiwa na ziada kulinganishwa na matumizi ya mbegu za kawaida.

Mageuzi hayo ya mbegu yanaelezwa kuwezesha mkulima kupanda hadi kuvuna katika kipindi cha miaka kati ya mitano hadi saba tu, huku Salum anatoa mfano wa miti milingoti ya umeme, inayotofautiana kulingana na aina ya mti anaolima akifurahia tija .

Anafafanua, mbinu kwamba matumizi ya mbegu bora yanapaswa kwenda sambamba na mbinu za kisasa za ukulima, ikiwamo kutumia mbolea na kupanda kwa umbali unaotakiwa kitaalamu.

> **"Tunachukua jukumu la kusambaza mbegu zilizoboreshwa na mbinu za ukulima wa kisasa kuongeza ubora wa mazao ambao kwa kufanya hivyo pia tunaongeza tija na kipato kwa mkulima," anasema.**

"Tunachukua jukumu la kusambaza mbegu zilizoboreshwa na mbinu za ukulima wa kisasa kuongeza ubora wa mazao ambao kwa kufanya hivyo pia tunaongeza tija na kipato kwa mkulima," anasema.

Salum anadokeza kwamba upandaji miti kama mikaratusi na misonobari ina nafaida kubwa ya 'kumtoa' mkulima kiuchumi kutokana na kuwapo soko kubwa, akiinyooshea kidole mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya.

### MITI SHAMBANI

Salum anasema, unapofanyika upandaji wa miti bora pembezoni mwa mshamba, chanzo kizuri cha mbegu bora za miti kwa wakulima wenyeji, wenye nia ya kuanza ukulima wa kisasa wa miti.

Kutokana na hilo, kuchagua chanzo sahihi cha mbegu za miti ni jambo muhimu kwa mkulima anayetaka kuanzisha mradi wa ukulima wa miti ya kisasa, huku akisisitiza kwamba upandaji una mengi ya tija, ukijumuisha upatikanaji na hali ya hewa. "Ikiwa ubora wa kijenetiki kwa mbegu haukubaliani na mazingira zinapopandwa, basi sio rahisi kuboresha mazao yatakayotokana na mbegu hizo na hutumia gharama akubwa," anasema.

Ukulima wa miti nchini, unaelezwa bado una changamoto ya kukosekana uzalishaji unaotosheleza mahitaji, upatikanaji wa mbegu

> **"Wakulima wengi wa miti wakubwa kwa wadogo, hawajui uwepo wa manufaa ya mbegu bora za miti, uwepo wa vifaa bora vya upandaji na hakikisho na ubora wa miche," anasema Charles Tizeba, alipokuwa Waziri wa Kilimo.**

bora na jenetiki misituni.

Anaeleza wasiwasi wake katika eneo la wazalishaji kuwa hawana vitalu binafsi na wanaegemea mbegu zinazogawiwa kiholela na zilizokosa ubora.

### KIONGOZI ALIPONENA

"Wakulima wengi wa miti wakubwa kwa wadogo, hawajui uwepo wa manufaa ya mbegu bora za miti, uwepo wa vifaa bora vya upandaji na hakikisho na ubora wa miche," anasema Charles Tizeba, alipokuwa Waziri wa Kilimo.

Ni kauli yake katika kuelezea ubora za mbegu kama jambo la msingi katika kuongeza tija katika kilimo. Tizeba anasema: "Ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa mnyororo wa ugavi wa pembejeo unafanya kazi vizuri,"

Kwa mujibu wa Taarifa ya Upatikanaji Mbegu Tanzania ya Mwaka 2017, tasnia ya mbegu nchini ina mifumo miwili; rasmi na usio rasmi.

Mfumo rasmi, unaelezwa ni kwa mkulima anazalisha, anavuna na kisha anatunza na kusambaza mbegu kutika msimu mmoja wa kilimo hadi mwingine.

Kutokana na sababu kama vile ukosefu wa ujuzi na aina za mbegu, pia upungufu wa rasilimali za kumwezesha mkulima kununua mbegu na kutofikika kwa masoko, wakulima wadogo wengi nchini bado wanategemea mfumo usio rasmi.





# Chadema yapata Naibu Meya Mbeya

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

DIWANI wa Kata ya Sinde (Chadema), katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Fanuel Kyanula, amechaguliwa kuwa Naibu Meya wa Jiji hilo baada ya kumbwaga mpinzani wake, Juma Changani wa CCM.

Uchaguzi wa Naibu Meya ulifanyika juzi na Kyanula kushinda kwa kupata kura 27 huku mpinzani wake akiambulia kura 15 na hivyo kutetea nafasi hiyo kwa mara ya tatu mfululizo.

Akizungumza baada ya kutangazwa kuwa mshindi katika uchaguzi huo, Kyanula aliwashukuru madiwani wa halmashauri hiyo kwa kumwamini na kumchagua kuwa kiongozi wao kwa mwaka wa tatu mfululizo huku akisisitiza anaendelea kuimarisha mshikamano.

Alisema ataendelea kusimamia posho na stahiki za madiwani ili zipatikane kwa wakati na vikao vyote vinavyohitajika kwa mwaka vifanyike katika muda mwafaka.

"Halmashauri yetu ni miongoni mwa halmashauri zenye utulivu na utengamano wa hali ya juu, hii ni kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya madiwani wa pande zote mbili pamoja na wataalamu wetu, hivyo nitahakikisha hali hii inaendelea kutamalaki," alisema Kyanula.

Aidha, aliahidi kumshauri vizuri Meya wa Jiji Mchungaji David Mwashilindi, ili aendelee kuongoza vizuri na kuifanya Mbeya kuwa ya mfano kitaifa.

Kwa upande wake Changani ambaye alikuwa mpinzani wa Kyanula, alikiri kushindwa kihalali katika uchaguzi huo kwa maelezo kuwa kura zake hazikutosha kumfanya awe Naibu Meya wa Jiji hilo huku akiwashukuru waliopigia kura.

Alisema ataendelea kushirikiana na wenzake katika kuwaletea maendeleo wananchi kama walivyowaamini wakati wa uchaguzi mkuu uliofanyika mwaka 2015.

"Nashukuru sana kwa wale ambao mmenipigia kura kwenye uchaguzi huu, naamini mlikuwa na imani kuwa ningeweza kuwa kiongozi wenu, lakini ndio hali halisi iliyotokea kwamba kwenye uchaguzi wowote kuna kushinda na kushindwa, naomba tuendelee kushirikiana," alisema Changani.

Akizungumza baada ya uchaguzi huo, Meya wa Jiji hilo Mchungaji Mwashilindi ambaye ndiye aliyeusimamia alimpongeza Kyanula kwa kushinda katika uchaguzi huo huku akimpongeza pia Changani kwa kutimiza haki yake ya kikatiba.

Aliwataka madiwani kuendelea kushirikiana na wataalamu wa halmashauri ili kuhakikisha mipango yote ya maendeleo wanayopanga inafanikiwa kikamilifu na kuendeleza utulivu uliopo ndani ya halmashauri hiyo kwa sasa.

Aidha, aliwataka madiwani kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri kuendelea kushirikiana na wazazi katika ujenzi wa vyoo kwenye shule za msingi na sekondari ndani ya jiji hilo ili kupunguza tatizo hilo.

"Jiji letu lina changamoto kubwa ya vyoo hasa kwenye shule zetu za msingi, sasa wenye jukumu la kumaliza tatizo hilo ni sisi madiwani kwa kushirikiana na wazazi, hivyo nawaombeni tujitahidi kupunguza tatizo hilo," alisema Mwashilindi.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (kulia), akikagua baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenye Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) ambayo kikanda yanafanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# TBS yaondoa tozo ya nembo

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS) limetangaza msamaha wa tozo za kupata nembo ya ubora kwa bidhaa za wajasiriamali wenye nia ya kuanzisha viwanda vidogo.

Watakaopata msamaha ni wale watakaokidhi vigezo, lengo likiwa kuwarahisishia wananchi kazi ya kuanzisha viwanda na kutekeleza sera ya serikali ya uchumi wa viwanda.

Hayo yalisemwa jana na Mkaguzi wa Ubora wa TBS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Yekonia Sanga, wakati alipokuwa anazungumza na wajasiriamali waliojitokeza kwenye Maonyesho ya Nanenane kikanda yanayofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Alisema lengo la kuondoa tozo hiyo ni kuwasaidia wananchi wanaoanzisha viwanda vingi vya kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo zitauzwa ndani na nje ya Tanzania na kuongeza ushindani katika soko.

Alisema wajasiriamali hao watahudumiwa bure kuanzia hatua za awali mpaka wanapopewa alama ya ubora ambayo wataitumia bure kwa muda wa miaka mitatu.

"Sasa tunawakaribisha wajasiriamali wadogo wote kujitokeza kuja kuomba matumizi ya nembo hii bila malipo yoyote, tunataka wale wote wanaotaka kumuunga mkono rais wetu kwenye huu uchumi wa viwanda basi wamuunge kwa vitendo," alisema Mhandisi Sanga.

Baadhi ya wanufaika waliojitokeza kwenye banda la TBS kwa ajili ya kujifunza walisema hatua iliyochukuliwa na shirika hilo itawezesha bidhaa wanazozalisha kuaminiwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Ledia Amos, alisema utaratibu huo pia utawasaidia kukuza viwanda ambavyo kwa muda mrefu vilikuwa vinashindwa kuimarika kutokana na kukosa nembo ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Aliliomba shirika hilo kuwasaidia pia upatikanaji wa nembo hiyo ya ubora pindi wanapoomba ili wawe na uhakika na kile wanachozalisha kuwa kitapata soko.

# Kweleakwelea watishia wakulima wa mpunga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mpunga katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameomba wataalamu wa kilimo kuwasaidia mbinu za kisasa za kukabiliana na ndege wa kweleakwelea wanaoharibu mazao shambani.

Walitoa kilio hicho juzi walipokuwa kwenye Maonyesho ya Wakulima ya Nanenane yanayoendelea katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, wakisema ndege hao ndiyo changamoto kubwa kwa sasa.

Mmoja wa wakulima hao, Batazan Lusigi, alisema ndege hao wanavamia mashamba ya mpunga wakiwa katika makundi makubwa na wanaharibu mpunga na kusababisha upotevu mkubwa wa zao hilo.

Alisema wanalazimika kuishi mashambani muda wote kufukuza ndege hao badala ya kufanya shughuli nyingine na kwamba kutokana na baadhi ya mashamba kuwa makubwa wanalazimika kutumia rasilimali kubwa kuyalinda. "Ndege hawa huanza kushambulia mashamba mpunga ukianza kutengeneza mbegu ambazo zinakuwa na maziwa ndani na wanaweza wakala hata nusu ya ekari, lakini pia mpunga ukisha kauka ndio wanaharibu zaidi maana wanakula na wanaporuka wanapukutisha mpunga ambao hatuwezi kuokota," alisema Lusigi.

Alisema wakulima wanaingia hasara kubwa kwa madai kuwa ndege hao huwasumbua kwa muda wa miezi mitatu mfululizo kuanzia mwezi Machi mpaka Mei na kwamba huwa wanawafukuza kwa kupiga kelele mashambani.

Ofisa Kilimo mstaafu, Nuhu Mchame, anayejihusisha na utafiti wa kweleakwelea alisema ndege hao wanatabia ya kutembea katika makundi makubwa yanayofikia hata milioni moja. Alisema utafiti unaonyesha kuwa ndege hao husababisha uharibifu unaofikia asilimia 75 ya mazao ndani ya mashamba ya wakulima na hivyo kuwakosesha mavuno yanayokuwa yanakusudiwa.

Alisema ndege hao wana tabia ya kuhama hama kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta chakula na kwamba wanakula kwa kasi kubwa na kwamba endapo ikatokea mkulima akazembea kuna uwezekano asivune kabisa.

"Hawa ndege kwa Mbarali wanapatikana katika Bonde la Usangu, Mbarali yenyewe na Madibila, wanapotua shambani wanaharibu na wanaporuka wanaharibu vilevile, lakini pia ndege mmoja anakula gramu tano mpaka nane kwa siku. Sasa kutokana na ukubwa wa makundi yao, wanasababisha hasara kubwa," alisema Mchame.

Akizungumzia changamoto hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema wanashirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Wizara ya Kilimo kusaidia wakulima kupunguza ndege hao kwa kuwaua.

Alisema wanawaua kwa kuwamwagia sumu lakini changamoto inayowakabili ni ndege hao kuzaliana na kujificha ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambako sheria za uhifadhi haziruhusu kuwaua wakiwa hifadhini.

Alisema mbali na ndege hao kuwaathiri wakulima pia halmashauri inaathirika kwa mazao kupungua kutokana na ukweli kuwa asilimia 80 ya mapato ya halmashauri yanatokana na kilimo.



# Vyuo vyapewa miezi 3 kutoa vyeti

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, ametoa muda wa miezi mitatu kwa baadhi ya vyuo vya afya nchini kuhakikisha vinatoa vyeti kwa wahitimu wao wa miaka ya nyuma.

Agizo hilo alilitoa jana wakati alipokuwa akizungumza na uongozi pamoja na wanachuo wa Chuo cha Dodoma Institute of Health and Allied Sciences (DIHAS), jijini hapa.

Dk. Chaula alitoa muda huo kwa baadhi ya vyuo vya afya nchini kuhakikisha wanakamilisha kutoa vyeti kwa wahitimu waliomaliza masomo yao kwenye vyuo hivyo miaka ya nyuma haraka vinginevyo watawajibishwa kwa uzembe.

"Miaka ya nyuma kulikuwa na changamoto ya kucheleweshwa kwa vyeti vya wahitimu wa vyuo vya afya hapa nchini, lakini kwa sasa tulishaanza kulishughulikia hili, hivyo nawataka wakuu wote wa vyuo ambavyo havijakamilisha kuhakikisha wahitimu wao wanapatiwa vyeti hivyo maana ni haki yao," alisema.

Alisema kukosekana kwa vyeti hivyo vimeendelea kuwanyima fursa wahitimu hao waliomaliza masomo yao kwenye vyuo hivyo miaka ya nyuma kuwasababishia kukosa haki yao ya kupata ajira.

Alibainisha kuwa kuna jumla ya vyuo vya afya 77 hapa nchini na kipindi cha miaka ya nyuma vyeti vya wahitimu hao vilikuwa vikicheleweshwa kutokana na wakuu wa vyuo husika kutopeleka majina ya wahitimu wizarani.

Vile vile, aliwataka wakuu hao kuwa wabunifu katika kujiongezea mapato ili kutoa huduma za vyakula kwa wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo hivyo hata kama kwa kuongeza ada.

"Tunatoka kwenye mazingira tofauti haiwezekani mwanafunzi anasoma huku anafikiria namna ya kupata chakula, jitahidini kuangalia ili huduma ya chakula na malazi vyote vipatikane hapa kwa lengo la kupunguza usumbufu," alisema. Hata hivyo, aliwataka wanafunzi wanaohitimu katika vyuo hivyo vya afya kuonyesha mabadiliko katika kuihudumia jamii.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo hicho, Rehema Mligo, alisema idadi ya wanafunzi waliopo chuoni hapo kwa fani zote ni 257 na walimu 15 na watumishi wengine ambao sio walimu ni wanane na wengine watatu kutoka nje ya chuo.

Mligo alisema Taasisi hiyo ya Sayansi shirikishi Dodoma, zamani ilikuwa ikiitwa Chuo cha Uuguzi na Ukunga Mirembe na kilianzishwa Julai mwaka 1973 kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kwa wauguzi wa afya ya akili.

Alisema toka 1973 hadi 2008 fani zilizokuwa zikitolewa ni uuguzi wa kujiendeleza kwa ngazi ya stashahada na shahada ya juu ya uuguzi wa magonjwa ya akili kwa muda wa miaka miwili.

Kadhalika alisema tangu mwaka 2008 hadi 2014 chuo hicho kilianza kutoa mafunzo ya kujiendeleza kwa njia ya masafa ya uuguzi kutoka mikoa mbalimbali.

Alibainisha baadhi ya changamoto zinazokikabili chuo hicho kuwa ni upungufu wa majengo, vyumba vya madarasa, mabweni, miundombinu ndani ya chuo pamoja na upungufu wa watumishi.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Tiba, Dk. Zainab Chaula, akizungumza na wanachuo wa Chuo cha Wauguzi Milembe, jijini Dodoma juzi, alipotembelea kwa ajili ya kusikiliza na kubadilishana mawazo na wanachuo hao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# GFF yatoa msaada wa madawati Sekondari ya Kinyasi

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalojihusisha na kuhudumia makundi mbalimbali katika jamii (GFF) limetoa msaada wa madawati 50 katika Shule ya Sekondari Kinyasi, Kata ya Kinyasi wilayani Kondoa mkoani Dodoma.

Msaada huo ulikabidhiwa shuleni hapo juzi na kiongozi wa shirika hilo, Aisha Msantu na kuwataka wadau wengine kujitoa katika kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Msantu alisema kutokana na shule hiyo kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya madawati, shirika hilo limeamua kutoa mchango huo kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali katika utoaji wa elimu bila malipo na kuandaa viongozi bora kwa kuwapatia elimu inayokidhi mahitaji.

"Ili wanafunzi wapate elimu bora tumeamua kuanza kutatua changamoto katika sekta ya elimu na hapa ni mwendelezo wa mradi wetu wa 'Mimi kwa ajili yako' ukilenga kuwa suluhisho la changamoto katika jamii," alisema Msantu.

"Madawati haya tuliyotoa yana thamani ya Sh. milioni tano, lakini pia tumeamua kutoa taulo za kike boksi 10 hizi zitawasaidia wanafunzi kutokatisha masomo yao wakati wa hedhi badala yake watakuwa wanahudhuria masomo yao siku zote," alifafanua Masantu.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Fedha na Mpango, Dk. Ashatu Kijaji, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kondoa Vijijini, aliwataka wananchi kutowaficha watoto wenye ulemavu kwa kuwa wanamchango mkubwa katika jamii.

Alisema kila mtu ana haki ya kupata elimu bila kujali ulemavu alionao.

Alilishukuru shirika hilo kwa mchango huo katika jamii kwa kuwa lengo la serikali ni kutoa elimu bora kwa wananchi kwa kukabiliana na changamoto zilizopo katika sekta hiyo.

Awali Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Elizabeth Sanga, alizitaja changamoto zilizopo katika shule hiyo ikiwa ni pamoja na upungufu wa walimu wa masomo ya sanyasi, vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Sanga aliiomba serikali kuwaongezea walimu wa masomo hayo ili kumaliza changamoto hiyo.

# SIDO yaomba kiingilio 88 kupunguzwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO), mkoani Dodoma limewataka waandaaji wa maonyesho ya Nanenane kupunguza kiingilio katika maonyesho hayo ili watu waingie kwa wingi kupata elimu ya uzalishaji mbegu bora katika kilimo na ufugaji.

Pia katika maonyesho hayo watapata elimu juu ya uongezaji thamani ya mazao wanayolima kutoka kwa wataalamu wa Shirika hilo jambo ambalo litawasaidia kuzuia upotezaji wa bidhaa wanazolima.

Hayo yalisemwa na Ofisa uendelezaji biashara kutoka SIDO, Dodoma Crispin Kapinga, wakati akitoa maelezo kuhusu uongezaji thamani ya mazao mbalimbali katika maonyesho ya Nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Nzuguni jijini hapa.

Kapinga alisema wakulima wanapaswa kuingia katika maonyesho hayo ili kupata elimu ya kuongeza thamani ya mazao jambo ambalo litawapa faida kwa kile wanacholima au kufuga katika maeneo wanayotoka.

Crispini alisema SIDO iko katika maonyesho hayo ili kuhakikisha wanatoa elimu ya uongezaji thamani ya mazao ili kuhakikisha wajasiriamali wanapiga hatua kwa kile wanachofanya badala ya kubaki nyuma.

"Nawaomba waandaaji waliangalie kwa undani suala la kiingilio katika maonyesho yajayo ili kuisaidia jamii kuingia kwa wingi katika maonyesho hayo kwa sababu wanakwenda kufanya manunuzi na kujifunza," alisema Kapinga.

Alisema maonyesho ya Nanenane ni mujimu kwa wakulima, wafugaji na jamii kwa ujumla na wanapoingia kwa wingi inawasaidia kunufaika na elimu ya uzalishaji mbegu bora na uongezaji thamani wa mazao pia huchangia kuongeza soko kwa wajasiriamali kupitia bidhaa wanazonunua.

Kapinga alisema wananchi wengi wanashindwa kujitokeza kwa wingi kutokana na kiingilio kwa sababu wengi wao wanatoka maeneo ya nje ya Jiji la Dodoma na kulazimika kutumia fedha nyingi ili kufika katika maonyesho.

Aliwataka wakuu wa mikoa ya Dodoma na Singida kuweka mikakati ya shule za msingi na sekondari za mikoa hiyo kutumia viatu vya ngozi vinavyotengenezwa na wajasiriamali ili kusaidia kutangaza soko la wafanyabiashara hao.

Ofisa uendelezaji biashara huyo alisema bidhaa za ngozi zina thamani kubwa na wajasiriamali wa mikoa hiyo wameonyesha ubora katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

"Kuna kila sababu ya kufanya mchakato wa kuzishawishi shule za msingi na sekondari kutumia viatu vya ngozi mkifanya hivyo itakuwa mmewasaidia kwa kiasi kikubwa wajasiriamali," alisema Kapinga.

Alisema wajasiriamali wanapojiinua wanapaswa nao kupewa msaada wa kutafutiwa masoko ili waweze kuongeza thamani ya kile wanachofanya jambo litakalofanya waweze kupiga hatua zaidi katika utengenezaji wa bidhaa hizo.



# Meli kupunguza uhaba wa mafuta Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUPATIKANA kwa meli ya mafuta kutapunguza tatizo la uhaba wa mafuta Zanzibar na kuondoa usumbufu kwa watumiaji wa vyombo vya moto na wananchi kwa ujumla.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Aboud Jumbe, alisema tayari Zanzibar inameli ya mafuta ambayo imewasili juzi katika Bandari ya Malindi hivyo matarajio yake kuwa Zanzibar itaondokana na tatizo la uhaba wa mafuta ambao umekua ukijitokeza mara kwa mara.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasili kwa meli hiyo Ukombozi namba mbili, alisema imetengenezwa na kampuni ya kutengeneza meli ya Damian Ship iliyopo nchini Uholanzi.

Alisema meli hiyo inauwezo wa kubeba mafuta tani 3,500 ya dizeli, petroli, mafuta ya taa na mengine.

Alisema meli hiyo ya kisasa inauwezo wa kusafiri kokote duniani kutokana na viwango vilivyoundwa kuwa vya kimataifa.

Pia alisema ujio wa meli hiyo utasaidia kuondoa tatizo la uhaba wa mafuta kutokana na serikali kuendelea na mpango wake wa kuhamisha matangi ya mafuta yaliyopo Mtoni na kupelekwa Mangapwani, eneo lenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi matangi mengi.

Vile vile, alisema inampango wa kujenga bandari ya mafuta huko Mangapwani huku mpango huo ukifikia sehemu nzuri ili kuhakikisha uhaba wa mafuta Zanzibar unapungua au kumalizika kabisa.

"Meli hii ya kisasa ilianza kundwa mwaka 2017 na imegharimu kiasi cha Sh. bilioni 36 fedha hizo zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar," alisema Jumbe.

Alisema meli hiyo itakabidhiwa kwa Shirika la Meli Zanzibar ili iweze kujiendesha kibiashara kama ilivyo meli ya mafuta ya Ukombozi namba moja.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Meli Zanzibar, Salum Ahmada Vui, alisema meli hiyo itakuwa suluhisho la tatizo la uhaba wa mafuta ambalo mara kwa mara linajitokeza Zanzibar.

Alisema ana imani meli hiyo ya Ukombozi itaingiza mapato kutokana na kujipanga kuimarisha kibiashara zaidi.



Maofisa madini kutoka mikoa ya Mwanza na Shinyanga wakifungua dhahabu bandia zilizokuwa zikitumika kuwatapeli wafanyabiashara kutoka nje. Mwanza zilikamatwa dhahabu bandia kilo 6.255 na Shinyanga kilo 4.58. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Bil. 2/- kununua madawati shule za msingi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZAIDI ya Sh. bilioni mbili zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kununulia madawati kwa ajili ya shule za msingi Zanzibar, ili kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa madawati katika shule hizo.

Akizungumza wakati wa mkutano wa kujadili hatua iliyofikia ya makusanyo ya fedha za madawati hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya uhamasishaji ya upatikanaji wa madawati, Haroun Ali Suleiman, alisema kupitia fedha hizo, wanatarajia kununua madawati 14,065 ambayo yatakuwa ni awamu ya kwanza kwa shule za msingi.

Alisema tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeshatangaza tenda kwa kampuni mbalimbali na nne zimeshachaguliwa za nchini China na muda mfupi wataalamu watakwenda kukagua ili kujiridhisha viwango wanavyovihitaji kwa madawati hayo.

Haroun ambaye pia ni Waziri wa Katiba na Sheria alisema, wanatarajia ifikapo mwishoni mwa mwezi wa Desemba, mwaka huu hadi Januari mwakani, madawati hayo yatakuwa tayari yameshawasili nchini. Pia alisema hiyo ni miongoni mwa malengo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein, katika kuwasaidia wananchi wake hasa wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri na salama ili kupata wataalamu zaidi nchini.

"Nimshukuru sana Rais wa Zanzibar, kwa kuanzisha kamati hii ambayo imeisaidia Wizara ya Elimu ununuzi wa madawati kupitia michango ya wadau mbalimbali nchini ambayo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa," alisema.

Haroun aliwaomba wananchi wote wa Zanzibar kuendelea kushirikiana na kuhimizana kutoa michango mbalimbali ili kuwasaidia vijana wao waweze kusoma katika mazingira mazuri, juhudi hizo zimeonekana kwa kuweza kuongeza idadi ya ufaulu kwa wanafunzi katika ngazi mbalimbali nchini.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Madawati, Riziki Pembe Juma, aliitaka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kuhakikisha wanafanya maandalizi ya madarasa yatakayowekwa madawati hayo kutokana na usalama wa maeneo ya shule kwa kuwa zinaonekana baadhi yake hazipo salama kuwekwa madawati hayo.

Wajumbe wa kamati hiyo walishauri kuhakikisha ubora wa madawati yatakayonunuliwa yanakuwa na kiwango, kwa kuwa upo uwezekano wa kuchakachuliwa na kusababisha kuingia hasara baadaye.

# Madaktari bingwa wa Misri wawasili kutibu watoto

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

JUMLA ya madaktari bingwa wanane kutoka Chuo Kikuu cha Alexandria nchini Misri, wamewasili Zanzibar na wanatarajia kufanya upasuaji kwa watoto wenye matatizo mbalimbali ya kiafya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume baada ya mapokezi ya madaktari hao, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mohamed Haji Hamza, alisema kila mwaka hufika kambi ya madaktari hao kufanya huduma ya upasuaji kwa watoto.

Alieleza huduma za afya zitakazotolewa kwa watoto katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni wale wasiokuwa na sehemu ya kutoka haja kubwa na haja ndogo.

Pia alieleza kuwa zaidi ya watoto 200 wamefanyiwa upasuaji toka walivyoanza kuja mara ya kwanza mwaka 2013 hadi kufikia hivi sasa na ni mwendelezo wa huduma hiyo kupitia juhudi za serikali kuwasogezea wananchi matibabu karibu.

Vile vile, alisema wanatarajia kufanya upasuaji wa watoto 50 wenye matatizo hayo.

Aliwataka kuitumia vyema fursa hiyo kwa kuwaleta watoto wenye matatizo ili kufanyiwa huduma hiyo ambayo hutolewa bure huko Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja.

Naye Daktari kutoka Idara ya Upasuaji ya Watoto, Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mwanabaraka Saleh Haji, alisema lengo la madaktari hao kuja Zanzibar ni kufanya upasuaji kwa pamoja na madaktari wazalendo ili waweze kupata taaluma zaidi.

Kwa upande wake Daktari Bingwa na Mkufunzi Mkuu wa huduma ya tiba ya upasuaji wa watoto kutoka Chuo Kikuu cha Alexandria nchini Misri, Dk. Saber Waheeb, alisema ujio wao unatokana na urafiki uliopo baina ya Zanzibar na Misri na kufanya kazi kwa pamoja ili kukuza udugu huo.

# Wakulima wa alizeti walilia mikopo

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAKULIMA wadogo wa alizeti Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, wameiomba serikali kuwawezesha kupata mitaji na mikopo ambayo itawasaidia kufanya shughuli zao za kibiashara na kupunguza gharama za uzalishaji ambazo zitawafikisha katika uchumi wa kati.

Hayo yalibainishwa jana na Elizabeth Nguhi, mmoja kati ya wanakikundi cha Tumaini wanaojishughulisha na kilimo cha alizeti, mahindi na usindikaji wa mafuta ya alizeti wakati wa mahojiano na wanahabari waliotembelea maonyesho ya Nanenane yanayoendelea katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu

Mkulima huyo alisema wanategemea kufika mbali zaidi, ila wanakabiliwa na changamoto ya kifedha na uhalali wa umiliki wa ardhi, hali inayowafanya washindwe kufikia malengo yao licha ya kuwa wapo wadau waliojitokeza kuunga mkono jitihada zao.

"Matarajio yetu ni kufika mbali kati shughuli zetu za uzalishaji, lakini tunashindwa kutokana na kukosa mitaji na mikopo ya kutosha...serikali bado haijaweza kutusaidia na kuwekeza katika vikundi vya kilimo," alisema Eliza.

Eliza aliongeza kuwa mwaka huu wamejipanga kuhakikisha wanalima ekari tatu kupitia mbegu walizoziacha awali, huku akibainisha uwapo wa changamoto kubwa ya eneo ambapo wanalazimika kukodi shamba kwa kiasi cha Sh. 80,000 kwa ekari moja ili waweze kulima.

Meneja wa asasi isiyokuwa ya kiserikali katika miradi wa REDESO inayoshirikiana na OXFAM, Charles Buregeya, alisema wamefanikiwa kuwajengea uwezo wakulima wadogo wakiwa na lengo la kujikwamua kiuchumi.

Aliongeza kuwa asasi hiyo kwa Kanda ya Ziwa, wanafanya kazi katika Wilaya ya kishapu iliyopo mkoani Shinyanga na Wilaya ya Meatu iliyopo mkoa wa Simiyu ambapo katika kikundi cha Tumaini walikiwezesha shilingi 500,000.

Aidha, alisema miongoni mwa vikundi walivyovisaidia ni cha Tumaini ambacho walikiwezesha kupata mafunzo ya ujasiriamali, kupata mbegu bora za alizeti aina ya rekodi, vifungashio sambamba na kuwajengea uwezo juu ya kuongeza thamani ili waweze kukamua na kusindika mafuta.

# Rita kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi

**Na Salome Kitomari**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita), utaadhimisha siku ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu duniani, kwa kusajili na kukabidhi vyeti vya kuzaliwa kwa watu mbalimbali.

Sherehe hizo zitafanyika kesho jijini Dar es Salaam, na kwamba watakaofika kwenye sherehe hizo na hawana vyeti muhimu wataruhusiwa kufanya hivyo na wengine kukabidhiwa vyeti hivyo muhimu kwa maisha yao.

Kwa mujibu wa Meneja Masoko na Mawasiliano wa RITA, Josephat Kimaro, ni mara ya pili kwa maadhimisho hayo kufanyika nchini, na kauli mbiu ya mwaka huu ni cheti cha kuzaliwa kwa wote, msingi wa kulinda haki za binadamu na kukuza ujumuishaji.

Aidha, Waziri wa Katiba na Sheria, Augustine Mahiga, atakuwa mgeni rasmi na lengo kubwa ni kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanaandikishwa kwenye matukio muhimu ya binadamu.

"Kwa miaka kadhaa kumekuwa na juhudi mbalimbali za kuleta maboresho katika mifumo ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ambapo katika mkutano wa kwanza wa mawaziri wenye dhamana ya usajili wa umma uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwaka 2010, uliamua kuanzisha ushirikiano na kuunganisha juhudi za kuboresha mpango na mfumo wa usajili wa umma na Takwimu muhimu barani Afrika," alieleza Kimaro.

Alisema tangu uamuzi huo upitishwe mawaziri wamekuwa wakikutana kila baada ya miaka miwili, suala linaloonyesha utashi wa hali ya juu wa kisiasa wa nchi za Afrika na katika mkutano wa nne iliamriwa na kupendekezwa kwa siku ya maadhimisho hayo duniani.

"Katika kikao chake cha kawaida cha 32, kilichofanyika Januari 25-26, mwaka huu, Baraza Kuu la Umoja wa Afrika (AU) lilipitisha mapendekezo hayo yaliyotolewa na tamko la mkutano wa mawaziri, hapa nchini juhudi za kuimarisha mfumo wa usajili zilianza mnamo mwaka 2013 kwa kubuni mkakati wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu ambao umeanza kutekelezwa nchini," alibainisha.

Alisema hatua hiyo imeleta mafanikio chanya kupitia mipango mbalimbali iliyogawanyika kutokana na makundi ya umri.

"Vilevile, serikali imeanza mapitio ya sheria zinazoongoza usajili wa matukio haya ambazo zimepitwa na wakati hivyo kuwafanya wananchi kushindwa kusajiliwa ambapo kwa hapa nchini msimamizi mkuu akiwa Rita," alisema.



Mdau wa elimu nchini, Ndele Mwaselela, akikagua baadhi ya vyoo vya Shule ya Msingi Iziwa, jijini Mbeya juzi, ambavyo amevijenga kama sehemu ya jitihada zake za kuunga mkono serikali ya awamu ya tano ya kuinua ubora wa elimu hapa nchini. Mwaselela alitunukiwa tuzo na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kutambua mchango wake katika elimu Mkoa wa Mbeya. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumia mifugo ujenzi sekondari

**Na Sabato Kasika**

WAFUGAJI wa Kijiji cha Nyasaungu, Musoma Vijijini mkoani Mara, wameamua kutumia mifugo yao kuchangia ujenzi wa sekondari ya kijiji chao, zahanati na vyumba vya madarasa kwenye shule ya msingi.

Katika kuchangia maendeleo, wakazi wa kijiji hicho wamekubaliana kwamba michango yao kwenye miradi ya maendeleo itazingatia wingi wa mifugo alionayo mchangiaji.

Hayo yalisemwa na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, mara baada ya kumaliza kuendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa sekondari ya kijiji hicho juzi.

"Kwa mfano kwenye kila awamu ya mchango, wafugaji wenye ng'ombe zaidi ya 51, wanachangia Sh. 200,000 kila mmoja ili kufanikisha miradi ya maendeleo katika kijiji hicho," Prof. Muhongo.

Mbunge huyo alisema, kutokana na utaratibu huo wa uchangiaji, kijiji kina miradi hiyo mitatu, ambayo inaendelea kutekelezwa kwa wakati mmoja.

Kuhusu harambee alioifanya juzi, alisema ilianza na ya ujenzi wa sekondari ya Nyasaungu na kupata mifuko 67 ya saruji na nondo 27 kutoka kwa baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, huku akichangia mifuko 35 ya saruji.

"Kwa upande harambee ya ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho, nilichangia nondo 20 lakini kwa suala la saruji, ni kwamba nilishachangia mifuko 100, wanakijiji na viongozi wao walichangia nondo 20," alisema.

Alisema, kijiji cha Nyasaungu kiko Kata ya Ifulifuli, kwamba kata hiyo haina sekondari ya kata, ambapo wanafunzi wanatembea umbali usiopungua kilomita 3 kwenda kwenye sekondari za kata jirani.

"Sekondari za jirani za kata za Mugango na Nyakatende, kutokana na jiografia kama mito na mabonde ya Kata ya Ifulifu, wakazi wa vijiji vya Kabegi na Kiemba Kata ya Ifulifu wanajenga sekondari yao, huku wa kijiji cha Nyasaungu katika kata hiyo nao wakijenga ya kwao," alisema.

## HABARI KIMATAIFA

## Madaktari wakamatwa kwa kuhusika na mauaji

**KINSHASA,** Congo

MADAKTARI watatu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wanashikiliwa na maofisa wa usalama, baada ya kuhusishwa na kifo cha daktari wa Shirika la Afya Duniani (WHO), aliyekuwa anatoa tiba kwa wagonjwa wa ebola.

Kiongozi wa mashtaka wa kijeshi nchini DRC amethibitisha hilo baada ya kubainika kuwa daktari huyo, Richard Valery Mouzoko Kiboung raia wa Cameroon, aliuawa kwa kupigwa risasi Aprili baada ya watu wenye silaha kushambulia hospitalini mjini Butembo.

Madaktari wanaoshikiliwa watafunguliwa mashtaka ya ugaidi na upangaji wa uhalifu, baada ya maofisa wa usalama kusema kuwa walikuwa na ushahidi unaonesha kuwa madaktari hao wa DRC walikutana na kupanga kuuawa kwa daktari huyo wa WHO.

Daktari Mouzoko ni miongoni mwa maofisa wa afya waliotumwa na WHO katika mkoa wa Kivu Kaskazini, kusaidia kutoa matibabu kwa wagonjwa wa ebola tangu mwaka 2018, ugonjwa ambao umesababisha watu zaidi ya 1,800 kupoteza maisha hadi sasa.

Hata hivyo, kukamatwa kwa madaktari hao kumezua hasira miongoni mwa madaktari mjini Butembo ambao wametishia kugoma iwapo wenzao hawataachiliwa huru baada ya saa 48. **RFI**

## Boko Haram waua tena Maiduguri

**LAGOS,** Nigeria

WASHAMBULIAJI wawili wa kujitoa muhanga wameuawa watu watatu kwenye shambulio linalodhaniwa kuwa limefanywa na kundi la kigaidi la Boko Haram katika eneo la Kaskazini Mashariki mwa Nigeria.

Watu wengine wanane walijeruhiwa kwenye mashambulio mawili yaliyotokea katika Mji wa Mafa ulioko kilomita 50 kutoka kwenye mji wa Maiduguri ambao ni mji mkuu wa Jimbo la Borno, Kaskazini Mashariki mwa Nigeria.

Mkuu wa Kitengo cha Usalama wa Jimbo la Borno, Bello Danbatta, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa washambuliaji hao waliingia kwenye mji wa Mafa wakiwa miongoni mwa wanawake waliokuwa wamekwenda kutafuta kuni.

Kundi la Boko Haram linaloshukiwa kuhusika na mashambulio hayo limekuwa linafanya mashambulizi kwa kipindi cha miaka 10 sasa katika eneo hilo la Kaskazini Mashariki mwa Nigeria na mara nyingi limekuwa linawatumia wanawake kufanya mashambulio ya kujitoa muhanga katika maeneo kama vile misikiti, masoko na kwenye vituo vya usafiri. **DW**

# Polisi waomba radhi kwa 'kumburuza' mtu mweusi

**WASHINGTON,** Marekani

POLISI wa Jimbo la Texas nchini Marekani wameomba msamaha baada ya picha ya maofisa weupe wawili wakiwa wamepanda farasi wakiongoza mtu mweusi aliyeonekana amefungwa kamba hatua iliyozusha ukosoaji mkubwa kwenye mitandao ya kijamii.

Mkuu wa Polisi wa Galveston, Vernon Hale alisema mbinu hiyo ilikuwa inakubalika katika baadhi ya matukio, lakini maofisa hawakufanya uamuzi mzuri katika tukio hili.

Alisema hakuna nia mbaya na imebadilisha sera ya idara kuzuia utumiaji wa mbinu hiyo.

Watu wengi kwenye mitandao ya kijamii wamesema picha hiyo imeibua mawazo hasi kuhusu nyakati za utumwa.

Kulingana na habari iliyotolewa kutoka Idara ya Polisi ya Galveston, maofisa hao wawili ambao ni Brosch na A Smith, walimkamata Donald Neely baada ya kukiuka sheria.

**Hili lilikuwa kosa la kijinga. Ninachojua ni kwamba kama angekuwa mzungu, wasingetumia mbinu hiyo waliotumia kwa Neely.**

Polisi walieleza kuwa hakufungwa na kamba, lakini alikuwa amefungwa pingu mikononi na kamba ilikuwa imefungwa kwenye pingu.

Ilieleza kuwa: "Tunaelewa maoni hasi kuhusu hatua hii na tunaamini maoni haya yanafaa kabisa kukomesha utumiaji wa mbinu hii."

Hale alimwomba msamaha Neely kwa kudhalilishwa na kueleza kuwa wangeweza kusubiri usafiri katika eneo la kukamatwa.

"Tumebadilisha mara moja sera ya kuzuia matumizi ya mbinu hii na tutaangalia mafunzo na taratibu zote zilizowekwa kwa njia sahihi zaidi," alisema Hale.

Jarida la Houston lilieleza kuwa Neely aliachiwa kwa dhamana lakini hakuweza kupatikana kwa ajili ya kutoa maoni.

Leon Phillips, Mkurugenzi wa Masuala ya Sheria katika Kaunti ya Galveston, alieleza kuwa picha ambayo ilisambaa mitandaoni ilipigwa na mtu ambaye hakutaka kufahamika. Phillips alisema tukio hilo ni gumu kulizungumzia kama mkazi wa Galveston.

"Hili lilikuwa kosa la kijinga. Ninachojua ni kwamba kama angekuwa mzungu, wasingetumia mbinu hiyo waliotumia kwa Neely," alisema Phillips.

Alibainisha kuwa Neely ni mgonjwa wa akili, na maofisa walipaswa kusubiri bila kujali ni muda gani gari ingechukua kufika, kwani si kana kwamba wanalipwa baada ya kukamata.

Phillips alisema amepanga kutoa ombi la wazi katika ukumbi wa Jiji ili kuangalia sera za utekelezaji wa sheria.

"Mkuu wa polisi anasema hawakuvunja sera yoyote, lakini ni sera gani ya kusafirisha mfungwa? Ninajuaje kuwa sera hiyo haikuandikwa mnamo 1875? Kuna maswali mengi ambayo hayajajibiwa," alisema Phillips. **BBC**



Askari wa India wakiwa wameimarisha ulinzi kwenye mpaka wake na Pakistan. **PICHA: REUTERS**

## Pakistan yamtimua balozi wa India

**ISLAMABAD,** Pakistan

PAKISTAN imesema imemfukuza balozi wa India, Islamabad saa chache baada ya kupunguza hadhi yake ya kidiplomasia na biashara na India.

India imechukuwa hatua kuiondolea Kashmir utawala wa ndani, jimbo ambalo linagombaniwa na nchi hizo mbili.

Bunge la Pakistan lilipitisha azimio Jumatano kulaani hatua ya India.

Bunge hilo pia limeitaka India iondoe vikwazo vyote vya kiusalama ilivyoyiwekea Kashmir tangu Jumatatu.

Nchi jirani China na Pakistan ambazo zote zinadai eneo fulani la ardhi ya Kashmir limepinga vikali hatua ya India kuondoa madaraka ya kikatiba ambayo yanaruhusu Kashmir kutunga sheria zake yenyewe. **VOA**

## Trump atembelea majeruhi

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, alifuatana na mke wake Melania Trump jana kuwatembelea waathirika wa shambulizi la bunduki waliolazwa hospitalini katika majimbo ya Ohio na Texas.

Trump pia alipofika maeneo yalipotokea mashambulizi hayo katika mji wa Dayton na duka la Walmart katika mji wa El-Paso mahala ambapo watu wenye silaha waliua watu 31. Maeneo yote juzi yalijaa waandamanaji ambao walipinga Rais Trump kutembelea katika miji hiyo huku wakitoa wito wa kurejeshwa muswada wa kudhibiti bunduki. Wafuasi wa Rais Trump pia walikuwapo kwenye miji yote hiyo. **VOA**

# NMB yatoa mkopo wa bil. 40/- kwa wakulima pamba

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI



KATIKA kukuza sekta ya kilimo nchini, Benki ya NMB imetoa mkopo wa Sh. bilioni 40 kwa wakulima wa pamba, kwa ajili ya kukuza mitaji na kuendeleza mashamba yao.

Akizungumza jana katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima Nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Nyakabindi Wilaya ya Bariadi mkoani hapa, Ofisa Mkuu wa Wateja Wadogo na Wakati wa NMB, Filbert Mponzi (pichani), alisema mkopo huo wametoa kwa kampuni mbili kubwa za nchini.

"NMB tuko vizuri pesa tunayo, niwatakae wakulima hususan wa pamba waje katika benki yetu tuwape mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mikopo," alisema Mponzi.

Ofisa huyo alisema benki hiyo ina kitengo kinaitwa NMB Foundation kwa ajili ya wakulima kupewa mafunzo kabla ya kupatiwa mikopo hiyo, ili watakapopata fedha hizo wasizitumie vibaya.

Naye Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwataka wakulima kutumia fursa hiyo ya mikopo kukuza mitaji yao ili waweze kufanya kilimo chenye tija.

"Kwa kweli nimefurahi sana kusikia Benki ya NMB tayari, imeshatoa mikopo kwa wakulima wa pamba tena kwa riba nafuu, kwa hiyo hivi sasa kilimo cha pamba kitaweza kuchangia vizuri pato la Taifa," alisema Waziri Mkuu.

Aidha, Majaliwa aliwataka wanunuzi wakubwa wa pamba, waende kuchukua fedha NMB kwani pesa zipo, na kuwa waitumie benki hiyo kwa kuwa ni ya Watanzania, hivyo watu wajifunze kutumia vitu vya kwao.



Meneja Uhusiano wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), William Kallahge (kulia), na Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Ziwa, Josephat Mazumira, wakiwa wameshika kombe na cheti cha mshindi wa pili, baada ya kukabidhiwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (hayupo pichani), katika kilele cha Maonyesho ya Wakulima ya Nanenane Kitaifa, mkoani Simiyu jana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Kinamama wapaa kiuwekezaji korosho

**Na Gaudensia Mngumi**

WANAWAKE wakulima wa korosho wilayani Newala mkoani Mtwara wakiwamo wajane wameibuka kuwa wajasiriamali wakubwa baada ya kutumia mbinu za utafutaji na uwekezaji waliofundishwa na wadau wa utetezi wa maendeleo ya wanawake.

Zainabu Mohamed, Katibu wa Kikundi cha Wanawake cha Tukazane kilichoko Newala, alisema anawaongoza wanawake nane wanaounda kundi hilo, ambao kwa kutumia mafunzo na ushauri wameibuka kiuwekezaji wakiwa na uwezo wa kubangua korosho na kuziuza maeneo mbalimbali nchini.

"Tuna mpango wa kuanzisha kiwanda kidogo, japo mwanzo ni mgumu lakini tuna uwezo wa kubangua tani moja ya korosho kila msimu zinazotupatia wastani wa Sh. milioni 6.0," alisema Zainabu.

Katibu huyo alikuwa anazungumza na timu ya wanahabari iliyoongozana na Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirika la Action Aid Tanzania, Pauline Teveli, walipokitembelea kikundi hicho hivi karibuni kuona mafanikio.

Kwa mujibu wa Teveli, AATZ imekuwa bega kwa bega kusaidia maendeleo ya wanawake kwa kuwawezesha kujikomboa kwa kudai haki za kiuchumi, kijamii, ushirikishwa kwenye masuala ya maamuzi na kupambana na ukatili wa kijinisia uliokuwa umejikita katika wilaya nyingi za mkoa wa Mtwara.

Teveli alisema shirika limehamasisha na kuunganisha wanawake kwa kuunda vyombo vya umoja ikiwamo Shirika la Newala Women Rights Association (Newora) na Tandahimba Women Rights Organizations (Taworo) ambavyo vimewaunganisha, kutetea haki za kiraia na kiuchumi na kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Wakati wa ziara hiyo, Zainabu alisema mbinu za ujasiriamali na utafutaji walizofundishwa na shirika hilo zimewaibua na kuwaingiza kwenye kulima na kuuza korosho, kufuga kuku na kutengeneza batiki ambazo wanaziuza katika maonyesho ya Sabasaba na Nanenane na kwamba mwaka huu walishiriki kwenye maonyesho hayo.

Suwabu Msuweta, Mwenyekiti wa Kikundi cha Tukazane, alisema pamoja na kutumia mbinu za asili kubangua korosho, wameongeza mitaji kwa kukopa na kujiunga na chama cha ushirika cha wanawake cha kuweka na kukopa kupitia Newora.

Alieleza kuwa wanawake wamebadilika kiuwekezaji na wamepata hamasa za ujasiriamali, wanathubutu na lengo lao ni kuwa mfano wa wanawake kimaendeleo wilayani Newala.

# Wanafunzi wanufaika na masomo ya bure

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 64 wananufaika na mpango wa shule ya Patrick Mission wa kusomesha bure wanafunzi ambao wanatoka kwenye kaya zisizo na uwezo.

Hayo yalisemwa jana shuleni hapo na Mkurugenzi wa shule hiyo, Ndele Mwaselela wakati akizungumzia mpango wa shule yake kusaidia wanafunzi wasiojiweza kupata elimu.

Alisema aliamua kuchukua uamuzi huo baada ya kuombwa na viongozi wa Wilaya na madiwani mkoani Mbeya anakotoka kusomesha wanafunzi ambao wanatoka kaya zisizo na uwezo.

"Waliniomba nikakubali na hivi sasa wako 64, nilikubali kwasababu nataka kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano ambayo imeamua kutoa elimu bure ili watoto wa kaya maskini nao wapate elimu," alisema na kuongeza.

"Nimeamua kufanya hivi kama jitihada za kumuunga mkono Rais wetu John Pombe Magufuli katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora na jitihada hizi zimechangia mimi kupewa tuzo na Ofisi ya Rais Tamisemi kutambua mchango wangu wa kuinua elimu Mkoa wa Mbeya," alisema

Alisema jitihada zake za kuhakikisha Mkoa huo unainuka kielimu zilisababisha Ofisi ya Rais Tamisemi imtunukie tuzo nyingine mwaka jana hali ambayo alisema imemwongezea ari ya kuzidi kuusaidia Mkoa huo.

Mwaselela alisema yeye kama mdau wa elimu amekuwa akisaidia kuboresha miundombinu kwenye shule mbalimbali mkoani Mbeya na nje ya Mkoa huo kwa kukarabati na kujenga madarasa, kukarabati vyoo na kujenga vyoo vipya.

Alisema amejenga vyoo katika shule ya msingi Mapambano jijini Mbeya, Shule ya Msingi Iyela ambako amewajengea vyoo vipya na shule ya sekondari Ikuti wilayani Rungwe .

Alisema kila mwaka shule hiyo imekuwa ikitoa wanafunzi wengi wanaosoma bure kwenda kidato cha tano na vyuo vikuu na kwamba utaratibu huo umekuwa endelevu.

"Kuitwa mdau wa elimu kumetokana na jitihada kubwa ninazofanya kwenye kuinua elimu kwenye masuala ya elimu tunafanya vizuri na kwenye jamii nako tunafanya vizuri zaidi kwa kuhakikisha shule nchini zinakuwa na vyoo vya kisasa na madarasa ya kisasa," alisema.

Mwaselela alisema hivi sasa yuko katika kampeni ya kuboresha ufaulu wa

Mkoa wa Mbeya kwa kuwapa walimu mitihani ya kuinua viwango vyao ili mwisho wa siku Mkoa huo uongoze kitaifa kwenye matokeo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**ANAHITAJIKA MHASIBU SIFA:** MWANAMKE ELIMU: DIPLOMA MAWASILIANO: 0715 885533 / 0752 610700.

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0767 223 311*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SANE AZUA HOFU CITY, BAYERN MUNICH




**MANCHESTER,** England

LEROY Sane wa Manchester City ambaye amekuwa akiwaniwa na Bayern Munich ameibua wasiwasi baada ya kuonekana ameumia zaidi tofauti na ilivyotarajiwa awali.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wameachwa na mshituko kwa mchezaji huyo ambaye ametajwa kuwa thamani yake ni pauni milioni 135, ambaye amekataa kusaini mkataba mpya hapo kwenye dimba la Etihad.

Hali ya Sane inaonekana kuwa tofauti na ilivyotarajiwa, kwani awali alipoumia goti katika mchezo wa Ngao ya Jamii, ilionekana angepona haraka, lakini sasa inaonekana kuwa ni mbaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 aliondoka kwenye uwanja wa Wembley akichechemea baada ya kugongana na mchezaji wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold Jumapili iliyopita.

Awali kulikuwa na matumaini kwamba tatizo lake hilo lingeweza kumalizika kwa kipindi cha wiki moja tu, lakini baada ya vipimo vilivyofanyika Jumatano, inaonyesha kwamba ameumia vibaya.

Na sasa majaliwa ya Sane yako shakani, huku klabu hizo mbili bado zikiwa kwenye machakato wa kufikia makubaliano ya kuuziana nyota huyo.

# Dili la Dybala kutua Spurs lavunjwa

**LONDON,** England

MPANGO wa Klabu ya Tottenham kutaka kumsajili winga wa Juventus, Paulo Dybala umeshindikana.

Spurs ilikuwa katika harakati za kutaka kukamilisha usajili wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina jana siku ambayo ilikuwa ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili ligi Kuu England, lakini mpango huo ukafutwa mapema asubuhi.

Kwa mujibu wa BBC Sport, Juventus ndio waliositisha mpango huo baada ya kubadilisha maamuzi na kuamua kumbakisha kikosini mwao.

Awali Spurs walifikia makubaliano na Juventus ya kumsajili Dybala kwa pauni milioni 69, lakini bado maslahi binafsi ya mchezaji huyo yalikuwa hajafikiwa.

Dybala alikuwa anataka kulipwa pauni 300,000 kwa wiki, kiasi ambacho kimezidi kile anacholipwa nahodha wa timu hiyo, Harry Kane pauni 200,000 kwa wiki.

Dybala mwenyewe licha ya kupewa muda zaidi wa kufikiria kuhusu mpango huo wa kuuzwa kwenda jijini London, lakini alionekana anataka kubakia nchini Italia.

Dybala alifunga bao katika mchezo wa kirafiki wa Jumatano dhidi ya Novara, ambayo inaheza daraja la tatu maarufu Serie C.






# *Barcelona yarudi kuipiku Real Madrid kwa Neymar*

**MADRID,** Hispania

BARCELONA ipo tayari kutoa ofa nyingine ili kuipiku Real Madrid ambayo nayo imeripotiwa kuingia kwenye mbio za kutaka kumsajili Neymar, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Nyota huyo wa klabu ya Paris Saint-Germain amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kipindi hiki cha majira ya joto kwa madai kwamba hana furaha nchini Ufaransa.

Barcelona imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumchukua tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, lakini Real Madrid iliingilia kati kwa kubainisha kuwa ipo tayari kutoa pauni milioni 111 pamoja na mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, Luka Modric ili Los Blancos wamsajili na kuwapiku wapinzani wao hao.

Hata hivyo, Barcelona miamba ya Katalunya baada ya juzi kudai haina mpango wa kumsajili mchezaji huyo, lakini ripoti za jana Alhamisi zilisema kuwa wamerudi kwa kasi kuhakikisha Neymar anatua pale Nou Camp.

Philippe Coutinho anaweza kutumika kama mbadala wa kumrudisha Neymar pamoja na kiasi ambacho Real Madrid wamekitangaza cha pauni milioni 111.

Neymar alijiunga na PSG kutoka Barcelona mwaka 2017 kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 198.

Winga huyo tangu atue pale PSG amefunga mabao 51 katika mechi 58 na kutoa pasi za mwisho 29.

Hata hivyo, licha ya kushinda taji la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika misimu yote aliyokaa na klabu hiyo, Neymar anataka kuondoka pale PSG.

# Balotelli mbioni kutua Flamengo

**SAO SAULO,** Brazil

MARIO Balotelli yupo kwenye mazungumzo ya kusajiliwa na klabu ya Flamengo ya nchini Brazil kwa dau la euro milioni 15 kwa mkataba wa miaka miwili na nusu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa sasa hana klabu baada ya kumaliza muda wake na Marseille mwanzoni mwa kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport, kwa sasa yupo kwenye mazungumzo ya mwisho kutua kwa miamba hao wa Amerika Kusini ambako anatarajiwa kusaini mkataba utakaomuweka hadi Desemba mwaka 2021.

Akiwa kama mchezaji huru, Balotelli anatarajiwa kusaini kwa mshahara wa euro milioni 4.5 kwa mwaka.

Ukijumlisha mshahara pamoja na bonasi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ataingiza kiasi cha pauni milioni 14 kwa kipindi chote atakachokaa nchini Brazil.

West Ham pia ilitoa ofa ya kutaka kumsajili Balotelli mwezi uliopita baada ya kushindwa kuwapata Maxi Gomez na Callum Wilson wa Bournemouth.

Balotelli aliichezea mechi 15 Marseille huku akifunga mabao nane kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Kabla ya kutua Marseille, Balotelli alicheza Nice chini ya kocha Patrick Vieira ambako alifunga mabao 43 katika mechi 76.





# LUKAKU ATUA INTER MILAN

**MILAN,** Italia

KLABU za Inter Milan na Manchester United zimeafikiana kuhusu usajili wa mshambuliaji, Romelu Lukaku.

Inter sasa itatoa kitita cha pauni milioni 74, dau ambalo Man United walikuwa wakilitaka toka awali.

Mapema Julai mwaka huu, United ilikataa dau la pauni milioni 54 kwa ajili ya usajili wa Lukaku kwenda Inter.

Lukaku alipigwa faini na United baada ya kukacha mazoezi ya timu hiyo bila ruhusa ya uongozi, ikiwa ni sehemu ya jitihada zake kuchochea uhamisho.

Mchezaji huyo amekuwa akifanya mazoezi na klabu yake ya zamani Anderlecht kwa siku mbili zilizopita.

Wakala wa Lukaku, Federico Pastorello, alilazimika kwenda jijini London juzi ili kukutana na wawakilishi wa Man United ili kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Usiku wa jana, Pastorello alituma picha katika mtandao wake wa Instagram akiwa kwenye ndege na Lukaku na kuandika maelezo yafuatayo: "Tayari kwa kupaa. Muelekeo Milano."

Inter na United wamekuwa wakivutana kwa wiki kadhaa juu ya thamani halisi ya mchezaji huyo, huku United ikitaka walau kurejesha pauni milioni 75 ambazo walitumia kumsajili miaka miwili iliyopita, na sasa wamefanikiwa.

Kocha wa Inter, Antonio Conte alitangaza toka awali kuwa Lukaku ndiye kipaumbele chake cha kwanza kwenye dirisha hili la usajili. "Ninamchukulia kama mchezaji ambaye anaweza kuboresha kikosi chetu," amesema Conte.

Lukaku alihamia United mwaka 2017 akitokea Everton huku kukiwa na shauku kubwa juu ya kipaji chake na mchango wake kwenye timu hiyo.

Wakati huo, alikuwa ni mchezaji wa nne wa chini ya miaka 24 kufunga magoli zaidi ya 80 katika ligi ya England. Wengine ni Wayne Rooney, Robbie Fowler na Michael Owen.

Katika msimu wake wa kwanza Old Trafford, Lukaku alifunga magoli 27, hata washambuliaji hatari wa zamani wa klabu hiyo kama kocha wa sasa Ole Gunnar Solskjaer, Cantona na Andy Cole hawakupata mafanikia ya namna hiyo kwenye msimu wa kwanza, maana wote walifunga magoli 25.

# Arsenal yamchukua rasmi Tierney

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Celtic, Kieran Tierney kwa pauni milioni 25.

Beki huyo wa kushoto alikuwa akiwaniwa kwa muda mrefu na Arsenal kwa kipindi hiki cha majira ya joto, na sasa dili hilo limeonekana.

Tierney jana Alhamisi alitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya, kabla ya kufikia saa ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la usajili kwa Ligi Kuu England.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 ambaye ameichezea timu ya taifa ya Scotland mechi 12 alitarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano kucheza hapo kwenye dimba la Emirates.

Arsenal imekuwa na uhitaji wa beki wa kushoto kwa ajili ya kuwasaidia Nacho Monreal na Sead Kolasinac ambao wamekuwa wakipigania kuwa kwenye ubora.

Arsenal tayari imewasajili Nicolas Pepe, Gabriel Martinelli, Dani Ceballos na William Saliba kipindi hiki cha majira ya joto, pamoja na beki David Luiz ambaye jana alitarajiwa kukamilisha uhamisho wake.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LUIZ AAMKIA ARSENAL

## Tuna mabeki wengi, lakini imekuwa tofauti wakati Koscielny alipotuambia anaondoka...

**LONDON,** England

ARSENAL jana ilikubali kutoa dau la pauni milioni nane Chelsea ili kuipata saini ya beki Mbrazil David Luiz kwa mkataba wa miaka miwili.

**Beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 32 kwa sasa, ambaye alitia saini mkataba wa miaka miwili Chelsea Mei mwaka huu, jana mchana alitarajiwa kupimwa afya Arsenal.**

Jumanne, Arsenal ilimuuza Laurent Koscielny kwa Bordeaux ya Ufaransa kwa dau la euro milioni tano (sawa na pauni milioni 4.6), pia jana miamba hiyo ya Emirates ilikamilisha usajili wa beki wa kushoto wa Celtic, Kieran Tierney kwa pauni milioni 25.

Luiz Jumatano alijifua pekee yake mbali na wachezaji wengine wa kikosi hicho cha Frank Lampard.

Kocha Mkuu wa Arsenal, Unai Emery aliiambia Sky Sports News anataka kusajili beki wa kati kabla ya dirisha la usajili England kufungwa jana na inatambukika Luiz alikuwa katika orodha yake.

"Kama tunaweza tu siku ya mwisho, tutajaribu kusajili beki wa kati, lakini mmoja mwenye uwezo wa kutusaidia," alisema Emery juzi.

"Tuna mabeki wengi. Pengine, ni tofauti wakati Laurent Koscielny alipotuambia anataka kuondoka.

Luiz ameitumikia Chelsea kwa miaka sita na nusu katika vipindi viwili na aliichezea mechi 160 za Ligi Kuu akifunga mabao 11.

Endapo jana angethibitishwa kuondoka, itakuwa ni wiki tano baada ya Lampard kurudi Stamford Bridge kama kocha.

Chelsea imefungiwa kusajili mchezaji yeyote hadi mwishoni mwa Januari 2020 kufuatia kubainika kusajili kinda wa kigeni mwenye umri chini ya miaka 18.

Na wakati Gary Cahill, ambaye tangu amejiunga na Crystal Palace, aliondolewa mwishoni mwa msimu uliopita, mbadala wa Chelsea katika beki ya kati wamekuwa ni Mjerumani Antonio Rudiger, Kurt Zouma, aliyekuwa akicheza kwa mkopo Everton msimu uliopita, na Mdennmark Andreas Christensen.

Alisajiliwa Chelsea kutoka Benfica kwa pauni milioni 21 Januari 2011, na kisha Luiz alijiunga na Paris St-Germain kwa pauni milioni 40 Juni 2014 kabla ya kurudi Stamford Bridge Agosti 2016 kwa pauni milioni 34.

Jumatano Luiz alikuwamo katika uwanja wa Chelsea wa mazoezi wa Cobham, ingawa hakuwa sehemu ya wachezaji wa kikosi cha kwanza.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR AGEUKIWA MADRID

REAL Madrid imefungua mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya straika Mbrazil Neymar, 27. ***(Sky Sports)***

### COUTINHO CHANGAMOTO BARCA

MATUMAINI ya Barcelona kumsajili kwa mara nyingine Neymar, 27, yanategemeana na klabu hiyo kumuuza kiungo wa Mbrazil Philippe Coutinho. ***(Goal)***

### WILLIAMS ATENGWA UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kulipa pauni milioni 81 zinazotakiwa kuvunja mkataba wa mshambuliaji wa Athletic Bilbao na Hispania, Inaki Williams, 25. ***(El Chiringuito TV - via Mail)***

### GOTI LAMZUIA SANE BAYERN

SUALA la Leroy Sane, 23, kuchomoka Manchester City na kutua Bayern Munich limekuwa na utata kutokana na Mjerumani huyo kuwa majeruhi wa goti. ***(Mail)***

### ZAHA AILAZIMISHA PALACE

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 26, jana alipeleka ombi la kutaka kuondoka, wakati akijaribu kulazimisha kujiunga na Everton. ***(Express)***

### AKE, TOMORI KWA EVERTON

EVERTON jana ilitarajiwa kumfuata beki wa Chelsea na England U-21, Fikayo Tomori, 21, na beki wa kati wa Bournemouth, Mholanzi Nathan Ake, 24. ***(Sun)***

### AMFUATA DRINKWATER

BURNLEY katika dakika za mwisho jana kabla ya dirisha la usajili kufungwa ilitoa ofa ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa Chelsea, Danny Drinkwater, 29. ***(Mail)***

### CARSON ANUKIA MKOPO CITY

KIPA wa zamani wa England, Scott Carson, 34, alitarajiwa kujiunga na Manchester City Derby kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu. ***(Sun)***

### ATLETICO YAMFUATA ERIKSEN

ATLETICO Madrid inajiandaa kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, 27. ***(Independent)***

### KHEDIRA AISUBIRI ARSENAL

KIUNGO wa Juventus, Sami Khedira, 32, alikataa ofa mbili kwa sababu alikuwa akisubiri nafasi ya kujiunga na Arsenal. ***(Star)***

### MONACO YAMTAKA SHAQIRI

MONACO ipo tayari kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Uswisi, Xherdan Shaqiri, 27. ***(Blick)***

### YAKUBALIWA KWA PRAET

LEICESTER imekubaliana na Sampdoria dili la kumsajili kiungo Mbelgiji Dennis Praet, 25. ***(Mail)***



HABARI MICHEZO

## Azam dozi mara mbili Ethiopia

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya juzi kuwasili salama nchini Ethiopia, wawakilishi wa Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC wameendelea kujiweka sawa kwa kujifua asubuhi na jioni tayari kwa mechi yao dhidi ya Fasil Ketema (Ethiopia 1) itakayopigwa Jumapili mjini Gondar Kaskazini mwa nchi hiyo.

Azam iliamua kwenda mapema ikiwa ni siku nne kabla ya mchezo wao kwa lengo la kuzoea hali ya hewa ya huko ambayo inaelezwa kwa sasa ni baridi kali.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya barua pepe kutoka nchini Ethiopia, Ofisa Habari wa timu hiyo, Jafari Iddi Maganga, alisema, licha ya hali ya baridi, kikosi chao kipo salama na katika mazoezi ya timu hiyo, hakuna mchezaji aliyeonekana kusumbuliwa na hali ya hewa ya Ethiopia.

"Tunashukuru tupo salama leo (jana), tumefanya mazoezi asubuhi na jioni pia tutaendelea kujifua kila siku hadi siku ya mechi kulingana na programu aliyojiwekea kocha wetu Etienne Ndayiragiji," alisema Maganga.

Aidha, alisema kwa mujibu wa kocha huyo mikakati yake ni kuanza kwa ushindi ugenini licha ya kwamba wanatarajia kupata ushindani mkubwa.

"Kocha wetu ameahidi kufanya vizuri kutokana na jinsi alivyokiandaa kikosi chake, kikubwa anaomba dua zenu huko nyumbani," alisema Maganga.

## Judo wa3 kufuata All Africa Games

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI watatu wa mchezo wa Judo wanatarajiwa kuingia kambini Jumatatu ijayo kujiandaa na safari ya kuelekea Morocco Jumatano kushiriki mashindano ya All Africa Games yatakayoanza kurindima nchini humo kuanzia Agosti 16-30, mwaka huu .

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Judo Tanzania (JATA), Innocent Mallya alisema wachezaji wamejiandaa kwa muda mrefu kwa kufanya mazoezi kwa ajili ya michuano hiyo.

"Wachezaji wetu tumewaandaa kwa muda mrefu, hivyo hatuna shaka na mashindano hayo," alisema Mallya.

Aliongeza kuwa, timu hiyo itaondoka ikiwa na wachezaji watatu pamoja na kocha mmoja.

Aliwataja wachezaji watakaondoka siku hiyo kuwa ni Anangise Pwele, Abdulrabi Alawi pamoja na Hamis Salim.

"Tunaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuiunga mkono timu yetu ambayo inakwenda kuwakilisha huko Morocco," alisema Katibu huyo.

# KAHATA: KWA SIMBA HII, MASHABIKI MTAIPENDA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia 'nyomi ya kufa mtu' Uwanja wa Taifa wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Power Dynamsos ya Zambia, kiungo mshambuliaji mpya wa Simba, Mkenya Francis Kahata, amewataka mashabiki wa klabu hiyo kuendelea kuisapoti timu yao ili iendelee kufanya makubwa zaidi.

Mashabiki wa Simba, Jumanne wiki hii walijitokeza kwa wingi na kufanikiwa kuujaza Uwanja wa Taifa huku wengine wakilazimika kuwekewa TV katika Uwanja wa Uhuru ili kushuhudia kilichokuwa kikiendelea siku hiyo ya kilele cha Simba Day, ambayo waliitumia kutangaza nyota wao wa msimu mpya pamoja na kucheza mechi hiyo ya kirafiki.

**Akizungumza baada ya mechi hiyo, Kahata alisema anaamini kutokana na ubora wa wachezaji wanaounda kikosi hicho, wanaweza kufika mbali kwenye michuano ya kimataifa na kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu Bara.**

"Kinachotakiwa ni kuendelea kushirikiana na kucheza kitimu, pia mashabiki wasichoke kutuunga mkono ili kutupa hamasa kufanya vizuri katika mechi zetu kama walivyofanya leo (Jumanne)," alisema.

Kahata ambaye amesajiliwa msimu huu akitokea Gor Mahia, wakati akiitumikia timu hiyo ya Kenya akiwa na Mnyarwanda Meddie Kagere, walitengeneza ushirikiano mzuri na kuifanya safu yao ya ushambuliaji kuwa tishio na kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Kenya.

Na kwa muda mrefu, Kagere alikuwa akitamani nyota huyo kusajiliwa Simba ili waweze kuendeleza ushirikiano wao wa kucheka na nyavu, jambo ambalo mashabiki wa Wekundu wa Msimbazi hao wanasubiri kuliona likitokea.

Simba ambayo msimu uliopita ilifika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), ilitarajiwa kuondoka leo asubuhi kwa ndege ya kukodi kuelekea Msumbiji tayari kwa kuanza kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi kwa kuivaa UD Songo kwenye mechi ya raundi ya awali.



Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, akizungumza na wachezaji wake wakati wa mapumziko kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Mlandege iliyopigwa Uwanja wa Amaan juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# *Zahera aukubali mchakamchaka wa Mlandege*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Yanga, Mwinyi Zahera amekisifu kikosi cha timu ya Mlandege kwa kucheza soka kwa kasi pindi wanapokuwa na mpira.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kumalizika mchezo wa kirafiki kati ya timu yake na Mlandege na kutoka na ushindi wa mabao 4-1 mchezo uliopigwa katika dimba la Amaan mjini hapa, Zahera alionyesha kuvutiwa na namna wapinzani wao walivyocheza licha ya kupoteza mechi hiyo.

Alisema kasi waliyonayo Mlandege imewapa mazoezi na maandalizi mazuri kuelekea mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Township Rollers ya Botswana, utakaopigwa Uwanja wa Taifa Jumamosi kwani kwa muda wote wapinzani wao walikuwa hawakubali mpira utulie.

Alisema licha ya mbio zao katika mchezo huo, lakini walishindwa kupachika mabao na badala yake wachezaji wake waliweza kutumia vema nafasi walizozipata kupachika mabao hayo na hatimaye kuibuka na ushindi.

Akizungumzia kutohudhuria mazoezini baadhi ya wachezaji wake wa kikosi hicho, alisema jambo hilo haliwezi kumkosesha usingizi.

"Kama mchezaji anakosa kwenda mazoezini hawezi kunikosesha usingizi, kwani kikosi kina wachezaji ambao viwango vyao vinakaribiana hivyo siku atakayokuja mazoezini atakuta timu imesonga mbele," alisema.

Kwa upande wa kocha wa Mlandege, Sheha Khamis, alisema kufungwa kwao kulitokana na kutojiandaa mapema lakini kikosi cha Yanga nacho kilikuwa kizuri zaidi yao.

Naye kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto' alisema mchezo huo umewapa mazoezi yakutosha kuelekea mechi yao ya kesho ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunakabiliwa na michuano ya Ligi ya Mabingwa, kwa hiyo mchezo huu umetupa mazoezi hususan katika kasi ya kukimbia.

Katika mechi hiyo mabao ya Yanga yalifungwa na Mnyarwanda Patrick Sibomana dakika ya 26, Mganda Juma Balinya dakika ya 36, Mnamibia Sadney Urikhob dakika ya 43 na Mtanzania Mrisho Ngasa dakika ya 65, huku bao pekee la Mlandege likipachikwa na Hassan Bamzu dakika 88.

Michezo
Ijumaa Agosti 9, 2019
Nipashe



Luiz aamkia Arsenal

UKURASA 30



Kikosi cha Yanga

## Simba bila Manula, Ajibu kwa UD Songo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ilitarajiwa kukwea pipa binafsi la kukodi leo asubuhi kuelekea Msumbiji tayari kwa mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo, nyota watatu wa kikosi hicho imeelezwa hawatakuwapo katika msafara huo kutokana kuwa majeruhi.

Wachezaji ambao walielezwa katika taarifa ya Simba jana kuwa hawatasafiri na timu ni kipa Aishi Manula, kiungo Ibrahim Ajibu na mshambuliaji Mbrazil Wilker Henrique da Silva.

Hata hivyo, nahodha wa Simba, John Bocco, amesema hawana wasiwasi kwa kuwa wanatambua kazi kubwa iliyopo mbele yao ni kupambana kupata matokeo kwenye mchezo huo wa kimataifa.

"Kazi kubwa ni kimataifa na kila mchezaji anajua jukumu lake jipya na namna ambavyo anapaswa kufanya, mashabiki wanapenda kuona timu inapata matokeo na sisi tunakwenda kupambana kwa ajili yao na Taifa," alisema.

Naye beki kisiki wa timu hiyo, Shomari Kapombe, alisema kwa sasa yupo fiti na anatumai kufanya vizuri ndani ya Simba kwenye michuano ya kitaifa na kimataifa.

# Yanga: Waleteni, tumeiva

## Township Rollers yawawahi Dar, Sibomana azidi kutisha kwa nyavu, yavuna Sh. milioni 283 Taifa, Simba Sh. milioni 376 kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

YANGA imekamilisha programu yake ya mazoezi visiwani Zanzibar kuelekea mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana itakayopigwa Uwanja wa Taifa kesho na kueleza sasa mambo ni moto na ipo tayari kwa mechi hiyo ya kimataifa.

**Baada ya kuhitimisha kilele cha Wiki ya Mwananchi Jumapili kwa kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya katika Uwanja wa Taifa, Yanga ilielekea Zanzibar kuweka kambi ya muda mfupi na kucheza mechi mbili za kirafiki ikianza na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Mlandege juzi kabla ya jana usiku kuhitimisha kwa kuvaana na Malindi FC kwenye dimba la Amaan.**

Kwa mazoezi waliyoyapata, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, alinukuliwa akieleza kuwa hana wasiwasi na kikosi chake kwa sasa na anaamini kitampa matokeo chanya kimataifa.

Zahera alisema anaona namna kikosi chake kilivyozidi kuimarika baada ya mechi yake dhidi ya Kariobangi Sharks na ile ya Mlandege, hivyo ana anaimani kitapata matokeo chanya kwenye michezo ya kimataifa.

"Kwa tulipofikia si sehemu mbaya, kila mmoja ana morali ya kufanya kazi na kutimiza majukumu yake uwanjani.

"Tunatambua kwamba ipo kazi ya kucheza kimataifa, hilo halitupi taabu tumejiandaa na mashabiki watupe sapoti ili tufanye vizuri," alisema.

Akizungumzia mechi dhidi ya Mlandege, ambayo walishinda mabao 4-1 juzi, Zahera licha ya kuvutiwa na namna wapinzani wao walivyocheza kwa kasi licha ya kupoteza, alisema walipata mazoezi mazuri kutokana na kasi ya wapinzani hao.

Alisema kasi waliyonayo Mlandege imewapa mazoezi na maandalizi mazuri kuelekea mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Township Rollers.

Katika mechi hiyo, Yanga ilipata mabao yake kupitia kwa nyota wa kigeni, Mnyarwanda Patrick Sibomana dakika ya 26, hilo likiwa ni bao lake la pili tangu ajiunge na Yanga, la kwanza likiwa ni dhidi ya Kariobangi Sharks alilofunga kwa mkwaju wa penalti.

Mabao mengine yalifungwa na Mganda Juma Balinya dakika ya 36, Mnamibia Sadney Urikhob dakika ya 42 na mzawa Mrisho Ngassa dakika ya 65, huku bao pekee na la kufutia machozi la Mlandege likifungwa na Hassan Bamzu dakika ya 88.

Katika hatua nyingine, wakati Yanga ikitarajiwa kurejea jijini Dar es Salaam leo ikitokea Zanzibar, wapinzani wao kimataifa, Township Rollers walitarajiwa kutua nchini jana tayari kwa mechi hiyo ya Jumamosi.

Yanga ikipata matokeo ya jumla katika mechi hiyo na ile ya marudiano itakayopigwa nchini Botswana kati ya Agosti 23-25, mwaka huu, itakutana na mshindi kati ya Green Mamba ya Eswatini na Zesco ya Zambia.

Wakati huo huo, kwa mujibu wa taarifa zilizolifikia Nipashe jana, Yanga imefanikiwa kuingiza Sh. milioni 283 na ushee katika kilele cha Wiki ya Mwananchi, fedha hizo zikitokana na kiingilio cha idadi ya mashabiki 48,630 walioingia uwanjani siku hiyo.

Wakati Simba yenyewe ikivuna Sh. milioni 376 na ushee kutokana na mashabiki 58,001 walioingia Uwanja wa Taifa kilele cha Simba Day juzi Jumanne.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >